**4 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 4 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. LEAH J. KOMANYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushotosasa aulize swali lake.

Na. 498

### Ukarabati wa Shule Kongwe za Makanya na Kwai

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itazipatia fedha za ukarabati Shule Kongwe za Msingi Makanya na Kwai katika Jimbo la Lushoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Makanya imechakaa kiasi cha kutokarabatika. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imetenga shilingi milioni 424.7 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mipya ambapo hadi Mei, 2025 shilingi milioni 96 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu ya vyoo kumi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Shule ya Msingi Kwai imetengewa shilingi milioni 202.2 kupitia Mradi wa *BOOST* kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu chakavu na ujenzi

wa vyumba vitatu vya madarasa na matundu ya vyoo kumi na mawili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za kukarabati au kujenga miundombinu mipya katika shule kongwe na chakavu kote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaishukuru Serikali nimeona kweli fedha zile zimefika na kazi imeshaanza.

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili; Shule za Msingi Kwemashai, Mshezee, Chumbageni, Mazumbai na Mkuzi nazo zimechakaa mno. Je, Serikali haioni sasa kuna ulazima wa kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kukarabati shule hizi kwa pamoja? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali haioni kwamba kuna lazima sasa za kujenga nyumba za walimu ili kuondoa changamoto zetu za walimu hawa kwa ajili ya kukaa karibu na vituo yao vya kazi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba shule ambazo Mheshimiwa Shekilindi amezitaja, Shule ya Chumbageni, Kweshai na nyingine ambazo amezitaja ni shule kongwe na chakavu ambazo zinahitaji kufanyiwa ukarabati, lakini pia ujenzi wa miundombinu mingine mipya. Ninaomba nimuhkikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja ya vipaumbele vya Serikali kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Shule za Msingi *(BOOST)* ni kuendelea kuzitambua kwanza shule chakavu, lakini pia kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati. Shule hizo tayari tumezitambua na tumeziingiza kwenye mpango wa kwenda kuzikarabati kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili kuhusiana na ujenzi wa nyumba za walimu; katika bajeti zetu kuanzia mwaka 2020/2021 mpaka sasa na hata bajeti ya mwaka ujao 2025/2026, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kuendelea kujenga nyumba za walimu kwa awamu, ili kuwawezesha walimu wetu kuishi mazingira bora na pia kuwa karibu na shule ambazo wanafundisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yawe mafupi na moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini Shule ya Tambazi, Kata ya Katumba itafanyiwa marekebisho kwa sababu imechakaa sana na ni shule kongwe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nimuhkikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafuatilia kupata taarifa za Shule hiyo ya Msingi Tambazi na kuona gharama za fedha ambazo zinahitajika kwa ajili ya ukarabati. Nitumie nafasi hii kumuelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kufanya tathmini kupitia *Engineer* wa Halmashauri na kutuletea taarifa za mahitaji ya fedha, ili tutenge fedha *either* kutoka mapato ya ndani kwa awamu pia kutoka Serikali Kuu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipatia nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kuleta fedha kujenga shule shikizi kwenye maeneo ambayo watoto wanasoma maeneo ya mbali, kwa mfano, Kata ya Kerege na Mapinga, Vitongoji vya Kimere na Amani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele cha hali ya juu katika kusogeza huduma za kijamii karibu na wananchi zikiwemo shule na katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 mpaka sasa Serikali imeendelea kutenga fedha na kujenga shule shikizi katika maeneo ambayo yanahitaji kujengwa shule hizo.

Kwa hiyo, ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Subira Mgalu kwamba tutakwenda kuanza ujenzi wa shule katika maeneo hayo ikiwa yatakidhi vigezo, kwa maana idadi ya wanafunzi watarajiwa katika eneo husika na pia ukubwa wa vitongoji au vijiji hivyo ili wananchi hao na watoto waweze kusoma karibu zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itakarabati Shule ya Msingi Kitingi na Shule ya Msingi Lusimbi katika Kata ya Kwa Kivu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilishaainisha shule zote kongwe na chakavu, lakini pia kuanza kufanya tathmini ya uhitaji wa fedha kwa ajili ya ukarabati kwa awamu.

Kwa hiyo, ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kutenga fedha kwenye bajeti zetu kupitia mapato ya ndani na pia kupitia Serikali Kuu kwa ajili ya kuanza ukarabati wa shule hizo kongwe ambazo ni chakavu katika jimbo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Kilima A iliyopo Nyohogo, Wilaya ya Kahama imechakaa sana, je, nini mpango wa Serikali kukarabati shule hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaomba nitumie nafasi hii kwanza nimkumbushe Mkurugenzi wa Halmashauri husika kwamba wanawajibika kutuletea taarifa rasmi za tathmini za mahitaji ya ukarabati wa shule hiyo na nimuhakikishie Mheshimiwa Dkt. Christina kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutakwenda kufuatilia na kuona shule hiyo inahitaji kiasi gani cha fedha ili tuanze kutenga fedha kwa ajili ya kuikarabati shuke hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylivia Sigula, swali la nyongeza.

**MHE. SYLIVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Shule ya Msingi Ilemba ni ya mwaka 1973 imechakaa sana na madarasa hayatumiki kwa usalama wa wanafunzi. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kukarabati shule hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, katika bajeti ijayo ya mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa shule chakavu sana za msingi na Serikali ambazo zinahitaji ukarabati kwa haraka. Kwa hiyo, ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Sylivia kwamba tutakwenda kufuatilia na kuona uhitaji wa gharama za ukarabati, ili tuanze kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ukarabati shule hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula, Mbunge wa Kuteuliwa, swali.

Na. 499

**Ujenzi wa Barabara ya Kyazi – Katanga**

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuanza ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kimkakati ya Kyazi Kayanga – Missenyi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kujenga Barabara ya Kyazi Kayanga – Missenyi kwa kiwango cha lami ili kuboresha usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa Kata za Bwanjai, Kitobo, Bugandika na maeneo jirani. Hivyo, katika mwaka wa fedha 2026/2027, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya kuifanyia usanifu na kupata gharama za kuijenga kwa kiwango cha lami. Pindi gharama za ujenzi kwa kiwango cha lami zikijulikana, Serikali itaanza ujenzi huo kwa bajeti zinazofuata.

Mheshimiwa Spika, katika kuiwezesha barabara hiyo kupitika na kurahisisha usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa kata hizo, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga shilingi milioni 59 kwa ajili ya kuifanyia matengenezo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mvua kubwa zilizonyesha kipindi hiki na kuharibu barabara nyingi pamoja na hiyo barabara ya kimkakati aliyoitaja Mheshimiwa Waziri; je, mkandarasi atawezeshwa kujenga makalavati na madaraja yale madogo madogo ambayo yameharibiwa na mvua hii kubwa? Maana yake madaraja mengi yameondoka kwenye hiyo barabara. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba katika msimu uliopita tulipata mvua nyingi na zilileta athari kwenye barabara mbalimbali ikiwemo barabara hii ambayo ipo katika Jimbo la Missenyi, Barabara ya Kyazi Kayanga – Missenyi na ndio maana katika bajeti ya mwaka ujao tumeitengea bajeti ya shilingi milioni 59 kwa ajili ya marekebisho katika maeneo korofi. Pia Serikali itaendelea kuona maeneo ambayo yanahitaji ujenzi wa makalavati na madaraja kwa udharura Serikali itaendelea kutumia fungu lake la dharura kwa ajili ya kurekebisha barabara hiyo, ili iweze kupitika vizuri. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itaifanyia kazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Migombani kata ya Nitekela kipo kisiwani kwa sababu barabara zote ambazo zinaingia kijijini hapo zimekatika kwa sababu ya mvua ambazo zinaendelea kunyesha Mkoani Mtwara. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura kuhakikisha kwamba, wanarejesha mawasiliano katika kijiji hiki? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kijiji hicho cha Migombani katika Jimbo la Nanyumbu kilipata athari pia na mvua barabara nyingi zilikatika na kufanya kufikika kijiji hicho kuwa na changamoto. Tayari kupitia Meneja wa *TARURA* wa Nanyumbu na Mkoa wa Mtwara, Ofisi ya Rais, TAMISEMI - *TARURA* tumeshakubaliana kwamba, tutapeleka fedha mapema iwezekanavyo kwa sababu tumeshafanya tathmini ya mahitaji ya fedha kwa ajili ya kwenda kukarabati.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Chikota kwamba ni suala tu la muda Serikali itakwenda kurejesha miundombinu hiyo katika Kijiji jhicho. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha kimkakati katika Jimbo la Mwibara bado hazijafika. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali ilitenga shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kupeleka fedha kwenye vituo vya afya vya kimkakati kwenye majimbo 120 awali na mpaka sasa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishatoa bilioni hizo 30 na majimbo yetu yameanza kupokea fedha hizo zaidi ya 80% na 90%. Nikuhakikishie tu Mheshimiwa Kajege pia katika Jimbo la Mwibara taratibu za kupeleka fedha zinafanyika na ninaamini ndani ya wiki hii kwenye kile kituo cha afya ambacho ulikiweka kama cha kimkakati kwa kila jimbo fedha itaingia katika jimbo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 500

**Wilaya ya Nkasi Kukosa Miradi ya Kimkakati**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza: -

Je, nini sababu ya Wilaya ya Nkasi kukosa miradi ya kimkakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** aliuliza: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutekeleza miradi ya kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuziwezesha halmashauri kuongeza mapato ya ndani na kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya Nkasi iliibua na kuandaa maandiko ya miradi miwili ya kimkakati ya kuboresha minada mitatu ya kisasa na ujenzi wa hoteli ya kisasa katika Mji wa Namanyere. Maandiko hayo yaliwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI mwezi Julai, 2020 kwa ajili ya uchambuzi. Aidha, miradi hii ilikosa baadhi ya vigezo ikiwemo umiliki wa ardhi ya maeneo ya miradi na kutofanyika kwa upembuzi yakinifu wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa halmashauri ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa vigezo vilivyokosekana wakati wa uchambuzi. Mara baada ya hatua hiyo kukamilika na miradi kukidhi vigezo, Serikali itatafuta fedha na kuanza utekelezaji wa miradi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na nimeyasikia majibu ya Serikali. Kwa kuwa mahitaji ya Wilaya ya Nkasi ni soko pamoja na stendi na kwa mujibu wa wataalam suala la soko hati tumepata na stendi. Gharama za kujenga soko

ni shilingi bilioni 1.3. gharama ya kujenga stendi ni shilingi bilioni mbili. Serikali mpo tayari kutujengea miradi hiyo kwa sababu vigezo hivyo vingine vimekamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; hamuoni kuna haja sasa ya kuwajengea uwezo Maafisa Mipango nchi nzima yaweze kuibua miradi ya kimkakati?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza niwapongeze watendaji na viongozi wote wa Halmashauri ya Nkasi pamoja na Mheshimiwa Mbunge kwa kusimamia suala hili ambalo alipewa maelekezo na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuhakikisha kwamba wanapata hati pia kukidhi vigezo vya mahitaji ya miradi ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, kwa kuwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwamba stendi na soko tumeshapata hati na gharama zinazotatarijiwa kufanyika kwa maana ya kutumika kujenga, ninaomba nitumie nafasi hii nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge tutafutilia ili kupata taarifa rasmi kutoka kwa Mkurugenzi kupitia Katibu Tawala Mkoa na kuja Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ili tutenge fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa miundombinu hiyo ya kimkakati kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, suala la pili Serikali imekuwa ikifanya mafunzo ya mara kwa mara kwa Maafisa Mipango ili kuwajengea uwezo zaidi wa kuandika miradi ya kimkakati kulingana na mazingira yao. Suala hili Mheshimiwa Mbunge tumepokea ushauri huo tutaendelea kuboresha mafunzo hayo ili Maafisa Mipango wawe *competent* zaidi katika uandishi wa miradi ya kimakati.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tena moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii, mwaka 2023 tuliwasilisha andiko na michoro kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa eneo la Madila; je, mradi huu ni lini utaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, zipo halmashauri kadhaa ikiwepo Halmashauri ya Meru ambayo waliandika miradi ya kimkakati kwa ajili ya ujenzi wa soko na Serikali imeweka utaratibu; kwanza, miradi inawasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, inafanyiwa uchambuzi wa kukidhi vigezo na baadaye tunawasiliana na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuangalia kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nikuhakikishie Mheshimiwa dkt. Pallangyo tutaendelea kufuatilia kuona andiko hilo limefikia hatua gani, ili baada ya hapo tuone uwezekano kama linakidhi vigezo, uwezekano wa kuanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ilishawasilisha wasilisho la ujenzi wa stendi. Ninataka kujua ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili tufanye ujenzi huu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, tutafanya tathmini ya andiko ambalo limewasilishwa na Halmashauri ya Chemba na baada ya kuona kama linakidhi vigezo basi tutaanza utaratibu wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Halmsahauri ya Wilaya ya Hai iliwasilisha andiko lao la mradi wa kimakakti wa machinjio ya kisasa Kata ya KIA. Je, ni lini sasa Serikali itatekeleza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Saashisha Mafuwe kwamba tunafahamu wana mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa, lakini ninafahamu Mheshimiwa Mbunge pia amefuatilia mara kwa mara na tulikubaliana kwamba tunafanya tathmini ya kukidhi vigezo pia tunaangalia uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wake.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* hayupo, lakini kwa sababu sasa hivi ipo Wizara hii ya Mipango chini ya Ofisi ya Rais, mimi nafikiri kwa sababu maswali yote ya Wabunge maana yake lazima mradi utoke kwao ndio uje upande wa Serikali, lakini Serikali baada ya kuwa na hii Wizara ya Mipango, Serikali iwe na mipango kwamba hapa tutapeleka soko, hapa tutapeleka stendi, hapa tutapeleka machinjio, kuliko kuwasubiria wale maafisa kule ndio waombe yaani akipelekwa Afisa ambaye kidogo yeye hana haraka, kwa hiyo maana yake halmashauri itakaa, lakini Serikali lazima iwe na mipango kwa sababu tayari wizara imeshaanzishwa kwa ajili ya shughuli hiyo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama nchi lazima tuwe na mipango, sio lazima wao hawa ndio waanzishe miradi, mimi nafikiri tuanze kubadili hako kamtazamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Shally Josepha Raymond.

Na. 501

**Kituo cha Afya Kamsamba – Momba**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND K.n.y. MHE. NEEMA G. MWANDABILA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ujenzi wa majengo mapya ya Kituo cha Afya cha Kamsamba – Momba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Kamsamba kilijengwa mwaka 1943 na ni miongoni mwa vituo vya afya kongwe 203 ambavyo Serikali imeviainisha kwa ajili ya ukarabati na kuongeza miundombinu yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha ukarabati wa hospitali 50 kongwe nchini na baadaye itafanya ukarabati wa vituo vya afya kongwe kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya cha Kamsamba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini *specifically* kwa hiki kituo alichotaja Mheshimiwa; ni lini hasa baada ya huo je, ni lini? swali la kwanza.

Swali la pili, ni lini Serikali itapeleka vifaatiba katika hospitali mpya ya Uru Kusini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika,

ahsante sana, kama ambavyo nimeanza kujibu katika jibu langu la msingi kwamba Serikali imeweka vipaumbele, tunafahamu mahitaji ni makubwa na tungetamani mahitaji yote yafanyiwe kazi siku moja, vituo vya afya vyote vikarabatiwe, zahanati kongwe, hospitali kongwe, lakini kupanga ni kuchagua kutokana na vyanzo vya fedha. Tumekubaliana tukarabati kwanza hospitali chakavu na kongwe za halmashauri kwa sababu hizi ni hospitali za rufaa ambazo zinatoa huduma kubwa zaidi ndani ya halmashauri, lakini baadaye tutakwenda kwenye ukarabati wa vituo vya afya kongwe na tayari tumekwisha viainisha vituo 203 kikiwemo Kituo cha Afya cha Kamsamba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mama yangu Mama Shally Raymond kwamba suala hilo tumelipa kipaumbele na tunatarajia hospitali za halmashauri zitakarabatiwa ndani ya miaka miwili ya fedha na baadaye tutakwenda kwenye vituo vile vya afya.

Mheshimiwa Spika, swali la pili Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba na katika kipindi hiki cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, vifaatiba vimenunuliwa kwa wingi na kupelekwa kwenye vituo vyote vipya na hospitali zote za halmashauri zilizokamilika lakini na hospitali zile za zamani na mpaka sasa katika mwaka huu wa fedha jumla ya shilingi bilioni 63.7 zimetengwa kwa ajili ya vifaatiba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutapeleka pia fedha katika Hospitali ya Halmashauri ya Uru Kusini ambayo nina uhakika tayari wamepokea fedha zaidi ya shilingi milioni 900 lakini tunaendelea kupeleka fedha kwa awamu kuhakikisha kwamba vituo hivyo vinakuwa na vifaa tiba vya kutosha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele, swali la nyongeza.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Ngunichile ambacho ni cha kimkakati, lakini pia ni ahadi ya viongozi wa kitaifa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, Mama Tecla Ungele, kwamba tunafahamu kwamba kituo hicho ni ahadi ya viongozi wa kitaifa na sisi katika mipango yetu ya utekelezaji ahadi za viongozi wa kitaifa ni kipaumbele nambari moja na tumekwisha ainisha na tayari fedha zimeanza kupelekwa kwenye vituo mbalimbali ambavyo ni ahadi za viongozi wa kitaifa.

Kwa hiyo, naomba nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba tutaendelea kutoa kipaumbele na tutapeleka fedha kwa ajili ya kujenga kituo hiko cha afya cha kimkakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, swali lake litaulizwa na.... hamna Mbunge kutoka Ndanda?

Wewe umeshauliza la nyongeza leo, kwa hiyo ambaye hajasimama, haya Mheshimiwa Esther Matiko.

Na. 502

### *CAG* Kukagua *URA SACCOSS* ya Jeshi la Polisi

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isiagize *CAG* akague *URA SACCOS* ya Jeshi la Polisi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, *URA SACCOSS* ni chama cha ushirika kilichosajiliwa na kinasimamiwa na kukaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na Sheria Namba 10 ya mwaka 2018 ya Huduma Ndogo ya Fedha na ni mali ya wanachama ambao ni watumishi wa Jeshi la Polisi. *URA SACCOSS* hukaguliwa kila mwaka na Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO),* pia hukaguliwa na mrajisi wa vyama vya ushirika kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika *(TCDC)*. *URA SACCOSS* ni ushirika uliopata hati safi kuanzia mwaka 2015 hadi 2024, pia umepata tuzo ya *SACCOSS* bora nchini kuanzia mwaka 2021 hadi 2024, hii ni kutokana na kufuata sheria, kanuni na taratibu za ushirika na fedha na taarifa zake husomwa kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama kama matakwa ya sheria yanavyoelekeza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, pamoja na majibu ya Serikali lakini bado kumekuwa na malalamiko kuhusiana na hizi *SACCOSS* ambazo kwenye Idara ya Polisi, lakini na Idara nyingine ambazo zipo ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Sasa Serikali mnachukua hatua gani kuhakikisha kwamba mnatekeleza yale madhaifu ambayo mnakuta yametokana na ukaguzi wa *CAG? (Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi *SACCOSS* hii haikaguliwi na *CAG*, inakaguliwa kwa mujibu wa sheria namba sita inayosimamiwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika na. 6 ya mwaka 2013 na kama nilivyosema *URA SACCOSS* hii ni *SACCOSS* bora hapa nchini kama nilivyosema

imepata tuzo toka mwaka 2021/2024 kwa hiyo ni *SACCOSS* ambayo haina malengo yoyote ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Polisi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana, ama una swali lingine? Haya unaswali lingine.

Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, sasa aulize swali lake.

Na. 503

**Hitaji la Gari la Polisi na Zimamoto**

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka gari la polisi na gari la zimamoto katika Wilaya ya Kyerwa inayopakana na nchi mbili ili kukabiliana na majanga ya moto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imepeleka gari jipya moja aina ya *Toyota Land Cruiser Pickup* kwa Polisi Wilaya ya Kyerwa. Aidha, kwa upande wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Serikali itapeleka gari moja katika wilaya hiyo ikiwa ni mpango wa Serikali wa kusambaza magari ya zimamoto na uokoaji kwa wilaya zote nchini kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya moto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza niishukuru Serikali kwa gari ambalo wamepeleka Kyerwa, Wilaya ya Kyerwa ni wilaya changam hatuna kituo cha polisi. Polisi wanafanya kazi kwenye mazingira magumu, kwenye vibanda ambavyo vilikuwa ni vya wakimbizi.

Je, Serikali ipo tayari kuunga mkono juhudi za wadau ambao tayari wameshaanzisha ujenzi wa kituo cha polisi? *(Makofi)*

Swali la pili, polisi hawana nyumba pale Kyerwa, je, Serikali ipo tayari angalau kwa kuanzia nyumba ya *OCD* pamoja na *OC-CID*? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Kyerwa, amekuwa akifuatilia sana kituo cha polisi pamoja na vitendea kazi katika wilaya hiyo. Naomba nijibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze wadau ambao tayari walishaanza ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kyerwa ambayo ni wilaya mpya na nimhakikishie Serikali imekuwa ikiunga mkono juhudi za wananchi au wadau wanaofanya kazi hii. Kwa hiyo Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kyerwa pia tutaweka kwenye mpango na kutengewa fedha ili tuweze kumalizia kazi kubwa iliyofanywa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu nyumba za makazi ni kweli wilaya hii ni mpya, haina nyumba ya *OCD* wala *OC-CID*, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumechukua hili pia tutaweka kwenye mpango tayari kwa kutengewa bajeti kwa ajili ya kujenga nyumba za viongozi hawa wa Polisi wa Wilaya hii ya Kyerwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 504

**Kurahisisha Upatikanaji wa *VISA* kwa Makundi ya Watalii**

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza: -

Je, jitihada gani zimefanyika kurahisisha upatikanaji wa *visa* kwa watalii wenye uraia tofauti wanaokuja nchini kwa mwitikio wa *Royal Tour?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha utaratibu wa utoaji wa *visa* nchini ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani. Mathalani, Serikali kupitia Idara ya Uhamiaji imeanzisha mfumo wa maombi ya *visa* kwa njia ya mtandao unaowawezesha watalii kuomba *visa* popote walipo duniani bila kulazimika kufika ubalozini. Halikadhalika, Serikali imeboresha Kanuni za Uhamiaji za mwaka 2023 ambapo kwa sasa watalii wanaotumia *visitors pass* wanaruhusiwa kutembelea nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kurejea Tanzania bila hitaji la kuomba upya pasi ya kuingia nchini alimradi pasi aliyopewa iwe haijaisha muda wake.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, Serikali imeendelea kuingia makubaliano na nchi mbalimbali ili kurahisisha utaratibu wa *visa* ambapo kwa sasa raia wa nchi 71 hawahitaji *visa* wanapoingia nchini. Aidha, kwa sasa watalii kutoka katika mataifa mengi duniani wanaruhusiwa kupata *visa* wanapowasili kwenye viwanja vya ndege vya kimataifa kama Julius Nyerere, Kilimanjaro na Zanzibar. Vilevile, Serikali imefanya mapitio ya nchi zilizo kwenye kundi la *visa* rejea kwa lengo la kufanya maboresho.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza; swali la kwanza, kwa kuwa Tanzania tuna urithi mkubwa wa utamaduni wa asili, hususani Mikoa ya Singida na Dodoma, je, nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba tuna *promote* utalii wa utamaduni kwa mikoa ya Singida na Dodoma?

Swali la pili, Manyoni katika Tarafa ya Kilimatinde ilikuwa ni *route* ya watumwa, sasa je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaboresha mali kale ya Kilimatinde ili iweze kutumika kwa ajili ya utalii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Taifa letu lina utajili wa mila, desturi, tamaduni na maeneo ya kiutamaduni ambayo yanafaa kutembelewa, lakini vilevile tuna utajili wa vyakula vingi katika nchi yetu kutokana na uwepo wa makabila zaidi ya 120. Kwa kulitambua hili Serikali imekuwa ikifanya mikakati ya kushirikiana na mikoa mbalimbali kukutana na wadau katika mikoa hiyo, kwanza kuainisha maeneo haya ambayo yanaweza kuwa vivutio vya utalii, lakini pili kuainisha aina ya vyakula ambavyo vinaweza kutumika kutangaza utalii kwenye maeneo yetu. Hivi tunavyozungumza kuna matamasha yanaendelea ya utalii *(cultural tourism)* katika Mkoa wa Dodoma, ambayo yanahusisha vilevile kutembelea mashamba ya zabibu na kuangalia vikundi vya utamaduni, lakini vilevile kupata fursa ya kuona mila na tamaduni za Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Singida tayari tuna mawasiliano na wenzetu wa Dodoma, tunakusudia kuwa na kongamano kubwa na wadau wa utalii katika mkoa ule ili kuweza

kuainisha kwa pamoja vivutio hivi na kuona jinsi ambavyo tunaweza ku-*promote cultural tourism* katika Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo hili la pili kuhusiana na vivutio vya utalii kule Manyoni, ni kweli timu yetu ilishakwenda katika Wilaya ya Manyoni na kwa Mkoa wa Singida kwa ujumla, tuna maeneo ambayo tumeyabaini kama vivutio, yapo maeneo ambayo yanamilikiwa na Kanisa Anglikana, yapo maeneo ambayo kuna Boma la Kale la Mjerumani lakini vilevile ipo njia ile ya kati ya watumwa kwenye maeneo ya Kilimatinde. Maeneo haya yote tumekwishayabaini, sasa tunachofanya ni tunampango wa kukaa na hao wadau katika eneo lile ili kukubaliana yale ambayo wanayamiliki kisheria tuone jinsi ambavyo tunaweza kuyatangaza kwa pamoja na yale ambayo wapo tayari kuyaachia ili Serikali iweze kuyasimamia tutafanya hivyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mbunge wa Ludewa, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Neema William Mgaya.

Na. 505

**Kujenga Miundombinu ya Umwagiliaji - Ludewa**

**MHE. NEEMA W. MGAYA K.n.y. MHE. JOSEPH Z. KAMONGA** aliuliza: -

Je, jitihada zipi zinafanywa na Serikali kuhakikisha Wilaya ya Ludewa inajengewa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa David Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umwagiliaji katika Wilaya ya Ludewa ikiwemo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Skimu za Umwagiliaji za Mbwila hekta 4,000, Iselela hekta 1,800 na Bonde la Mto Ruhuhu lenye ukubwa wa hekta 4,500. Upembuzi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025 na kuanza taratibu za kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi. Aidha, Tume inaendelea na uchimbaji wa kisima cha umwagiliaji katika Kijiji cha Mangalanyene chenye uwezo wa kumwagilia ekari 123. Kisima hicho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kunufaisha wakulima 80 wa zao la chai.

**SPIKA:** Mheshimiwa Neema William Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Mkoa wa Njombe ni wakulima wazuri wa zao la chai, je, Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba mnaweka miundombinu rafiki kwa wakulima wadogo wadogo wa chai ili chai ile iweze kuleta tija kwa wakulima hawa wadogo wadogo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Neema kwamba moja ya mkakati wa Serikali tulionao sasa hivi ni kuchimba visima 67,000 kwa wakulima wadogo wadogo nchini na kazi hiyo tunatarajia kuanza hivi karibuni ikiwemo katika Mkoa wa Njombe ambapo tumeshuhudia wiki mbili zilizopita tumepokea magari kwa ajili ya uchimbaji na magari yale yatafanya kazi hizo ikiwemo Mkoa wa Njombe kwenye kila zao.

Kwa hiyo, tutafanya kwenye chai, kwenye kahawa mazao karibu yote ambayo yanamgusa moja kwa moja mkulima mdogo. Kwa hiyo lipo katika mpango wetu na nimthibitishie litafanyika hivyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako.

Ahhh, samahani Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya Rungwe inapata mvua zaidi ya miezi nane lakini miezi minne inayobaki inakuwa ni ya jua na sisi ni wakulima wazuri sana wa chai na parachichi, umesema mmepata magari na mtayapeleka Njombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema nini juu ya Wilaya ya Rungwe kuhakikisha magari yanafika kwa kuwa na sisi ni wakulima wazuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimesema tutachimba mikoa yote nchini ikiwemo Mkoa wa Njombe na idadi ya visima tutakavyochimba ni 67,000 na magari yameshafika na tutafanya *operation,* tutakuwa tunavamia mkoa mmoja tunachimba tunamaliza, tunakwenda mkoa mwingine, hatutafanya kazi nusunusu. Kwa hiyo, hata Rungwe, Mkoa wa Mbeya tutafika, hata Songwe kule ninakotokea na kwenyewe tutafika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Grace Victor Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 506

**Uvunaji wa Maji ya Mvua Kupunguza Changamoto ya Maji**

**MHE. GRACE V. TENDEGA** aliuliza:

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha uvunaji wa maji ya mvua unapunguza changamoto ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa uvunaji wa maji ya mvua wa miaka mitano kuanzia mwaka 2022 hadi 2026 kwa kujenga mabwawa kwa lengo la kukabiliana na changamoto za mafuriko na ukame. Pia utekelezaji unaendelea wa mkakati wa uvunaji wa maji ya mvua kandokando ya barabara kwa miaka mitano kuanzia mwaka 2020 hadi 2025 kwa kujenga malambo ambao uliandaliwa mahususi kwa ajili ya kulinda miundombinu ya barabara na reli. Kupitia mikakati hiyo, jumla ya mabwawa 45 yamejengwa katika kipindi cha mwaka 2022 hadi 2025, mabwawa 19 yanaendelea na ujenzi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetenga zaidi ya shilingi bilioni 5.5 kwa ajili ya kukarabati mabwawa 15 ya ukubwa mdogo na wa kati sanjari kuhamasisiha uvunaji wa maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba hususani kwenye taasisi za umma kama mashule, zahanati, vituo vya afya, hospitali na ofisi mbalimbali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Victor Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali kwamba mmejenga mabwawa zaidi ya 45 na mengine 19 mnaendelea kuyafanyia kazi lakini katika maeneo ya zahanati, katika vituo vya afya na katika hospitali mbalimbali kumekuwa na changamoto kubwa sana ya maji.

Je, Serikali hamuoni haja sasa ya kujenga miundombinu kwa ajili ya uvunaji wa maji katika maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, mikoa iliyopo katika Nyanda za Juu Kusini ikiwepo Mkoa wa Iringa ni mikoa ambayo inapata mvua kwa miezi minne hadi minane na wakati wa mvua maji hutiririka na yakaenda kwenye mito mikubwa na kadhalika, lakini katika Jimbo la Kalenga bado kuna changamoto ya maji, mvua zikinyesha maji yanakuwepo yanatiririka yanaenda yanapotea.

Mheshimiwa Spika, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba maji hayo yanatengenezewa mabwawa katika Jimbo la Kalenga kwa mfano, Kata ya Luhota katika eneo Kijiji cha Kitayawa kuna mto huwa unatokea wakati wa mvua lakini mvua ikiondoka wanapata adha ya maji? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, pia namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali zuri kabisa, lakini pia ni kwamba kama ambavyo nimejibu katika majibu yangu ya msingi, Serikali tayari imejenga mabwawa 45, 19 yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ni hatua kwa hatua na maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja Serikali tunayachukua kwa ajili ya kuna namna ambavyo kadiri upatikanaji wa fedha utakaporuhusu tutajenga *specific* katika katika eneo la Kalenga kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

Mheshimiwa Spika, katika upande wa kujenga miundombinu rafiki ya uvunaji wa maji katika shule na taasisi nyingine mbalimbali kama ambavyo pia nimejibu katika majibu ya msingi, ni mkakati wa Serikali kuendelea kujenga, lakini kuboresha pale ambapo tayari miundombinu na pale ambapo tunaona kwamba kuna changamoto zaidi basi Serikali itaendelea kuwekeza fedha lengo kubwa ni kuendelea kuhakikisha kwamba maji ambayo yanapatikana yanatokana na mvua tuendelee kuyavuna na hatimaye yatasaidia katika kutatua katika upungufu wa maji na vilevile kuzuia uharibifu wa miundombinu katika maeneo ya shule au taasisi nyinginezo ambazo zinatokana na maji kutiririka hovyo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 507

**Kupeleka Maji ya Ziwa Victoria Tarime Vijijini**

**MHE. MWITA M. WAITARA** aliuliza: -

Je, lini maji kutoka Ziwa Victoria yatafika katika Vijiji vya Sirari, Nyamwaga na Nyamongo vilivyopo Tarime Vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Vijiji vya Sirari, Nyamwaga na Nyamongo vinapata huduma ya majisafi na salama kupitia vyanzo vya chemchem na visima virefu vilivyochimbwa kwenye maeneo hayo. Aidha, katika kuboresha zaidi huduma ya maji katika maeneo hayo, Serikali inatekeleza Mradi wa Miji 28 kutoka Ziwa Victoria kwenda katika Wilaya za Rorya na Tarime ambapo kukamilika kwake utanufaisha pia Kijiji cha Sirari. Mradi huo unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa miradi ya maji kwa ajili ya kufikisha huduma kwenye vijiji ambavyo havijafikiwa na Mradi wa Ziwa Victoria ikiwemo Vijiji vya Nyamwaga na Nyamongo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, tenki limejengwa Sirari, Mogabiri na pale Komaswa, naomba nijue uhakika wa Serikali na hasa Wizara ya Maji kuweka matoleo pale Sirari, Mogabiri na Komaswa ili wananchi hao wa Ganyange, Nyamwaga na Nyamongo wawe na uhakika kwamba kwa awamu ijayo watapata maji kutoka Ziwa Victoria?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mradi wa Maji Korotambe na Masanga ulichibwa maji yakaanza kutoka sasa umekwama. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba watu wa Korotambe, Masanga, Masurura, Kitawasi wanakunywa maji ya bomba kama ambavyo waliaminishwa hapo mwanzo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ni kweli kabisa mradi wetu huu na matenki yamejengwa pale Sirari na Mogabiri, lakini kuna maeneo ambayo tunafanya usanifu katika mwaka wa fedha 2025/2026 ili kuhakikisha kwamba maeneo ya Komaswa na Sirari tunayahakikishia kwamba Serikali hilo tumeshalipokea na Mheshimiwa Mbunge si mara ya kwanza kuliongelea siyo ndani ya Bunge lakini amekuwa akilifuatilia sana kwa kina hili suala na sisi tumeshalichukua na linaingizwa katika usanifu utakaofanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026 kuhakikisha kwamba matoleo katika upande wa komaswa na wao wanaenda kupata maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mradi wa Masanga, tulikuwa na kisima ambacho kilikuwa na uwezo wa kutoa maji lita 6,000 kwa saa, lakini kwa bahati mbaya kikapoteza uwezo wake wa kuzalisha maji na sasa kinazalisha takribani 1,500 ambayo hayawezi kutosheleza katika maeneo yote. Kwa hiyo, sisi tunachokifanya sasa ni kutumia ile miradi inayofanyika katika maeneo ya jirani ya Nyanungu, nafikiri kuna eneo Nyanungu pale ambapo ule mradi utakapokamilika ndio tutafanya *extension* kwa ajili ya kuja kuhudumia maeneo ya Masanga.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mradi ambao Korotambe, maeneo ya Korotambe tulikuwa tunatumia jenereta, ule mradi baada ya jenereta kuzidiwa ikabidi sasa tufanye utaratibu wa kubadilisha mifumo ambayo ilikuwa inasaidia ku-*pump* maji kwenda katika umeme wa *TANESCO* na sasa tayari mkandarasi yupo *site* anaendelea kuhakikisha kwamba maeneo mengi siyo kwa Korotambe pekee yake na yale maeneo mengine ambayo yanazunguka katika eneo hilo ambayo yalikuwa yananufaika na mradi huo. Lengo ni kwamba waendelee kupata huduma ya maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona maswali, nirejee tena maswali yawe mafupi.

Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itapeleka maji ya Ziwa Victoria katika Jimbo la Meatu ili kuweza kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu kwa kazi nzuri ambayo kwa kushirikiana na Wabunge wa Mkoa wa Simiyu kwa kuhakikisha kwamba umesemewa mradi huu kikamilifu na Mheshimiwa Rais alishatoa fedha takribani shilingi bilioni 440 kwa ajili ya kuyatoa

maji kutoka Nyashimo, Bariadi kwenda Itilima na sasa tupo katika awamu ya pili mradi wa kwanza upo 20% na mradi wa pili ambako sasa itaanza Maswa kwenda mpaka Meatu. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge awamu ya pili hii inaenda kufika mpaka Meatu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona, Mji wa Makambako wananchi wanapata shida sana suala la maji; je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inaondoa tatizo la maji katika Mji wa Makambako? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana kaka yangu kwa kazi nzuri anayofanya kwa ajili ya wananchi wake wa Makambako na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliridhia kutoa kiasi cha shilingi bilioni 42 kwa ajili ya kupeleka kwenye Mradi wa Miji 28 ambapo mpaka sasa mradi huu umeshafikia 20% na tunaamini kwamba mradi huu utakapokamilika Mji wa Makambako suala la maji halitokuwa tatizo tena, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, upembuzi yakinifu umefanyika katika Kata za Seke Bugoro, Mondo, Mwasubi na Bunambiyu; je, Serikali iko tayari sasa kupeleka shilingi bilioni 16.5 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu?

**SPIKA:** Hebu subiri Mheshimiwa, weka kisemeo vizuri malizia hiyo sehemu ya mwisho ya swali. Je, anzia hapo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, je, Serikali iko tayari kupeleka shilingi bilioni 16.5 ambazo zimeonekana katika zoezi la upembuzi yakinifu na wa kina kwa ajili ya utelezaji wa miradi katika kata hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana nashukuru pia Mheshimiwa Butondo kwa kazi nzuri aliyoifanya na kwa kushirikiana na Serikali mpaka tukafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ambao ikatupatia gharama ya shilingi bilioni 16.5. Serikali iko tayari kwa ajili ya kwenda kuhakikisha mradi huo unatekelezwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, baadhi ya maeneo katika Vijiji vya Sango, Shia, Mdawi na Kisaseni katika Kata ya Kimochi yana uhaba mkubwa sana wa maji; je, Serikali ina mikakati kupeleka maji katika maeneo haya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, Mbunge wa Moshi Vijijini, lakini lazima niseme jambo moja hapa kwamba Kata ya Kimochi, Serikali iliweka miundombinu na kwa bahati mbaya wananchi wa Kata hii ya Kimochi walihujumu miundombinu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge aliomba fedha na Serikali tumeshatoa shilingi milioni 983 na Mheshimiwa Mbunge ameshaomba nyingine tena shilingi milioni 484 lakini naomba tutoe maelekezo kwa wasimamizi wote wa vyanzo hivi na miundombinu wananchi wapewe elimu ya kutosha ili wasiendelee kuharibu miundombinu ni fedha ambazo ni za walipa kodi ambazo tunaamini kwamba wakisimamia hizi fedha zingeenda kufanya kazi nyingine. Serikali tuko tayari kuendelea kushirikiana na wananchi wa Moshi Vijijini, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mradi wa Miji 28 unapeleka maji Urambo kupitia Uyui; je, lini Serikali itaanza maandalizi ya kupeleka maji katika Vijiji vya Mabama, Ilolangulu, Ufuluma na Ndono? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ni kweli kabisa Serikali imeshapeleka maji Tabora kwa shilingi bilioni 680; imepeleka Urambo Kaliua pamoja maeneo mengine kwa shilingi bilioni 143 na sasa kazi iliyobaki ni kuendelea kufanya upanuzi wa mradi ili vijiji vingi zaidi viweze kufikiwa. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge na vijiji hivyo katika JIMBO lake la Uyui tutafikisha huduma hiyo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mradi wa Maji wa Kata ya Kapalamsenga umekwama kwa kukosa shilingi milioni 700 kukamilisha ujenzi wa matenki; ni lini Serikali itapeleka fedha hizo ili kukamilisha huo mradi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, lakini pia namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kukumbusha kwa sababu najua tumeendelea kuwasiliana kuhusu jambo hili na sisi Serikali tunalijukulia kwa uzito wake na Katibu Mkuu ameshaelekeza Mameneja wa Mikoa kuhakikisha kwamba wanaleta hati za madai ili tuhakikishe kwamba sasa wakandarasi wetu wanalipwa na ili warudi *site* ili wakaendelee na miradi ikamilike na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kazi hiyo tunaendelea nayo na naamini kwamba itakamilika muda si mrefu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mbokomu yenye vitongoji 21, ni vitongoji nane tu ndio vinapata maji licha ya kuwa na miundombinu mizuri ya maji. Ni lini Serikali itaenda kuweka miundombinu ili vitongoji vingine viweze kupata maji? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na namshukuru sana dada yangu Mheshimiwa Felista Njau kwa kuwasemea wananchi katika vitongoji hivyo. Naomba nilipokee hili ili tukalichakate kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaenda kutoa majibu stahiki yakiendana na utekekezaji husika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mbunge wa Iramba Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 508

**Ujenzi wa Barabara Inayoelekea Makao Makuu ya Wilaya – Mkalama**

**MHE. FRANCIS I. MTINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami kilometa 42 barabara inayoelekea Makao Makuu ya Wilaya Mkalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, barabara inayoelekea Makao Makuu ya Wilaya ya Mkalama inaitwa Barabara ya Iguguno Shamba hadi Nduguti yenye urefu wa kilometa 42.6. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa Serikali imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 2.5 katika Mji wa Iguguno. Kwa sasa Serikali inaendelea na taratibu za manunuzi ili kumpata mkandarasi wa ujenzi wa kilometa 10 kwa kiwango cha lami. Kwa sehemu iliyobaki Serikali itaendelea kutafuta fedha ili kuendelea na ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, swali la nyongeza.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara hii tulipewa kilometa 10 tangu enzi Mheshimiwa Mbarawa akiwa Waziri wa Ujenzi na tumekuwa tukisubiri barabara hii kwa muda mrefu sana. Je, Serikali sasa inaweza ikasema ni lini itakwenda *site* Mkalama kwa ajili ya kujenga hizi kilometa 10 ambazo zimekuwa ni hadithi kwa Wana-Mkalama? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, inapopita barabara hii katika Kata za Iguguno, Kinyangiri, Nduguti, Gumanga, Ibaga mpaka kule Mpambala, wananchi wameondoa nyumba zao wamevunja kwa hiyari na katika hawa wananchi wapo wenye alama za *X* ya kijani kwa maana wanastahili kulipwa; pamoja na kuwa Serikali inachelewa kujenga barabara hii. Ni lini basi itawalipa wananchi hawa ambao wamebomoa nyumba zao ili waweze kuendelea na maisha yao wakati wa kisubiri lami hii ambayo haifiki? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwenda *site* Wizara iko tayari lakini kinachoendelea sasa hivi ni kwamba tukishakamilisha taratibu za ununuzi kwa maana mkandarasi amepatikana ndio atakwenda *site* na Wizara itakuwa tayari kumsimamia huyo mkandarasi ambaye atakuwa amepatikana na tupo kwenye hatua za mwisho kabisa za ununuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia ya hawa watu ambao watapisha ujenzi ama mradi nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tulishakamilisha tathmini na tulishapeleka maombi ya malipo ya fidia Wizara ya Fedha na kabla hatujaanza ujenzi tuna uhakika kwamba tutakuwa tumewalipa hao wananchi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Yahya Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, mkandarasi anayeweka taa za barabarani katika Jimbo langu la Nanyumbu amesimamisha huduma hiyo kwa kukosa malipo; je, ni lini mkandarasi huyo atalipwa ili aendelee na kazi hiyo ya uwekaji wa taa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tumeshatoa hati za malipo kwa maana hati za madai za mkandarasi Hazina ili waweze kumlipa huyo mkandarasi na aweze kuendela na kazi ya kukamilisha uwekaji wa hizo taa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Buhigwe – Katundu-Heru Ushingo mpaka Kitanga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Mheshimiwa Spika, samahani.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara aliyotaja iko Mkoa wa Kigoma ambayo ni barabara ya ulinzi na tunavyoongea sasa hivi kitu cha kwanza ni kujenga kwanza daraja la kuunganisha Wilaya ya Kasulu na Kibondo halafu tukamilishe usanifu na kwa sababu kipaumbele pia ni barabara za ulinzi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya kukamilisha daraja ambalo litakuwa na uwezo wa kuunganisha sasa tutaanza mipango ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini Serikali itakamilisha Barabara ya Nyakato – *VETA* - Buswelu mpaka *Igombe TX* yenye kilometa 18.2 imebakia kilometa nne na imejengwa kwa miaka 10 sasa bila kukamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, dhamira ya Serikali ni kukamilisha hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami na hasa ikizingatiwa ukuwaji wa kasi wa Mji wa Mwanza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mipango yetu ya mwaka unaokuja wa fedha tumepanga hiyo barabara ili iweze kujengwa na kukamilika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephat Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, ni lini Serikali itamlipa mkandarasi ambaye anajenga barabara ya kimkakati ya Matai kwenda *Kasesha border* ambaye sasa hivi hayupo kwa sababu hajalipwa fedha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Barabara ya Matai - Kasesya ni kati ya barabara ambazo tumeshapata wakandarasi lakini wanasubiri kulipwa fedha za awali. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama Serikali tumeshawasilisha mahitaji ama madai ya mkandarasi kwa ajili ya *advance payment* na tuna uhakika akishalipwa mkandarasi huyo ataanza kazi ya kujenga ili kuunganisha Tanzania na Zambia kupitia mpaka wa Kasesya, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Elibariki Kingu, swali la nyongeza.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, Barabara ya Singida – Sepuka – Ndago mpaka Kizaga inajengwa kwa kusuasua licha ya mkandarasi kulipwa *advance payment* kwa muda wa miezi karibia minne sasa. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha mkandarasi huyu anatimiza wajibu wa kujenga barabara hii kwa *speed* inayotakiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tumeshamwelekeza Meneja wa Mkoa ambaye anasimamia mkandarasi huyu kwa ukaribu kwamba baada ya kukamilisha taratibu zote za maandalizi ya awali aweze kuongeza kasi ili barabara hii muhimu sana iweze kukamilishwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Singida kwamba hiyo barabara tutahakikisha kwamba inakamilika kwa muda, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Serikali imekuwa ikifanya matengenezo ya mara kwa mara kwenye eneo takribani kilometa 15 kutoka Mbamba Bay, eneo la Luika Ngindo ambapo kila mwaka maji yanakuwa mengi hapo kiasi kwamba magari yanalala jambo ambalo kwa siku hizi kwa kweli ni aibu kwa jinsi ambavyo Serikali imefanya kazi vizuri.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba eneo hilo litengenezwe kwa kiwango cha lami kwa kutumia upembuzi yakinifu ambao tayari umeshafanyika katika barabara hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU SPIKA WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, niseme tu kwamba katika mwaka huu wa fedha, fedha nyingi sana imepelekwa kwenye maeneo ambayo yalikuwa na changamoto na hasa kipindi cha mvua na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba naomba nilichukuwe hili suala kwa sababu maeneo yote yaliyokuwa na changamoto tuliweza kuyapangia fedha ili kuyadhibiti wakati wa mvua iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, niombe kuchukuwa suala la Mheshimiwa Mbunge, lakini pia nimuagize Meneja wa Mkoa wa Ruvuma aweze kwenda kwenye hilo eneo afanye tathmini na aweze kuleta mapendekezo yake Wizarani ili tuone namna ya kufanya ili kuondoa adha ambayo inawakuta wananchi hao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga Mbunge wa Mbinga Vijijini sasa aulize swali lake.

Na. 509

**Ujenzi wa Barabara ya Nyoni hadi Maguu – Mbinga**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza upembuzi yakinifu na kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Nyoni – Maguu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ujenzi wa Barabara ya Nyoni – Maguu yenye urefu wa kilometa 30.55 kwa kiwango cha lami inafanyika kwa awamu

kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa kipande cha barabara hiyo chenye jumla ya urefu wa kilometa 5.6 kinachopitia kwenye maeneo korofi yenye miteremko mikali tayari kimejengwa kwa kiwango cha lami na zege, ambapo kwa kilometa 4.6 kimejengwa kwa kiwango cha lami na kipande cheye urefu wa kilometa 1.0 kimejengwa kwa kiwango cha zege. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya kazi ya upembezi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nishukuru kwa majibu ya Serikali.

Kwa kuwa barabara hii ni barabara pekee inayounganisha Tarafa ya Hagati na barabara kubwa inayoelekea mjini, lakini barabara hii huwa inagemka sana hasa kule chini kutokana na hali ya udongo uliopo wa tifutifu, je, Serikali ipo tayari kuharakisha mpango wake iweze kuijenga barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kipande cha Luanda hadi Lituhi tayari tulipata mkandarasi toka mwaka jana na tayari mmesaini, lakini mpaka leo mkandarasi huyu hajaanza kazi kwa sababu hajapata *advance*, ni lini Serikali itampa *advance* barabara hii ianze kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi kulingana na jiografia na hali halisi ya udongo wa jimbo la Mheshimiwa na hasa huko ambako hii barabara inapita ndiyo maana katika jibu langu la msingi tumesema tumeangalia yale maeneo yote korofi, kuyajenga ama kwa lami ama kwa zege pamoja na kwamba hiyo barabara bado ni *rough road,* lakini tumeliona hilo na

niwahakikishie kwamba tutaendelea kufanya hivyo wakati tunaendelea kukamilisha usanifu ili tuweze kuondoa adha ambayo inatokea hasa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Barabara ya Luanda – Lituhi - *Ndumbi Port,* nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tulishasaini mkataba, tulishapeleka hati za madai kwa maana ya malipo ya awali ili mkandarasi huyo alipwe na aanze kazi ya ujenzi barabara yote hiyo ya Luanda – Lituhi – Ndumbi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas Van Zeeland, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, barabara ya kutoka Lusanga kwenda Kibati ni barabara muhimu sana kwa uchumi wa nchi kwa sababu inaunganisha Mkoa wa Tanga na Morogoro; je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kufanya upembuzi yakinifu ili barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli kwamba hiyo barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge ni muhimu sana ambayo inaunganisha Mkoa wa Morogoro na Tanga na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba itakuwepo kwenye mpango wa usanifu, lakini kwa sasa tutakachohakikisha ni kwamba tunaitengea fedha iweze kukarabatiwa ili iweze kupitika kipindi chote wakati tunafanya maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Barabara ya Mahenje – Ndolezi – Hasamba kupitia Kilimampimbi – Iboya Serikali ilishafanya upembuzi yakinifu lakini kuna kipande kilichobaki; ni lini Serikali itakamilisha upembuzi yakinifu wa kipande cha Hasamba – Kilimampimbi – Iboya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tulishaanza hiyo kazi ya kufanya upembuzi yakinifu wa hiyo barabara na inasimamiwa na Mkoa wa Songwe. Naomba nimwelekeze meneja kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha unaokuja kazi hiyo inakamilika ili tuweze sasa kuanza usanifu wa kina, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Halmashauri ya Mji wa Bunda inakuwa na ina barabara moja tu ya lami ya kwenda kwa Mkuu wa Mkoa, ni lini sasa Serikali mtatujengea lami kwenye mitaa yetu ya Mji wa Bunda ili na wenyewe uwe na hadhi na kufanana kama miji mingine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna wakala mbili, *TANROADS* na *TARURA*, kwa hiyo barabara nyingi ambazo zinajengwa ambazo sio kubwa kwa maana ya *Regional Roads* zinajengwa na *TANROADS* na zile nyingi ambazo ni za miji huwa zinasimamiwa na *TARURA*. Naomba nichukuwe suala hili, sisi kama tuta-*qualify* kujengwa na *TANROADS* tuweze kufanya hiyo kazi, lakini kama zitakuwa ni za wenzetu wa *TARURA* basi nilichukuwe hilo ili Serikali iweze kuangalia na kufanya huo mji uwe na barabara za kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, Barabara ya Holili – Moshi – Arusha ni barabara ya muhimu sana kwa uchumi wa nchi hii na ina msongamano mkubwa sana, niishukuru Serikali imeshatoa fedha kwa vipande vitatu, Tengeru, *Arusha National Park Junction,* Kikafu pamoja na pale Moshi Mjini

Maili Sita mpaka Kiboriloni, ni lini tutapata fedha kwa ajili ya upanuzi wa vipande vingine vyote vilivyobaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nishukuru tu kwamba Mheshimiwa Mbunge anatambua tumeshapata fedha kwa hivyo vipande vitatu lakini pia ni barabara ambayo tunakwenda kujenga njia nne ikiwa ni pamoja na daraja na kwa kufanya hivyo, maana yake ni kuwa Serikali pia tunajipanga kujenga barabara yote kwenye kiwango hicho ili kupunguza msongamano mkubwa ambao upo katika hiyo barabara ya Arusha – Moshi – Holili, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu Chakoma, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

Na. 510

**Ujenzi wa Barabara ya Kilindoni – Rasimkumbi (Km 52.28) kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. HAWA M. CHAKOMA** Aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kutoka Kilindoni – Rasimkumbi - Mafia kilometa 52.16?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** Alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Kilindoni – Rasimkumbi - Mafia (kilometa 52.16) kwa awamu. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 na 2023/2024 Serikali imekamilisha kujenga jumla ya kilometa 2.15. Kwa sehemu iliyobaki (kilometa 50.13) iko katika hatua za manunuzi ya kumpata mkandarasi wa ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa majibu yako mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini barabara ya Mbinga – Litembo – Meyangayanga katika Jimbo la Mbinga Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni lini Serikali itaweka taa kwenye barabara ya kutoka Hazina kupitia *UDOM* mpaka kule Iyumbu kwa sababu ni barabara ambayo hata viongozi wanapita hasa usiku?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara ya Mbinga – Litembo imeshafanyiwa upembuzi yakinifu na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili iweze kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwekaji wa taa za Hazina kwenda *UDOM*, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge ambaye mara kadhaa amekuwa akiliongelea. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumejibu kwamba tulishapata orodha ya maeneo yote ambayo yana uhitaji, lakini pia kama Wizara tutapeleka taa 200 ambazo mkoa husika utahusika kuona maeneo yapi ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo alilotaja la Hazina – *UDOM* litakuwa ni moja ya maeneo ambayo yatakwenda kuwekewa taa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwa kuwa barabara pekee ya kuingilia Ukerewe ya Lugizi - Nansio mkandarasi wake ana zaidi ya mwaka mzima amesimama kufanya kazi kwa kutolipwa *advance payment* na sasa ina…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, tafuta kiti uketi. Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Lugizi - Nansio ambayo mkandarasi wake amesimama zaidi ya mwaka mmoja kwa kutolipa *advance payment* na barabara hii imekuwa kero kubwa kila siku magari yanakwama na ndiyo barabara pekee ya kuelekea Ukerewe; nini kauli ya Serikali sasa kwa wananchi wa Ukerewe kuhusu barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia kwamba tumeshapata maelekezo pia ya Waziri Mkuu alivyokwenda huko kwamba tuweze kutafuta fedha ili kumlipa mkandarasi ambayo kimsingi alishafanya kazi, kwa hiyo, tulishapeleka hati za malipo Hazina na tuna uhakika muda sio mrefu atalipwa ili aweze kuendelea na kazi kukamilisha hiyo kazi ambayo ameshaianza, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Barabara ya Bigwa – Kisaki mkandarasi amesimama, haendelei na kazi na hiyo barabara ni muhimu sana kwa sababu ya uzalishaji wa watu wa Morogoro, je, ni lini barabara hii na mkandarasi ataanza kujenga hiyo Barabara ya Bigwa - Kisaki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni kweli kwamba barabara hiyo mkandarasi alishasaini mkataba na kinachosubiriwa ili aanze kazi ni kulipwa fedha ya awali kwa maana ya malipo ya awali na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari tunasubiria malipo kutoka Hazina ili mkandarasi huyo aweze kulipwa na kuanza kazi ya Barabara ya Bigwa – Kisaki, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 511

**Ujenzi wa Barabara ya Katoro hadi Daraja la Nyikonga**

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, Serikali ipo hatua gani kwenye ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Katoro hadi Daraja la Nyikonga kwenye Barabara ya Katoro – Ushirombo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza taratibu za kuijenga barabara hii kwa kuanza na ujenzi wa Daraja ya Nyikonga ambapo zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa daraja ziko hatua za mwisho. Kwa upande wa barabara, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika na kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, swali la nyongeza.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali kuhusu barabara ya kutoka Ushirombo – Katoro, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, je, upembuzi yakinifu uliofanyika miaka kadhaa iliyopita bado unafaa kwenye ujenzi wa barabara hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya kutoka Geita kwa maana ya Mpomvu – Nyarugusu – Bukoli – Irogi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kuhusu kama upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utakuwa unafaa au laa, wataalam watakwenda uwandani wakati kipande hiki kitakapotakiwa kuanza kujengwa na kupitia upya ule usanifu na kama kutakuwa na marekebisho basi wataalam watafanya hayo marekebisho yatakayohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Barabara ya Mtakuja – Nyarugusu – Bukoli – Kakola nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari mkandarasi alishapatikana na kinachosubiriwa sasa hivi ni kwamba mkataba huo upo kwa Mwanasheria Mkuu kwa ajili ya *vetting*, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Phillip Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara inayoanzia Ramadhan – Iyai inayounga Mkoa wa Njombe kupita Jimbo la Njombe, Halmashauri ya Mji wa Njombe – Wanging'ombe, ni lini barabara hii itapata fedha za kutosha ili ikamilishwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Ramadhan – Iyai kilometa 74 imeshafanyiwa usanifu na kwa sasa tumekuwa tukiijenga kwa awamu na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika bajeti ya mwaka tunaouendea wa 2025/2026 tumeitengea fedha ili iweze kuanza kujengwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, marekebisho kidogo wakati swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota lilipokuwa likijibiwa ambalo liliulizwa chini ya swali la msingi namba 499 lililoulizwa na Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati akijibu kuhusu Kijiji cha Migombani alisema

kipo Jimbo la Nanyumbu, lakini kijiji hiki kipo kwenye Jimbo la Nanyamba ambalo ni Jimbo la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota. Kwa hiyo Kumbukumbu Rasmi za Bunge zitarekebishwa.

Waheshimiwa Wabunge, wageni tulionao Bungeni asubuhi hii.

Tunao Wageni sita wa Mheshimiwa Maryprisca Winfred Mahundi, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, familia yake kutoka Jijini Mbeya, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu ambaye ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, huyu ni mpiga kura wake kutoka Kwela Mkoa wa Rukwa, Ndugu Walter Simusokwe.

Wageni 51 wa Mheshimiwa Augustine Holle Vuma ambao ni waumini wa Kanisa Kuu la Anglikana la Roho Mtakatifu kutoka Jijini Dodoma, pia yupo Mke wa Mheshimiwa Vuma, Ndugu Irene Vuma na Mke wa Mheshimiwa George Malima, Ndugu Miriam Malima, karibuni sana. *(Makofi)*

Haya mkishaketi wake za Waheshimiwa Wabunge wasimame, haya sasa Waheshimiwa Wabunge tulieni basi au mmeshajua mke yupi ni wa yupi hapo? Maana tayari naona mnapiga makofi, mke wa Mheshimiwa Vuma mkono juu, aah, ahsante sana. Kwa hiyo anayebaki anakuwa ndiyo mke wa Mheshimiwa George Malima, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo ambao ni Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ambao ni wapiga kura wake kutoka Mbogwe, Mkoani Geita. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa ambao ni makada wa CCM kutoka Busanda, Mkoani Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea bunge kwa ajili ya mafunzo; yupo Ndugu Casto Tarimo, mwanafunzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Jordan kutoka Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wanachuo nane na mhadhiri mmoja wa Chuo Kikuu cha Kikatoliki Mwenge kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Wanafunzi 145 na walimu 15 wa Shule ya Awali na Msingi Libermann kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 122 na walimu nane wa Shule ya Msingi Mecson kutoka Jijini Arusha, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge na hili tangazo linahusu vikao vya majumuisho ya bajeti.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kwamba kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kwanzia tarehe 5 hadi 11 Juni, 2025 yaani siku sita, itakuwa ni kipindi cha majumuisho ambapo Serikali kwa kushirikiana na Kamati ya Bajeti watazingatia hoja zilizojitokeza katika mjadala wa Bajeti za Wizara ama Bajeti za Kisekta. Aidha, katika kipindi hicho cha majumuisho Bunge litaendelea na shughuli zake nyingine kwa mujibu wa ratiba iliyopagwa.

Pia Wajumbe wa Kamati ya Uongozi mnatangaziwa ama mnakumbushwa kwamba kwa nafasi zenu mnakuwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti hivyo mnatakiwa kuhudhuria vikao hivyo vya majumuisho kwa mujibu wa Kanuni ya 124(3).

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo, sasa tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/2025. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu Namba 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(CAG)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele yako na mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mapitio na Mpandekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, naomba niweke wazi kuwa hii ni bajeti ya Wizara ya Fedha, siyo Bajeti Kuu ya Serikali. Bajeti Kuu ya Serikali itasomwa tarehe 12 Juni yaani Alhamisi ya wiki ijayo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uongozi wake na mageuzi makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ambayo ameyafanya kupitia kipindi cha miaka takribani minne ya uongozi wake. Tumeshuhudia mafanikio makubwa, mujarabu kabisa katika upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi

mbalimbali ya maendeleo. Jitihada zake zimekuwa na mafanikio makubwa katika maendeleo ya Taifa letu, hususan katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na diplomasia. Hakika mama apewe maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini, mimi pamoja na Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, kumsaidia katika kutekeleza majukumu, hususan katika usimamizi wa fedha za umma pamoja na uchumi jumla. Tunapenda kuwahakikishia kuwa tutatekeleza na tutaendelea kutekeleza kikamilifu majukumu yetu ili kufikia malengo na shabaha zilizobainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu yetu kila siku ni ukusanyaji wa fedha, utafutaji na ugawaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na huduma za jamii, kazi ambayo imefanyika kikamilifu. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema Mheshimiwa Rais, hekima na busara ili kuendelea kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa hekima, busara na weledi wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Ninawashukuru pia kwa maelekezo, ushauri na miongozo ambayo wamekuwa wakiisaidia Wizara ya Fedha pamoja na Wizara zingine za kisekta katika kutimiza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa

Mabunge Duniani kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa ustadi mkubwa, umahiri mkubwa na uadilifu mkubwa. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Jimbo la Kibiti kwa kukubali pamoja na Kamati nzima ya Bajeti kwa kukubali, kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/2025 na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/2026. Maoni na ushauri na maelekezo ya Kamati yamekuwa mchango mkubwa katika kuboresha mifumo ya usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya kisera ya Wizara na Serikali kwa ujumla. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake itaendelea kutoa ushirikiano stahiki na kufanya kazi kwa karibu ili kuhakikisha kuwa tunapata maoni na maelekezo ya Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upande wa mapitio ya utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka 2024, upande wa mwenendo wa matumizi hadi Aprili, 2025; kwa mwaka wa fedha 2024/2025 mafungu nane ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 17.99 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 17.43 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara, ikiwa ni shilingi bilioni 946.45 na matumizi mengineyo shilingi trilioni 16.48. Aidha, bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni

564.67 ikijumuisha fedha za ndani shilingi bilioni 482.84 na fedha za nje ikiwa ni shilingi bilioni 81.83.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mapitio ya muda wa kati wa utekelezaji wa mpango ya bajeti ya mafungu, Wizara ilihuishiwa kutoka shilingi trilioni 17.99 hadi shilingi trilioni 16.65. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 15.91 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 642.96 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo ikiwa ni shilingi trilioni 15.15 na mishahara ikiwa shilingi bilioni 760.40. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani ikiwa ni shilingi bilioni 590.72 na fedha za nje ikiwa ni shilingi bilioni 52.24.

Mheshimiwa Spika, Fungu 45 yaani Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi *(CAG)* liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 112.73 kwa mwaka 2024/2025 ambapo shilingi bilioni 101.26 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 11.47 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Bajeti hii ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeendelea kuongezewa bajeti mwaka hadi mwaka ukilinganisha na bajeti ya miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo ambayo ni shilingi bilioni 80.62 na mishahara shilingi bilioni 20.64 na bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa shilingi bilioni 8.83 na fedha za nje ikiwa ni shilingi bilioni 2.64.

Mheshimiwa Spika, jumla ya fedha zilizopelekwa kwa mafungu nane ya Wizara ya Fedha hadi Aprili, 2025 ni shilingi trilioni 13.67 na matumizi halisi yalikuwa shilingi trilioni 13.42. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo kwa idara, vitengo na taasisi yalikuwa shilingi trilioni 2.36 na huduma ya deni la Serikali ikiwa ni shilingi trilioni 10.19, mishahara ikiwa ni shilingi bilioni 443.63 na maendeleo ikiwa ni shilingi bilioni 422.34.

Mheshimiwa Spika, vilevile hadi kufikia Aprili 2025, Fungu 045 limepokea jumla ya shilingi bilioni 99.08 na matumizi halisi ikiwa ni shilingi bilioni 91.92 na kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yakiwa ni shilingi bilioni 70.65 na mishahara ikiwa ni shilingi bilioni 16.49 na shilingi bilioni 4.78 ikiwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa

miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilipokelewa na kutumika kwa kila fungu ni kama ambavyo inavyoonekana katika ukurasa wa 66 hadi ukurasa wa 68 wa kitabu cha hotuba ya Wizara ya Fedha, kitabu cha hotuba yangu na ninaomba taarifa yote iweze kuingia katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mwenendo wa utekelezaji wa vipaumbele vya Wizara, ikiwa ni kutafuta na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi trilioni 45.10; Wizara ya Fedha ilikadiriwa kukusanya shilingi trilioni 45.10 ikiwa ni sawa na 89.7% ya makadirio yote ya Serikali ya kukusanya jumla ya shilingi trilioni 50.29 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Hadi kufikia Aprili, 2025 Wizara imefanikiwa kutafuta na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi trilioni 37.91 ikiwa ni sawa na 84.1% ya lengo la mwaka kutoka vyanzo vya ndani na nje. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 24.45 zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na Idara za Wizara zimefanikiwa kutafuta jumla ya shilingi trilioni 5.32 kama misaada na mikopo yenye masharti nafuu na shilingi trilioni 8.14 kupitia dirisha la mikopo yenye masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuimarisha na kusimamia mifumo ya usimamizi wa fedha pamoja na mali za umma, kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kuimarisha na kusimamia mifumo ya mapato, matumizi pamoja na mali za Serikali ikiwemo *IDRAS, TANCIS, MUSE, NeST, CBMS* na *GAMIS*. Hadi kufikia Aprili, 2025 Wizara imefanikiwa kuunganisha mifumo 11 ya taasisi pamoja na mashirika ya umma na Mfumo wa Uhasibu Serikalini *(MUSE)* na kuunganisha Mfumo wa *MUSE* na *CBMS* na kuwezesha maombi na utoaji wa fedha *(exchequer)* kupitia Mfumo wa *CBMS* na kuruhusu Afisa Masuuli kufanya uhamisho wa bajeti ndani ya fungu lake; ujenzi wa moduli saidizi za ulipaji wa mikataba yaani *e-Payment* na kuunganisha Mfumo wa *NeST* na Mifumo ya *MUSE;* na kuimarisha uundwaji wa moduli ya uchakataji wa uondoaji wa mali chakavu katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali Serikalini.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imekamilisha kazi ya maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Forodha *(TANCIS)* pamoja na awamu ya kwanza ya ujenzi wa

Mfumo wa Kodi za Ndani ambapo huduma za usajili wa magari na leseni za udereva zimeanza kutolewa kupitia mfumo huo. Ujenzi wa maboresho ya mifumo hiyo imesaidia kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali ambapo shughuli zote za ukadiriaji wa kodi zinafanywa kwa usahihi kupitia mifumo hii na hivyo kuondoa urasimu na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika masuala ya fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuhudumia deni la Serikali, hadi Aprili, 2025 jumla ya shilingi trilioni 10.19 zimelipwa kwa notisi za madai ya deni lililoiva, sawa na ufanisi wa 84.8% ya lengo la mwaka na kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 6.01, ikijumlisha riba ya trilioni 2.48 na mtaji shilingi trilioni 3.53 na deni la nje ikiwa ni shilingi trilioni 4.18, ikujumlisha riba ya shilingi trilioni 1.62 na mtaji ikiwa ni shilingi trilioni 2.56.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kutoa elimu ya huduma za fedha kwa wananchi katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ilipanga kuendelea kutoa elimu ya fedha kwa umma kwa lengo la kujenga uelewa na kuongeza maarifa kwa wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya fedha na kukuza huduma jumuishi za fedha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2025 elimu ya fedha imetolewa katika halmashauri 61 za Mikoa ya Lindi, Mtwara, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Mwanza, Mara na Pwani, ambapo jumla ya wananchi 49,301 walipatiwa elimu kuhusu huduma jumuishi za fedha. Aidha, jumla ya wananchi 3,419 walipatiwa elimu ya huduma za fedha kupitia Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uwezo wa Wakaguzi wa Ndani, Kamati za Ukaguzi na Waratibu wa Usimamizi wa Vihatarishi kwa mwaka 2024/2025, Wizara ilipanga kujenga uwezo kwa Wakaguzi wa Ndani, Kamati za Ukaguzi na Uratibu wa Usimamizi wa Vihatarishi katika taasisi za umma ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2025 Wakaguzi wa Ndani 485 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa Mfumo wa Uhasibu Serikalini *(MUSE)* pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini *(GePG)*; Wakaguzi wa Ndani 200 kutoka taasisi 80 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma *(NeST);* Wakaguzi wa Ndani 200 kutoka taasisi 100 walijengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Ukaguzi *(GIAMIS)* pamoja na Waratibu wa Usimamizi Vihatarishi 120 walijengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vihatarishi; na Wakaguzi wa Ndani 300 kutoka halmashauri 184 walijengewa uwezo kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato *(TAUSI)*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uhakiki binafsi wa kidijitali wa wastaafu kwa mwaka 2024/2025, Wizara ilipanga kuwezesha uhakiki binafsi wa kidijitali kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina kwa lengo la kupunguza gharama za uhakiki na usumbufu kwa wastaafu na Serikali kwa ujumla. Hadi Aprili, 2025 Wizara ilikamilisha uundwaji wa moduli kwenye Mfumo wa Malipo ya Wastaafu na Uhifadhi wa Nyaraka ili kuwezesha wastaafu kufanya uhakiki binafsi. Aidha, Wizara imefanya maboresho na kuunganisha Mfumo wa Malipo ya Wastaafu na Kuhifadhi Nyaraka na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* na Mfumo wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA)* ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wastaafu pamoja na wanufaika wengine kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kuwezesha taasisi za umma na binafsi kutumia moduli ya usimamizi wa fedha katika Mfumo wa *MUSE*. Hadi mwaka 2025 Wizara imefanikiwa kuunganisha moduli ya usimamizi wa fedha katika Mfumo wa *MUSE* kwa taasisi za umma 452 na benki 38. Moduli hiyo inawezesha kanzidata ya uhakika ya akaunti za Serikali, kurahisisha ufunguaji na ufungaji wa akaunti za Serikali, utoaji wa vibali, masurufu kwa Wizara, mikoa na idara za Serikali, uandaaji na upatikanaji wa taarifa za fedha kwa wakati na kurahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa mapato na matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/2025 upande wa sera za kiuchumi jumla; Wizara ilipanga kusimamia utekelezaji wa hatua mbalimbali za sera za uchumi jumla ili kujenga uchumi jumuishi, himilivu na endelevu. Shabaha za uchumi jumla zilizotarajiwa kufikiwa ilikuwa ni ukuaji wa pato la Taifa kufikia 5.4% mwaka 2024 kutoka ukuaji wa 5.1% mwaka 2023; mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0; mapato ya ndani kufikia 15.8% ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia 12.9% ya Pato la Taifa; nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada isiyozidi 3.0% ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2025 Wizara imesimamia utekelezaji wa hatua mbalimbali za kisera ili kufikia malengo na shabaha za uchumi jumla. Hatua hizo ni pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei, kuhudumia deni la Serikali kwa wakati, kuelekeza rasilimali fedha katika miradi inayochochea ukuaji wa uchumi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuwezesha mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya utekelezaji wa hatua hizo ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa *(GDP)* kukua kwa kiwango cha 5.5% kwa mwaka 2024 ikilinganishwa na lengo la 5.4% na ukuaji wa 5.1% kwa mwaka 2023. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 mfumuko wa bei nchini ulifikia wastani wa 3.1%, ikilinganishwa na 3.2% katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024 na wastani huu ni wastani imara kuliko nchi zote katika majirani zetu. Hadi Machi, 2025 akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,693.2, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ambapo katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Wizara ilifanikiwa kuandaa miongozo mbalimbali ya kisera, kisheria na kitaalam ikiwemo Mwongozo wa

Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026. Aidha, jumla ya ridhaa ya matumizi iliyotolewa ni shilingi trilioni 38.10 ambapo kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 25.14 ni matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 12.96 ni matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha zilizotolewa, jumla ya shilingi bilioni 996.5 zimetolewa kwa ajili ya malipo ya wakandarasi (shilingi bilioni 918.8), wazabuni (shilingi bilioni 38.4) na watumishi wa umma (shilingi bilioni 38.8).

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2024/2025 kwa upande wa mafao ya kustaafu, pensheni na mirathi; Wizara ilipanga kulipa kwa wakati mafao kwa wastaafu na warithi wanaolipwa na Hazina, kuwasilisha michango ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa malipo ya mafao, mirathi na michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Hadi Aprili, 2025 Wizara imelipa kwa wakati shilingi bilioni 315.08 kama mafao ya kiinua mgongo baada ya kupokea nyaraka zilizotosheleza Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Aidha, michango ya kisheria ya kila mwezi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ililipwa kwa wakati na malipo ya kila mwezi kama pensheni ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kufanya madai hayo yafikishwe katika mfuko uliokuwa unatakiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usimamizi wa mali za Serikali; kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji wa mali za umma katika taasisi na vituo 274; kuondosha mali chakavu, sinzia na ziada katika taasisi 240; na kuwezesha taasisi za umma 612 kuandaa, kuhuisha na kuweka kumbukumbu ya mali katika mfumo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi; kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mapendekezo ya miradi 20 ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuendesha mikutano 10 ya uhamasishaji kuhusu Sera ya Taifa ya *PPP* ya mwaka 2009 na mikutano sita ya kuhamasisha mafunzo kuhusu Sheria ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili, 2025 Wizara ilifanya tathmini ya mapendekezo ya miradi nane ya *PPP* na kutoa ushauri kwa taasisi husika. Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa Usalama Barabarani Tanzania; Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Moto; Ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi Chuo cha Elimu ya Biashara Kampasi ya Dar es Salaam; Mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu); Ujenzi wa Barabara ya Haraka ya Tozo kipande cha Kibaha - Mlandizi - Chalinze kilometa 78.9; Ujenzi na Uendeshaji wa Jengo la Biashara Kariakoo, Dar es Salaam; Mradi wa *Mlimani City* - Mkataba kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kampuni ya *Mlimani Holding*; na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Kutengeneza Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ilijengea uwezo wadau 728 kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa kuhusu utambuzi na uchambuzi wa miradi inayofaa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ununuzi wa umma; kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi na Mkakati wa Utekelezaji wake. Hadi Aprili, 2025 Wizara imekamilisha zoezi la kuandaa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi pamoja na mkakati wa utekelezaji wake. Aidha, Wizara imekamilisha utungaji wa Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 za mwaka 2024 na kutoa elimu kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa wadau 1,880 kutoka katika taasisi za umma 212.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uboreshaji wa miundombinu ya Wizara na taasisi zake; kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilipanga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi za Wizara na taasisi zake ili kuboresha mazingira ya kazi. Hadi Aprili, 2025 ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Serikali - Mtumba umefikia 93% na jengo la Ofisi za Wizara katika Mkoa wa

Geita umekamilika na kuanza kutoa huduma. Aidha, Wizara ilitoa jumla ya shilingi bilioni 6.88 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya taaluma na hosteli za wanafunzi katika taasisi za elimu zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utekelezaji wa vipaumbele Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; kwa mwaka 2024/2025 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika na Taasisi za Umma; kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalum, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na pamoja mifumo ya TEHAMA; kuimarisha matumizi ya TEHAMA; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi zake. Hadi Aprili, 2025 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi na kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu jumla ya ripoti 21 za taarifa za hesabu za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2024.

Mheshimiwa Spika, nitumie Bunge lako Tukufu kuipongeza sana Ofisi ya *CAG*; kumpongeza sana *CAG* na ofisi yake kwa kazi kubwa na ya kizalendo anayoifanya katika masuala ya ukaguzi na usimamizi wa rasilimali za Taifa letu. Aidha, kupitia kaguzi hizo jumla ya ripoti 1,730 zimeandaliwa na kutolewa kwa mchanganuo ufuatao:-

(i) Kaguzi wa Serikali Kuu, ripoti 469;
(ii) Mamlaka za Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI (787);
(iii) Mashirika na Taasisi za Umma (273);
(iv) Ukaguzi wa ufanisi (15);
(v) Ukaguzi wa kiufundi (12);
(vi) Ukaguzi maalum (53); na
(vii) Mifumo ya TEHAMA (121).

Aidha, ofisi imekamilisha kuandaa ripoti jumuishi sita za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Machi, 2025. Hongera sana *CAG*, hongera sana Ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa kazi ya kizalendo unayoifanya kwa nchi yetu na hongera sana Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kujali na kuonesha kwa vitendo masuala ya utawala bora na utawala wa kitaasisi, kuzisimamia taasisi ziweze kufanya majukumu yake kwa uwazi na kwa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa changamoto katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024/2025; baadhi ya mambo yaliyojitokeza ni kuhusu mwitikio usioridhisha kwenye upande wa matumizi ya mifumo; kushuka kwa thamani ya shilingi katika baadhi ya vipindi; na kuongezeka kwa madeni na michango ya uanachama na katika kukabiliana nayo tumeendelea kujenga uwezo wa wadau wetu kuweza kutumia mifumo; tumeendelea kutanua wigo wa mikopo kupitia fedha za kigeni; kuwezesha utekelezaji wa mikakati ya Taifa; na kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni jambo ambalo tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, taarifa zaidi tutatoa katika hotuba kubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapendekezo ya mpango na bajeti kwa Wizara na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu, Ofisi ya Taifa ya Mkaguzi ya mwaka 2024/2025, 2025/2026 ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele, ninaomba sasa kutoa Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/2026. Kwa upande wa vipaumbele 2025/2026 ni kama ifuatavyo: -

(i) Kutafuta na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi trilioni 50.98;

(ii) Kuhudumia kwa wakati deni la Serikali linaloiva kwa kiwango cha shilingi trilioni 14.22;

(iii) Kujenga mfumo wa pamoja wa kutoa ankara za malipo ya Serikali ili kuongeza ufanisi;

(iv) Kuboresha, kuunganisha na kuimarisha usalama wa mifumo ya kielektroniki; na

(v) Kuandaa Sera ya Usimamizi wa Mali za Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/2026, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni kama ifuatavyo: -

(i) Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi, ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA, ukaguzi wa ufanisi na kiufundi ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali;

(ii) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA;

(iii) Kujenga uwezo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(iv) Kujenga uwezo wa ukaguzi juu ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA;

Mheshimiwa Spika, na kwa upande wa vipaumbele vya Taasisi za Wizara kwa mwaka 2025/2026; vipaumbele vya Taasisi za Wizara ya Fedha kwa mwaka 2025/2026 vinapatikana katika ukurasa wa 55 hadi 64 katika kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Fedha imekadiria kutafuta na kukusanya jumla ya shilingi trilioni 50.17; kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kukusanya jumla ya shilingi trilioni 34.10, misaada ikiwa ni shilingi trilioni 1.07, mikopo nafuu na ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje shilingi trilioni 14.95 na maduhuli shilingi bilioni 53.54. Aidha, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi linakadiriwa kukusanya shilingi milioni 843, ikiwa ni ukodishaji wa kumbi za mikutano na kodi ya pango kutokana na upangishaji wa majengo ya ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi; kwa mwaka 2024/2025 mafungu nane ya Wizara ya Fedha yanaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya shilingi trilioni 20.19 kwa ajili ya

matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 19.43 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 757.79. Matumizi ya kawaida yanajumuisha deni la Serikali pamoja na mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 122.52 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kama nilivyosema, kwa jinsi Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan inavyoonesha kwa vitendo kwamba imedhamiria kusimamia rasilimali za umma, fedha za umma ziweze kutumika ipasavyo bila kupotea. Mwaka hadi mwaka imeendelea kuiongezea fedha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo sasa imefika shilingi bilioni 122.52 ikilinganishwa na chini ya shilingi bilioni 80 zilizokuwa zinapatikana miaka mitano iliyopita. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 110.42 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 12.10 matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi kwa mafungu nane ya kibajeti ya Wizara ya Fedha na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi unapatikana ukurasa wa 69 wa kitabu cha hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, kwa namna ya pekee tena ninapenda kumshukuru mke wangu mpendwa Bi. Neema pamoja na watoto wetu kwa upendo wao, uvumilivu, maombi na faraja ambayo wamenipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kumshukuru na kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamad Chande pamoja na timu nzima ya Wizara ya Fedha ikiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, mwalimu wangu, Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Manaibu wake wote, Naibu Katibu Mkuu Bi. Amina Shaaban; Bi. Jenifa Omolo pamoja na Elijah Mwandumbya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wamekuwa nguzo muhimu sana ya Wizara yetu na hata Bunge lako Tukufu litakiri ushirikiano ambao wataalam hawa wanautoa punde tunapoitwa katika

vikao vya Bunge na kupokea ushauri na maelekezo kutoka kwa Wabunge na Kamati za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niwashukuru wakuu wa idara, vitengo na wafanyakazi wote wa Wizara na taasisi zake, kwa ushirikiano na utekelezaji thabiti wa majukumu yao ya kila siku. Kwa moyo wa dhati kabisa, ninapenda kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na timu yake wanafanya kazi nzuri, kazi ya kutukuka, kazi ya kizalendo kwa Taifa letu. Kazi yao imeonesha mafanikio makubwa hasa ikiwa ni kubaini maeneo yenye upungufu, kupitia taarifa zake na kushauri na kutoa maelekezo na Bunge lako Tukufu ni mashahidi jinsi ambavyo hatua kubwa imefikiwa na nchi yetu katika masuala ya usimamizi wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo kwa michango yao ya hali na mali ambapo ushiriki wao katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo umeleta tija na umejitokeza bayana katika maeneo tofauti tofauti ambayo tunashirikiana nayo.

Mheshimiwa Spika, nikiwa namalizia kipekee kabisa kwa kihistoria kabisa niwapongeze timu ya Singida kwa kuwafunga Simba liingie kwenye *Hansard* hili, goli tatu moja ni ushindi mkubwa sana mambo yaliyotokea kule Babati na nimemuomba radhi Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba sikuwatuma mimi nilikuwa kwenye majukumu aliyonituma, kwa hiyo hayo walifanya tu wenyewe na wamefuzu kucheza fainali, hiyo ni hatua kubwa na Mheshimiwa Kingu pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Singida wanakusubiri upongeze kama unavyofanyaga kwa timu zingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu, Waheshimiwa Wabunge na umma wa Watanzania umesikiliza kwa umakini na narudia tena wasikose kusikiliza Bajeti Kuu ya Serikali itakayoelezea mafanikio ya kihistoria yaliyofikiwa katika nchi yetu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan tutakayowasilisha tarehe 12 Juni, siku ya

Alhamisi ya wiki ijayo panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha ambayo ni *www.mof.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, kwa unyenyekevu mkubwa sasa naomba kutoa hoja, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHESHIMIWA DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB,) AKIWASILISHA BUNGENI MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25 inayoundwa na mafungu tisa (9) ambayo ni: Fungu 001 – Deni la Serikali; Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 013 – Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu; Fungu 021 – Hazina; Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu; Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 050 – Wizara ya Fedha; na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26 ya mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

**1.1 Salamu za Shukrani**

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25 na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, napenda kutumia fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uongozi wa mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hakika, katika kipindi cha miaka minne (4) ya uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio mujarabu katika upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali ya maendeleo. Jitihada zake zimekuwa na mafanikio katika maendeleo ya Taifa letu, hususan katika nyanja za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidiplomasia. **Mama apewe maua yake**.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutuamini, mimi pamoja na Naibu Waziri, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb,), kumsaidia kutekeleza majukumu yake, hususan katika usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla. Tunapenda kumhakikishia kuwa, tumetekeleza na tutaendelea kutekeleza kikamilifu majukumu yetu ili kufikia malengo na shabaha zilizobainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Maeneo ya kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku ni utafutaji, ukusanyaji na ugawaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za serikali, ikiwemo miradi mikubwa ya maendeleo pamoja na huduma za jamii. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azidi kumjalia afya njema, hekima na busara ili kutekeleza majukumu yake kwa manufaa na ustawi wa watanzania wote.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb,), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb,), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa hekima, busara na weledi wao katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa mafanikio makubwa. Aidha, ninawashukuru kwa maelekezo, ushauri na miongozo yao ambayo imenisaidia mimi pamoja na Naibu Waziri, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb,), kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa ustadi, umahiri na uadilifu mkubwa. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb,), Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya kukusaidia wewe kuendesha shughuli za Bunge kwa weledi.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Jimbo la Kibiti kwa kukubali kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25 na kupitisha Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/26. Maoni na ushauri wa Kamati umekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha mifumo ya usimamizi na utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Aidha, napenda kuwashukuru waheshimiwa wabunge wote kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika utekelezaji wa majukumu ya kisera ya wizara na Serikali kwa ujumla. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zake, itaendelea kutoa ushirikiano stahiki na kufanya kazi kwa karibu ili kuhakikisha tunatoa huduma stahiki kwa wananchi na wadau wetu wa maendeleo.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano mkubwa katika kuwaletea maendeleo. Ninawaahidi kuwa nitaendelea kushirikiana nao kufanya kazi bila kuchoka ili kutimiza malengo tuliyojiwekea ya kuboresha hali ya maisha, huduma za jamii na kuimarisha uchumi wa wananchi katika Jimbo la Iramba Magharibi. Nitumie nafasi hii kuwaambia kuwa, nitaendelea kuwatumikia kwa unyenyekevu, uadilifu, uwazi na uwajibikaji ili kutekeleza kwa ufanisi yale yote yaliyoainishwa kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

### 1.2 Salamu za Pongezi

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 2025. Kwa mafanikio makubwa tuliyoyapata chini ya uongozi wake, nawaasa watanzania wamuunge mkono ili aendelee kuleta mageuzi ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Balozi, Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa mgombea mwenza. Mheshimiwa Balozi, Dkt. Nchimbi ni mwanasiasa mkongwe mwenye uzoefu mkubwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali na jumuiya za kimataifa. Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema, hekima na maarifa katika kupigania na kutetea maslahi ya Chama Cha Mapinduzi na taifa kwa ujumla.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake makini na kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. Aidha, nampongeza kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya urais wa Zanzibar kwa kipindi cha pili cha Awamu ya Nane katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika Oktoba 2025.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima na taadhima, nawapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kazi kubwa waliyoifanya ya uwakilishi wa wananchi katika kupigania maendeleo ya nchi yetu na majimbo yao. Kazi imefanyika na matokeo yanaonekana. Hongereni sana na nawatakia kila la heri katika mchakato wa kuomba ridhaa ya wananchi kurejea tena katika jengo hili kupitia uchaguzi mkuu ujao. Aidha, kutokana na kazi kubwa mliyoifanya katika majimbo yenu, nina imani mtachaguliwa kwa kishindo.

### 1.3 Salamu za Pole

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na watanzania wote, kufuatia kifo cha Hayati Cleopa David Msuya, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Fedha aliyefariki tarehe 7 Mei 2025. Tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, amina.

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, natoa pole kwako wewe binafsi na Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Rorya na waziri katika wizara mbalimbali, Mheshimiwa Prof. Philemon Mikol Sarungi na Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema aliyewahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Naungana na wabunge wenzangu na watanzania wote kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hiyo. Aidha, natoa pole kwa waheshimiwa wabunge na wananchi wote waliofiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao kutokana na maradhi, ajali, majanga na matukio mbalimbali yaliyotokea katika nchi yetu. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, amina.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo ya utangulizi, naomba kuwasilisha hoja iliyo mbele yetu kwa mjadala na idhini ya Bunge lako Tukufu. Hoja yangu imegawanyika katika maeneo makuu matatu (3) ambayo ni: Muhtasari wa Majukumu ya Wizara; Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25; na Mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26.

## 2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 619A la tarehe 30 Agosti 2023. Majukumu hayo ni pamoja na: Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla, fedha, ununuzi wa umma na ubia kati ya sekta ya umma na binafsi; kuandaa na kusimamia miongozo na utekelezaji wa

bajeti ya serikali; kuratibu upatikanaji wa fedha na kuimarisha uhusiano na taasisi za kifedha za kikanda na kimataifa; kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi; kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina; kusimamia fedha na mali za serikali; kusimamia deni la serikali; kusimamia masuala ya pamoja ya fedha kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; kusimamia maendeleo ya sekta ya fedha; na kusimamia takwimu rasmi za kitaifa.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

### 3.1 Mwenendo wa Matumizi hadi Aprili 2025

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2024/25, mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya **shilingi trilioni 17.99** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 17.43** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha **mishahara shilingi bilioni 946.45** na matumizi mengineyo **shilingi trilioni 16.48.** Aidha, bajeti ya matumizi ya maendeleo ilikuwa **shilingi bilioni 564.67** ikijumuisha fedha za ndani **shilingi bilioni 482.84** na fedha za nje **shilingi bilioni 81.83.**

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, wakati wa mapitio ya muda wa kati wa utekelezaji wa mpango na bajeti, bajeti ya mafungu ya Wizara ya Fedha ilihuishwa kutoka **shilingi trilioni 17.99** hadi **shilingi trilioni 16.55**. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 15.91** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 642.96** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo **shilingi trilioni 15.15** na mishahara **shilingi bilioni 760.40**. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani **shilingi bilioni 590.72** na fedha za nje **shilingi bilioni 52.24**.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi liliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 112.73** kwa mwaka 2024/25 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 101.26** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 11.47** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo**.** Matumizi ya kawaida yanajumuisha matumizi mengineyo **shilingi bilioni**

**80.62** na mishahara **shilingi bilioni 20.64.** Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha fedha za ndani **shilingi bilioni 8.83** na fedha za nje **shilingi bilioni 2.64.**

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, jumla ya fedha zilizopokelewa kwa mafungu nane (8) ya wizara kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo ni **shilingi trilioni 13.71,** sawa na **asilimia 86.5** ya bajeti. Aidha, matumizi halisi yalifikia **shilingi trilioni 13.46**, sawa na **asilimia 98.2** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo kwa idara, vitengo na taasisi yalikuwa **shilingi trilioni 2.36**, huduma ya deni la Serikali **shilingi trilioni 10.19**, mishahara **shilingi bilioni 443.63** na maendeleo **shilingi bilioni 456.80**. Vilevile, hadi Aprili 2025, Fungu 045 limepokea jumla ya **shilingi bilioni 99.08**, sawa na **asilimia 87.9** ya makisio ya mwaka 2024/25. Matumizi halisi yalifikia **shilingi bilioni 91.92**, sawa na **asilimia 92.8** ya fedha zilizopokelewa. Kati ya kiasi hicho, matumizi mengineyo yalikuwa **shilingi bilioni 70.65**, mishahara **shilingi bilioni 16.49** na shilingi **bilioni 4.78** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilipokelewa na kutumika kwa kila fungu ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Na.1 – 3.**

### 3.2 Mwenendo wa Utekelezaji wa Vipaumbele vya Wizara

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa vipaumbele vya mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

#### 3.2.1 Kukusanya na Kutafuta Mapato ya Jumla ya Shilingi Trilioni 45.10

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, mafungu ya Wizara ya Fedha yalikadiriwa kukusanya jumla ya **shilingi trilioni 45.10**, sawa na asilimia 89.7 ya makadirio yote ya serikali ya kukusanya jumla **ya shilingi trilioni 50.29**. Hadi Aprili 2025, wizara imefanikiwa kutafuta na kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi trilioni 37.91,** sawa na asilimia 84.1 ya lengo la mwaka kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Kati ya kiasi hicho**, shilingi trilioni 24.45** zimekusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na idara za wizara zimefanikiwa kutafuta jumla ya **shilingi trilioni 5.32** kama misaada na mikopo yenye masharti nafuu na **shilingi trilioni 8.14** kupitia dirisha la mikopo yenye masharti ya kibiashara.

### 3.2.2 Kuimarisha na Kusimamia Mifumo ya Usimamizi wa Fedha na Mali za Umma

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuimarisha na kusimamia mifumo ya mapato, matumizi na mali za serikali ikiwemo IDRAS, TANCIS, MUSE, NeST, CBMS na GAMIS. Hadi Aprili 2025, wizara imefanikiwa kuunganisha mifumo 11 ya taasisi na mashirikia ya umma na Mfumo wa Uhasibu Serikalini (MUSE); kuunganisha mfumo wa MUSE na CBMS ili kuwezesha maombi na utoaji fedha (exchequer) kupitia mfumo wa CBMS na kuruhusu Afisa Masuuli kufanya uhamisho wa bajeti ndani ya fungu lake; ujenzi wa moduli saidizi ya ulipaji wa mikataba (*e-Payment*) na kuiunganisha na mfumo wa NeST na mfumo wa MUSE; na kukamilisha uundwaji wa moduli ya uchakataji wa mali uchakavu na moduli ya uondoaji wa mali chakavu katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS).

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara inaendelea kuimarisha na kuboresha mifumo ya usimamizi wa mali za serikali ikiwemo: Kuhamisha kanzidata mbili (GeRAS na GAMIS Portal) kwenda kwenye teknolojia ya chanzo huria (Open- Source) kwa lengo la kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo, kuongeza usalama, kuimarisha udhibiti wa teknolojia na kuondoa utegemezi katika uendeshaji wa mifumo. Aidha, wizara kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imekamilisha kazi ya maboresho ya Mfumo wa Usimamizi wa Forodha (TANCIS) pamoja na ujenzi wa Mfumo wa Kodi za Ndani (IDRAS) ambapo huduma za magari na leseni za udereva zimeanza kutolewa kupitia mfumo huo. Mifumo hiyo itasaidia kuongeza mapato ya serikali, ambapo shughuli zote za ukadiriaji wa kodi zitafanywa kwa usahihi kupitia mfumo huo na hivyo kuondoa urasimu, kuongeza uwazi na uwajibikaji.

**24.** ***Mheshimiwa Spika***, wizara inaendelea na ujenzi wa Mfumo wa Ghala la Takwimu za masuala ya fedha na uchumi ambao utaunganishwa na mifumo ya Benki Kuu ya Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Waziri Mkuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, wizara imefanikiwa kuingiza kwenye mfumo taarifa za matumizi kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na takwimu za mfumuko wa bei na Pato la Taifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Mfumo huu unatumika

kuhifadhi takwimu mbalimbali za uchumi na fedha kwa ajili ya uchambuzi na kuwezesha serikali kutoa maamuzi sahihi, na kwa wakati.

**3.2.3 Kuhudumia Deni la Serikali**

**25. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, jumla ya **shilingi trilioni 10.19** zimelipwa kwa notisi za madai ya deni lililoiva, sawa na asilimia 84.8 ya lengo la mwaka. Kati ya kiasi hicho, jumla ya malipo ya deni la ndani ni **shilingi trilioni 6.01**, ambapo riba ni **shilingi trilioni 2.48** na mtaji **shilingi trilioni 3.53** na deni la nje ni **shilingi trilioni 4.18**, riba ikiwa ni **shilingi trilioni 1.62** na mtaji **shilingi trilioni 2.56**. Aidha, wizara imefanya maboresho ya mfumo wa usimamizi wa takwimu za madeni (CS Meridian) na kuunganishwa na mifumo mingine ya usimamizi wa fedha za umma, ikiwemo Mfumo wa Benki Kuu ya Tanzania – CBS, GSS na Mfumo wa Uhasibu Serikalini - MUSE. Hatua hii imeiwezesha serikali kutoa taarifa za deni la serikali kwa shilingi ya Tanzania kwa wakati na kwa usahihi.

**3.2.4 Kutoa Elimu ya Huduma za Fedha kwa Wananchi 26. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuendelea kutekeleza programu ya elimu ya fedha kwa kutoa elimu ya fedha kwa lengo la kujenga uelewa na kuongeza maarifa ya masuala ya fedha kwa umma na kukuza huduma jumuishi za fedha nchini. Hadi Aprili 2025, elimu ya fedha ilitolewa katika halmashauri 61 za mikoa ya Lindi, Mtwara, Kilimanjaro, Arusha, Morogoro, Mwanza, Mara na Pwani ambapo jumla ya wananchi 49,271 walipatiwa elimu kuhusu huduma jumuishi za fedha. Aidha, jumla ya wananchi 3,419 walipatiwa elimu ya huduma za fedha kupitia Maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yaliyofanyika katika Mkoa wa Mbeya. Vilevile, wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Upatikanaji wa Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati wa mwaka 2023/24 – 2028/29 kwa lengo la kuongeza wigo wa vyanzo vya mitaji kwa wajasiriamali, ambapo wajasiriamali 640 kutoka mikoa ya Morogoro, Pwani, Mtwara, Lindi na Tanga wamepatiwa mafunzo.

### 3.2.5 Kujenga Uwezo kwa Wakaguzi wa Ndani, Kamati za Ukaguzi na Waratibu wa Usimamizi wa Vihatarishi

**27. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kujenga uwezo kwa wakaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi na waratibu wa usimamizi wa vihatarishi katika taasisi za umma ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma. Hadi Aprili 2025, wakaguzi wa ndani 485 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa Mfumo wa Uhasibu Serikalini - MUSE pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato Serikalini - GePG; wakaguzi wa ndani 200 kutoka taasisi 80 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa Mfumo wa Ununuzi wa Umma - NeST; wakaguzi wa ndani 200 kutoka taasisi 100 walijengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Ukaguzi - GIAMIS; waratibu wa usimamizi wa vihatarishi 120 walijengewa uwezo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Vihatarishi - GERMIS; na wakaguzi wa ndani 300 kutoka halmashauri 184 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato - TAUSI. Aidha, wakaguzi wa ndani 50 kutoka taasisi 50 walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa taarifa za fedha kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa na kimataifa. Mafunzo hayo yameimarisha uwezo wa wakaguzi wa ndani katika kukagua mifumo ya kielektroniki na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma.

### 3.2.6 Kuwezesha Uhakiki Binafsi wa Kidijiti kwa Wastaafu

**28. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuwezesha uhakiki binafsi wa kidijiti kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina kwa lengo la kupunguza gharama za uhakiki na usumbufu kwa wastaafu na serikali kwa ujumla.

Hadi Aprili 2025, wizara ilikamilisha uundwaji wa moduli kwenye Mfumo wa Malipo ya Wastaafu na Kuhifadhi Nyaraka – TPPS ili kuwezesha wastaafu kufanya uhakiki binafsi. Aidha, wizara imefanya maboresho na kuunganisha Mfumo wa Malipo ya Wastaafu na Kuhifadhi Nyaraka - TPPS na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa - NIDA na Mfumo wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini – RITA ili kuboresha huduma zinazotolewa kwa wastaafu pamoja na wanufaika wengine kwa mujibu wa sheria.

### 3.2.7 Kuwezesha Matumizi ya Moduli ya Usimamizi wa Fedha

**29. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuwezesha taasisi za umma na binafsi kutumia moduli ya usimamizi wa fedha katika mfumo wa MUSE. Hadi Aprili 2025, wizara imefanikiwa kuunganisha moduli ya usimamizi wa fedha katika mfumo wa MUSE kwa taasisi za umma 452 na benki 38. Moduli hiyo imewezesha kanzidata ya uhakika ya akaunti za serikali, kurahisisha ufunguaji na ufungaji wa akaunti za serikali, utoaji wa vibali vya masurufu kwa wizara, mikoa na idara za serikali, uandaaji na upatikanaji wa taarifa za fedha kwa wakati na kurahisisha usimamizi na ufuatiliaji wa mapato na matumizi ya serikali. Aidha, taasisi za umma 284 na benki 38 zilipatiwa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli ya usimamizi wa fedha.

### 3.3 Utekelezaji wa Majukumu Mengine ya Wizara

### 3.3.1 Usimamizi wa Sera za Uchumi Jumla

**30. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kutekeleza sera za uchumi jumla ili kujenga uchumi jumuishi, himilivu na endelevu. Shabaha za uchumi jumla zilizotarajiwa kufikiwa ni Pato la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023; mfumuko wa bei kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0; mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa; mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa; nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

**31. *Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, wizara imechukua hatua mbalimbali za kisera ili kufikia malengo na shabaha za uchumi jumla. Hatua hizo ni pamoja na kudhibiti mfumuko wa bei, kuhudumia deni la serikali kwa wakati, kuelekeza rasilimali fedha katika miradi inayochochea ukuaji wa uchumi, kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa fedha za umma. Matokeo ya utekelezaji wa mikakati hiyo yamechangia ukuaji halisi wa Pato la Taifa (GDP) kwa kiwango cha asilimia 5.5 mwaka 2024 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5.4,

na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, mfumuko wa bei nchini ulifikia wastani wa asilimia 3.1, ikilinganishwa na asilimia 3.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Vilevile, hadi Machi 2025, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,693.2, kiasi kilichotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 3.3.2 Usimamizi wa Bajeti ya Serikali

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa bajeti ya serikali ambapo katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, wizara ilifanikiwa kuandaa miongozo mbalimbali ya kisera, kisheria na kitaalamu ikiwemo Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26. Aidha, jumla ya ridhaa ya matumizi iliyotolewa ni **shilingi trilioni 38.10**, ambapo kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 25.14** ni matumizi ya kawaida na **shilingi trilioni 12.96** ni matumizi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha zilizotolewa, jumla ya **shilingi bilioni 996.5** zimetolewa kwa ajili ya malipo ya wakandarasi **(shilingi bilioni 918.8),** wazabuni **(shilingi bilioni 38.4)** na watumishi wa umma **(shilingi bilioni 38.8).**

### 3.3.3 Huduma za Mafao ya Kustaafu, Pensheni na Mirathi

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kulipa kwa wakati mafao kwa wastaafu na warithi wanaolipwa na Hazina, kuwasilisha michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kwa wakati na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa malipo ya mafao, mirathi na michango ya kisheria kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii. Hadi Aprili 2025, wizara imelipa kwa wakati **shilingi bilioni 315.08** kama mafao ya kiinua mgongo baada ya kupokea nyaraka kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Aidha, michango ya kisheria ya kila mwezi kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii iliwasilishwa kwa wakati na malipo ya kila mwezi ya pensheni ya mifuko ya hifadhi ya jamii yalifanyika kwa wakati baada ya kupokea hati za madai.

### 3.3.4 Usimamizi wa Mali za Serikali

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji wa mali za umma katika taasisi na vituo 274; kuondosha mali chakavu, sinzia na ziada katika taasisi 240; na

kuwezesha taasisi za umma 612 kuandaa, kuhuisha na kuweka kumbukumbu ya mali katika mfumo wa GAMIS. Hadi Aprili 2025, wizara ilifanya ufuatiliaji wa mali za umma kwenye taasisi 371; kuondosha mali chakavu, sinzia na ziada katika taasisi 116 zenye thamani ya shilingi bilioni 1.79; na taasisi 386 zimewezeshwa kuandaa, kuhuisha na kuweka kumbukumbu ya mali zenye thamani ya shilingi trilioni 31.22 katika mfumo wa GAMIS.

**3.3.5 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi**

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mapendekezo ya miradi 20 ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi na kuendesha mikutano 10 ya uhamasishaji kuhusu Sera ya Taifa ya PPP ya mwaka 2009 na mikutano sita (6) ya uhamasishaji na mafunzo kuhusu sheria ya PPP.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, wizara ilifanya ufuatiliaji na tathmini ya mapendekezo ya miradi nane (8) ya PPP na kutoa ushauri kwa taasisi husika. Miradi hiyo ni: Mradi wa Usalama Barabarani Tanzania; Mradi wa Ujenzi wa Vituo vya Ukaguzi wa Lazima wa Vyombo vya Moto; Ujenzi wa Hosteli za Wanafunzi Chuo cha Elimu ya Biashara Kampasi ya Dar es Salaam; Mradi wa Uendeshaji wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu); Ujenzi wa Barabara ya Haraka ya Tozo kipande cha Kibaha - Mlandizi - Chalinze Km 78.9; Ujenzi na Uendeshaji wa Jengo la Biashara Kariakoo, Dar es Salaam; Mradi wa Mlimani City - Mkataba kati ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kampuni ya Mlimani Holding; na Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Kutengeneza Vitambulisho vya Taifa. Aidha, wizara iliendesha mikutano mitano (5) ya uhamasishaji kuhusu Sera ya Taifa ya PPP ya mwaka 2009 kwa wadau wa maendeleo, taasisi za umma, mashirika ya umma, mifuko ya hifadhi ya jamii na umma kwa ujumla.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** wizara kupitia Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ilijengea uwezo wadau 728 kutoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa kuhusu utambuzi na uchambuzi wa miradi

inayofaa kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

### 3.3.6 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**38. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi na Mkakati wa Utekelezaji wake na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya taasisi nne (4) za usimamizi wa ununuzi wa umma. Hadi Aprili 2025, wizara imekamilisha zoezi la kuandaa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025 pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake. Aidha, wizara imekamilisha utungaji wa Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 za Mwaka 2024 na kutoa elimu kuhusu Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa wadau 1,180 kutoka katika taasisi za umma 212.

### 3.3.7 Udhibiti wa Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Silaha za Maangamizi

**39. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu (FATF) na kuhamasisha wadau kuwasilisha taarifa za miamala shuku na takwimu za utakasishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi kwa wakati. Hadi Aprili 2025, wizara iliratibu utekelezaji wa vipengele vyote 21 vya mpango kazi wa FATF na hivyo kukidhi vigezo vya kuondolewa kwenye orodha ya nchi zilizo katika usimamizi wa karibu. Aidha, Wizara imeboresha mfumo maalumu wa kuratibu takwimu za matukio ya utakasishaji fedha haramu, kufanya ukaguzi kwa watoa taarifa 72 Tanzania Bara (Arusha, Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza) na Zanzibar na kutoa elimu kwa wadau 1,120 kutoka taasisi 24 kuhusu usimamizi na udhibiti wa utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

### 3.3.8 Masuala ya Pamoja ya Fedha kati ya Tanzania Bara (SJMT) na Zanzibar (SMZ)

**40. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuchambua mapato na matumizi ya muungano kwa mwaka 2022/23, 2023/24 na 2024/25; kuandaa na kutoa mapendekezo

kuhusu ukusanyaji na mgawanyo wa mapato yanayotokana na utekelezaji wa majukumu ya mamlaka za udhibiti na usimamizi wa masuala ya muungano; kujenga uelewa kwa wadau kutoka pande zote mbili za muungano kuhusu masuala ya uhusiano wa kifedha kati ya SJMT na SMZ na kufanya ukarabati wa jengo la Serikali Na.12 Barabara ya Kivukoni, Dar es Salaam kwa ajili ya ofisi za Tume. Hadi Aprili 2025, Wizara imekamilisha uchambuzi na kuandaa taarifa ya mwenendo wa mapato na matumizi ya muungano kuanzia mwaka 2022/23 hadi 2024/25; na kufanya stadi na kuandaa mapendekezo kuhusu ukusanyaji na mgawanyo wa mapato yatokanayo na utekelezaji wa majukumu ya mamlaka za udhibiti na usimamizi wa mambo ya muungano. Aidha, wizara imeendesha semina ya kujenga uelewa kuhusu masuala yanayohusu uhusiano wa kifedha kati ya SJMT na SMZ kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria na maafisa wa Wizara ya Fedha SJMT na SMZ, Ofisi ya Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar.

### 3.3.9 Uboreshaji wa Miundombinu ya Ofisi za Wizara na Taasisi zake

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi za wizara na taasisi zake ili kuboresha mazingira ya kazi. Hadi Aprili 2025, ujenzi wa jengo la wizara katika Mji wa Serikali - Mtumba umefikia asilimia 93 na jengo la ofisi za wizara katika Mkoa wa Geita umekamilika na kuanza kutoa huduma. Aidha, wizara ilitoa jumla ya **shilingi bilioni 6.88** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya taaluma na hosteli za wanafunzi katika taasisi za elimu zilizo chini ya wizara. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 4.00** zimetolewa kwa Taasisi ya Uhasibu Tanzania kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa majengo ya taaluma katika Kampasi ya Mwanza ambapo ujenzi umekamilika na kuanza kutoa huduma, Kampasi ya Kigoma ujenzi umefikia asilimia 85 na Kampasi ya Zanzibar ujenzi umefikia asilimia 8; **shilingi milioni 650** zimetolewa kwa Chuo cha Uhasibu Arusha kwa ajili ya ujenzi wa hosteli (asilimia 85) na mradi wa jengo la utawala ambao umekamilika na kuanza kutumika; na **shilingi bilioni 2.23** zimetolewa kwa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa bweni la wanafunzi awamu ya pili katika

Kampasi ya Mwanza (asilimia 40) na ujenzi wa jengo la taaluma Miyuji (asilimia 30). Vile vile, wizara imetoa **shilingi milioni 831.90** kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Soko la Bidhaa Tanzania ambao umefikia asilimia 10.5.

**3.3.10 Usimamizi wa Masuala ya Utafiti na Ubunifu**

**42. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, wizara ilipanga kuandaa Mwongozo wa Utafiti na Ubunifu na kufanya tafiti nne (4) za kisera. Hadi Aprili 2025, wizara imeandaa Mwongozo wa Utafiti na Ubunifu na kutoa mafunzo kwa watumishi wa wizara kuhusu matumizi ya mwongozo huo. Aidha, wizara ilifanya tafiti nne (4) za kisera ikiwemo: Utafiti wa Ufanisi wa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Wateja katika Sekta ya Fedha; Utafiti wa Ufanisi wa Masoko ya Mitaji na Dhamana katika Kuwezesha Upatikanaji wa Mitaji ya Muda Mrefu kwa Taasisi za Umma na Binafsi nchini; Utafiti wa Namna ya Kukuza Matumizi ya Huduma za Fedha na Malipo kwa njia za Kidijiti; na Utafiti wa Matokeo ya Kiuchumi Yatokanayo na Maboresho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Tanzania Bara.

**3.4 Mwenendo wa Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara**

**43. *Mheshimiwa Spika,*** wizara inatekeleza baadhi ya majukumu kupitia taasisi zilizo chini yake ikiwemo Taasisi za elimu; bodi za kitaalamu na kitaaluma; taasisi za benki na fedha; taasisi za usimamizi wa kodi, ununuzi na ugavi na michezo ya kubahatisha; taasisi za uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi; na takwimu. Utekelezaji wa vipaumbele vya taasisi ni kama ifuatavyo:

**3.4.1 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi**

**44. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilipanga kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya **shilingi trilioni 29.42**. Hadi Aprili 2025, Mamlaka ilikusanya mapato ya **shilingi trilioni 24.45**, sawa na asilimia 101.5 ya lengo la kukusanya **shilingi trilioni 24.09**, sawa na ukuaji wa asilimia 14.8.

**45. *Mheshimiwa Spika,*** ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya kodi umetokana na sababu mbalimbali ikiwemo: Uboreshaji wa

Mfumo wa Usimamizi wa Forodha (TANCIS) na Mfumo wa Dirisha Moja la Pamoja (TeSW) ambayo imesaidia kuimarisha ufuatiliaji wa shehena za mizigo, kupunguza urasimu na kuongeza uwazi; kuendelea kuhamasisha wananchi kulipa kodi kwa hiari; na kuimarisha doria na ukaguzi kwa kutumia teknolojia, kuendesha kampeni za uelimishaji na ushirikishwaji wa jamii, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa na kuchukua hatua mbalimbali za kisheria dhidi ya wafanyabiashara waliokamatwa kujihusisha na biashara za magendo.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Bodi ya Rufani za Kodi, Baraza la Rufani za Kodi na Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi zilitarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri na malalamiko ya kodi mara yanapowasilishwa. Hadi Aprili 2025, Baraza la Rufani za Kodi limesajili jumla ya mashauri 254 ya kodi bishaniwa ya shilingi 817,027,757,648.37 ambapo mashauri 234 ya kodi bishaniwa ya shilingi 442,263,474,483.79 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, Bodi ya Rufani za Kodi imesajili mashauri ya kodi 1,033 (rufaa 948 na maombi 85) ya kodi bishaniwa ya shilingi 2,124,375,044,554.47 na imesikiliza na kutolea uamuzi mashauri 671 (rufaa 579 na maombi 92) ya kodi bishaniwa ya shilingi 3,511,702,017,126.81. Vilevile, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi imepokea malalamiko 50 ya kodi, imesuluhisha malalamiko 43 na malalamiko saba (7) yapo katika hatua mbalimbali za usuluhishi. Taasisi pia imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kupokea na Kuchakata Malalamiko na Taarifa za Kodi ili kuwezesha uwasilishaji wa malalamiko kidijiti.

### 3.4.2 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalamu

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** taasisi za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara ya Fedha zimeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kuhusu masuala mbalimbali ya fedha, mipango na takwimu. Kwa mwaka 2024/25, taasisi tano (5) za mafunzo na elimu zilitarajia kudahili jumla ya wanafunzi 86,804 katika ngazi ya astashahada, stashahada, shahada na shahada ya uzamili. Hadi Aprili 2025, taasisi hizo zilidahili jumla ya wanafunzi 82,225, sawa na ufanisi wa asilimia 94.7 ya lengo, ikiwemo ngazi ya astashahada 13,439, stashahada 13,856, shahada 48,696 na shahada ya uzamili

6,234. Aidha, jumla ya watumishi 267 wa taasisi hizo wamewezeshwa kujiendeleza kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu, sawa na asilimia 57.5 ya lengo. Vilevile, taasisi zilifanya jumla ya tafiti 39, sawa na asilimia 68.4 ya lengo na kutoa huduma elekezi 13, sawa na asilimia 54.2 ya lengo la mwaka.

**3.4.3 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha**

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ilipanga kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kutoa mafunzo ya uandaaji na ukaguzi wa taarifa za fedha kwa wahasibu na wakaguzi 12,500; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65 za ukaguzi; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa watahiniwa 14,540; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu 1,451 wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji; na kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 150.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Bodi imesajili wahasibu na wakaguzi 244 katika ngazi mbalimbali za uanachama, sawa na asilimia 81.3 ya lengo la mwaka; kutoa mafunzo ya kitaaluma ya uandaaji na ukaguzi wa hesabu kwa wahasibu na wakaguzi 13,545, sawa na asilimia 108.3 ya lengo; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 64, sawa na asilimia 85.3; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 52 za ukaguzi, sawa na ufanisi wa asilimia 80; kuendesha mitihani ya kitaaluma katika ngazi mbalimbali kwa awamu ya kwanza kwa watahiniwa 7,566, sawa na ufanisi wa asilimia 52; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji kwa awamu kwanza kwa watahiniwa 1,861, sawa na asilimia 128.3 ya lengo; na kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 131, sawa na ufanisi wa asilimia 87.3 ya lengo la mwaka.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi ilipanga kufanya ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ya Bodi kwa taasisi za umma na binafsi na kuhuisha kanzidata ya wataalamu wa ununuzi na ugavi; kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi; kuendesha mafunzo na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa watahiniwa 6,500; na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000. Hadi Aprili 2025, bodi imefanya ukaguzi kwa taasisi za umma na binafsi 211; kuhuisha kanzidata na kusajili wataalamu 1,952, sawa na asilimia 56 ya lengo la mwaka; kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 3,706, sawa na ufanisi wa asilimia 57; na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 1,403, sawa na asilimia 35 ya lengo la mwaka.

### 3.4.4 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma ilipanga kukamilisha ujenzi wa moduli tatu (3) za mfumo wa NeST; kufanya tafiti tatu (3) kuhusu matumizi ya fomula ya mabadiliko ya bei katika miradi ya ujenzi, ununuzi endelevu na matumizi ya *force account*, na ununuzi kwa njia ya mzabuni mmoja ikilinganishwa na ushindani; kuandaa na kupitia nyaraka sanifu 42 na miongozo tisa (9) ya ununuzi wa umma kwa matumizi ya taasisi nunuzi; kutoa elimu kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa watumishi 8,160 kutoka katika wizara, taasisi za serikali, ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri, wazabuni 4,000, asasi za kiraia 100, makundi maalumu 110 na wanafunzi 4,000 wa vyuo vikuu; na kufanya ukaguzi wa ununuzi kwa taasisi nunuzi 500.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma imekamilisha ujenzi wa moduli tatu (3) za mfumo wa NeST ambazo ni usajili wa watumiaji (*e-Registration*), uchakataji wa zabuni kimtandao (*e-Tendering*) na usimamizi wa mikataba (*e-Contract Management*). Aidha, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa moduli saidizi za upekuzi wa mikataba (*Contract Vetting*), ukaguzi na ukidhi wa ununuzi (*Compliance Audit Tool*) na malalamiko na rufaa za zabuni.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imefanya utafiti kuhusu fomula ya mabadiliko ya bei katika miradi 93 ya ujenzi inayotekelezwa na taasisi za serikali. Aidha, Mamlaka imefanya mapitio ya nyaraka sanifu 43 za zabuni, mikataba 43, nyaraka sanifu mbili (2) pamoja na kuandaa hati msako mbili (2) kwa ajili ya ununuzi katika ngazi za chini za serikali za mitaa; na kufanya mapitio ya miongozo nane (8) na kuandaa miongozo mipya minne (4) ya ununuzi ambayo ni Mwongozo wa Utoaji Upendeleo katika Ununuzi wa Umma, Mwongozo wa Jumla wa Ununuzi Endelevu, Mwongozo wa Ununuzi katika Ngazi za Chini za Serikali za Mitaa na Mwongozo wa Ununuzi kwa Kutumia Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka imetoa elimu kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa watumishi 53,206 kutoka katika wizara, taasisi za serikali, ofisi za wakuu wa mikoa na halmashauri, wazabuni 2,943, asasi za kiraia 121, makundi maalum 2,876 na wanafunzi wa vyuo vikuu 243. Aidha, Mamlaka imefanya ukaguzi wa tathmini ya uzingatiaji wa sheria (*Compliance Audit*) kwa taasisi nunuzi 620 na ukaguzi wa thamani ya fedha (Value for Money) kwa taasisi nunuzi 106. Matokeo ya ukaguzi yanaonesha ongezeko la ukidhi wa sheria kutoka asilimia 65.1 mwaka 2022/23 hadi asilimia 75.5 mwaka 2023/24 pamoja na miradi kupata hadhi ya thamani ya fedha kwa kiwango cha wastani.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini ulipanga kununua magari manne (4) ya kusafirishia mafuta; kuunganisha mfumo wa GIMIS na pampu na matenki ya mafuta; kuanzisha utoaji wa huduma za mafuta kwa kutumia kadi kupitia mfumo wa GIMIS; kujenga ofisi, ghala na kituo cha mafuta katika Wilaya ya Mbarali (Mbeya), Masasi (Mtwara), Korogwe (Tanga) na Jiji la Arusha; na ujenzi wa ofisi ya Mkoa Dar es Salaam. Hadi Aprili 2025, Wakala umenunua magari sita (6) ya kusafirishia mafuta, sawa na ufanisi wa asilimia 150; mshauri elekezi kwa ajili ya kuanzisha utoaji wa huduma ya mafuta kwa kutumia kadi kupitia mfumo wa GIMIS amepatikana na anaendelea na ukusanyaji wa mahitaji ya mfumo; na mshauri elekezi kwa ajili ya usanifu wa ujenzi wa vituo vya mafuta, ofisi,

ghala na kituo cha mafuta katika Wilaya ya Mbarali (Mbeya), Masasi (Mtwara) na Korogwe (Tanga) na ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam amepatikana na utayarishaji wa michoro na makadirio ya ujenzi umekamilika.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma ilipanga kusajili na kusikiliza rufaa 55; kutoa mafunzo kwa wazabuni 800 kuhusu moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa; na kutoa mafunzo kwa wakuu wa idara na vitengo 300 vya ununuzi na sheria kuhusu usimamizi wa malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki. Hadi Aprili 2025, rufaa 44 zimesajiliwa ambapo kati ya hizo, rufaa 40 zimesikilizwa na kutolewa uamuzi na rufaa 4 zinaendelea kufanyiwa kazi. Aidha, mafunzo kuhusu moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa yametolewa kwa wazabuni 605, sawa na ufanisi wa asilimia 75.63 na kwa wakuu wa idara na vitengo vya ununuzi, TEHAMA na sheria wapatao 1,428, sawa na ufanisi wa asilimia 476.

**3.4.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ilipanga kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mitaji Ubia (*venture capital*); kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida za masoko ya mitaji; kuidhinisha bidhaa mpya mbili (2) ili kuwezesha taasisi na kampuni katika sekta ya umma na binafsi kupata fedha za kugharamia biashara na miradi ya maendeleo; na kuboresha mifumo ya usimamizi wa shughuli za masoko ya mitaji. Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania lilipanga kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Soko linavyofanya kazi na faida zake; na kuboresha Mfumo wa Mauzo kulingana na mazingira ya bidhaa husika.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imeidhinisha bidhaa mpya 15 za masoko ya mitaji, sawa na ufanisi wa asilimia 750 na kuwezesha upatikanaji wa shilingi bilioni 481.28 na imeendesha semina 35 kuhusu fursa na faida zinazopatikana kwenye masoko ya mitaji kwa makundi ya vijana, wanawake, wajasiriamali, wabunge, taasisi za umma na binafsi na watu wenye mahitaji maalumu. Aidha, Mamlaka

imeendesha mashindano kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kuhusu masoko ya mitaji na uwekezaji ambapo wanafunzi 18,738 walishiriki. Vilevile, Mamlaka imeboresha na kuanza kutumia mfumo unaozingatia vihatarishi katika usimamizi wa shughuili za masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa - *Risk Based Supervision (RBS)*.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Soko la Bidhaa Tanzania lilitoa elimu kwa wadau 4,383 wa soko katika mikoa 19 ikiwemo Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Katavi, Rukwa, Kigoma, Mwanza, Dodoma, Lindi, Tanga, Mbeya, Morogoro, Arusha, Manyara, Mtwara, Ruvuma, Mara, na Geita. Aidha, Soko limeboresha Mfumo wa Mauzo wa Kidijiti kulingana na mahitaji ya bidhaa husika na kuwezesha biashara ya bidhaa 10 kuuzwa kidigiti ambapo bidhaa tisa (9) ni za kilimo (ufuta, korosho, kakao,mbaazi, dengu, soya, choroko, kahawa na chai) na moja (1) ni madini ya vito. Vile vile, mauzo ya bidhaa katika soko yalifikia shilingi trilioni 2.4.

### 3.4.6 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25**,** Benki Kuu ya Tanzania ilipanga kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo mpya unaotumia riba ya Benki Kuu ya Tanzania; kudhibiti kiwango cha riba za mikopo ya siku saba (7) baina ya benki; kudhibiti mwenendo wa sera ya fedha ili kuendana na malengo ya utekelezaji wa programu ya *Extended Credit Facility* (ECF); kufuatilia taasisi za fedha kupanga riba na viwango vya kubadilisha fedha kwa kuzingatia nguvu ya soko; na kushiriki katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya benki ili kudhibiti akiba ya fedha za kigeni.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, utekelezaji wa sera ya fedha kwa kutumia mfumo unaotumia Riba ya Benki Kuu - CBR uliwezesha kudhibiti mfumuko wa bei kuendelea kubaki ndani ya lengo la asilimia 5 na kuendana na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC). Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1. Aidha, riba ya mikopo ya siku saba (7)

katika soko la fedha baina ya benki ilikuwa tulivu katika kipindi cha miezi 10 ya mwanzo ya mwaka 2024/25, na kubakia ndani ya wigo wa riba ya benki kuu wa asilimia 4 hadi 8. Hali ya ukwasi ilikuwa ya kutosha, ikilingana na mahitaji ya kiuchumi na kuwezesha ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kufikia wastani wa asilimia 15.1 katika kipindi hicho. Vilevile, Benki Kuu ya Tanzania ilifanikiwa kufikia malengo ya utekelezaji wa programu ya ECF inayofadhiliwa na IMF, ikijumuisha rasilimali halisi za ndani za benki na akiba halisi ya fedha za kigeni.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuimarisha utulivu wa uchumi; kusimamia sekta ya fedha na kuhakikisha inaendelea kuwa imara, thabiti, na himilivu; na kuhimiza benki na taasisi za kifedha kutumia mfumo wa utambuzi wa historia za wakopaji ili kupunguza mikopo chechefu. Aidha, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kusimamia sheria, kanuni na miongozo inayolenga kumlinda mtumiaji wa huduma za fedha, kutoa elimu ya fedha na kuongeza huduma jumuishi za fedha. Jitihada hizo zimewezesha kupunguza viwango vya riba za mikopo kutoka wastani wa asilimia 15.3 Juni 2024 hadi asilimia 15.2 Aprili 2025.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 56.54; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 20.83 kutoka shilingi bilioni 18.79 ya mwaka 2023; kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 197 ikilinganishwa na shilingi bilioni 161.6 iliyotolewa mwaka 2023; kuongeza thamani ya mali za benki kufikia shilingi bilioni 866.23 kutoka shilingi bilioni 606.94 mwaka 2023; na kufuatilia marejesho ya mikopo shilingi bilioni 70 kutoka kwa wateja.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2024, Benki ilizalisha mapato ya shilingi bilioni 60.73, sawa na asilimia 107.41 ya lengo la mwaka. Aidha, benki ilitengeneza faida kabla ya kodi ya shilingi bilioni 24.59, sawa na asilimia 118.1 ya lengo na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 286.38, sawa na asilimia 145.4 ya lengo. Vilevile, thamani ya mali za benki ilifikia shilingi bilioni 924.76,

sawa na asilimia 106.7 ya lengo na urejeshwaji wa mikopo ulifikia shilingi bilioni 124.49, sawa na asilimia 177.9 ya lengo la mwaka.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Benki ya Maendeleo TIB ilipanga kuongeza mtaji wa benki hadi kufikia shilingi bilioni 204.61 kutoka shilingi bilioni 86.61 mwaka 2023; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 89.02 ikilinganishwa na shilingi bilioni 9.74 mwaka 2023; kuongeza mali za benki hadi shilingi bilioni 545.48 kutoka shilingi bilioni 425.15 mwaka 2023; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya benki shilingi bilioni 17.44 na mikopo iliyo katika mizania ya benki shilingi bilioni 30.38; na kusimika mifumo mitatu (3) ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2024, mtaji wa msingi wa benki ulifikia shilingi bilioni 90.23, sawa na asilimia 44.1 ya lengo la mwaka; benki ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 19.52, sawa na asilimia 21.9 ya lengo; na mali za benki zilifikia shilingi bilioni 453, sawa na asilimia 83.1 ya lengo. Aidha, benki ilikusanya shilingi bilioni 6.1, sawa na asilimia 34.1 ya lengo kutoka kwenye mikopo iliyo nje ya mizania na shilingi bilioni 19.37 kutoka kwenye mikopo iliyo katika mizania ya benki, sawa na ufanisi wa asilimia 63.8. Vilevile, benki imesimika mifumo miwili (2) ya TEHAMA, sawa na asilimia 66.67 ikiwa ni hatua ya kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Mifumo hiyo ni: Mfumo wa Usimamizi wa Ukaguzi wa Ndani na Mfumo wa Ukusanyaji Matukio katika Mifumo.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Benki ya Biashara Tanzania ilipanga kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 225; kukuza faida ya benki kabla ya kodi shilingi bilioni 37.3; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,173; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,340; kukuza mali za benki hadi shilingi bilioni 1,701 kutoka shilingi bilioni 1,389.3 mwaka 2023; kukuza mtaji wa benki hadi shilingi bilioni 147 kutoka shilingi bilioni 118.9 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja kufikia 881,122 kutoka wateja 831,122 mwaka 2023; na kukamilisha ujenzi na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mwenendo wa mikopo.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2024, Benki ilizalisha mapato ya shilingi bilioni 236.64, sawa na asilimia 105 ya lengo na kukuza faida ya benki kabla ya kodi shilingi bilioni 43.80, sawa na asilimia 117 ya lengo. Aidha, benki ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 1,151, sawa na asilimia 98 ya lengo; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,286, sawa na asilimia 96 ya lengo; kukuza mali za benki hadi shilingi bilioni 1,741, sawa na asilimia 102 ya lengo kutoka shilingi bilioni 1,389.3 mwaka 2023. Vilevile, benki ilikuza mtaji hadi shilingi bilioni 150.85, sawa na asilimia 103 ya lengo kutoka shilingi bilioni 118.9 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja 82,937 kufikia 914,059, sawa na asilimia 110 kutoka wateja 831,122 mwaka 2023; na kukamilisha ujenzi na usimikaji wa mfumo wa kielektroniki wa tathmini na ufuatiliaji wa mikopo.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF ulipanga kutoa mikopo ya shilingi bilioni 48 kwa wajasiriamali 48,000; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 3.28 kutoka shilingi bilioni 1.89 mwaka 2023; kukuza mtaji hadi shilingi bilioni 65.48 kutoka shilingi bilioni 61.14 mwaka 2023; kuongeza idadi ya wateja hadi 48,000 kutoka wateja 37,024 mwaka 2023; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya mfuko shilingi bilioni 2 na mikopo iliyo katika mizania shilingi bilioni 48.53; na kuzalisha mapato ya jumla ya shilingi bilioni 11.03.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Desemba 2024, Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 45.20, sawa na asilimia 94 ya lengo, kwa wajasiriamali wadogo 55,743, sawa na asilimia 116 ya lengo; faida iliyotengenezwa kabla ya kodi ilifikia shilingi bilioni 1.09, sawa na asilimia 94 ya lengo; mtaji wa Mfuko ulifikia shilingi bilioni 58.99, sawa na asilimia 90.09 ya lengo. Aidha, shilingi bilioni 1.49, sawa na asilimia 74.5 ya lengo zilikusanywa ikiwa ni marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya mfuko. Vilevile, shilingi bilioni 41.63, sawa na asilimia 95.9 ya lengo zilikusanywa ikiwa ni mikopo iliyo katika mizania; na Mfuko ulizalisha mapato ya shilingi bilioni 8.32, sawa na ufanisi wa asilimia 75.4 ya lengo la mwaka.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS ilipanga kuongeza rasilimali za mifuko hadi shilingi bilioni 2,642.7 kutoka shilingi bilioni 2,238.15

mwaka 2023/24; kuongeza idadi ya wawekezaji hadi 367,500 kutoka 328,578 mwaka 2023/24; na kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 28.03 kutoka shilingi bilioni 18.82 mwaka 2023/24. Hadi Aprili 2025, rasilimali za mifuko ziliongezeka hadi shilingi bilioni 2,971.89 kutoka shilingi bilioni 2,238.15, sawa na ufanisi wa asilimia 132.8; idadi ya wawekezaji ilifikia 445,163, sawa na ufanisi wa asilimia 121.1; na faida kabla ya kodi ilifikia shilingi bilioni 31.3, sawa na asilimia 111.7 ya lengo.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania ilipanga kujenga mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ya tozo na ada za bima; kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi jijini Dodoma kwa gharama ya shilingi bilioni 3.80; kufanya ukaguzi kwa wadau wa bima 309 (kampuni 25, matawi 30, madalali 66, mawakala 150, benkiwakala 10, matawi 20 na wauza bima kidijiti nane (8)); kuchambua mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 36; kutoa elimu ya bima kwa umma; kuidhinisha bidhaa mpya tano (5) zinazokidhi mahitaji ya watu wenye kipato cha chini; na kuongeza wasajili wapya wa bima 105.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Mamlaka imekamilisha ujenzi wa mfumo wa kielektroniki na kuanza kutumika katika ukusanyaji wa mapato ya tozo za ada ya bima (*TIRA Billing System*); kupokea na kufanya uchambuzi wa mikataba ya bima mtawanyo kwa kampuni 38; kuendelea na ujenzi wa jengo la mamlaka jijini Dodoma ambao umefikia asilimia 89; na kufanya ukaguzi kwa wadau wa bima 135 ikiwemo kampuni za bima na matawi 39, kampuni za bima mtawanyo moja (1), watoa huduma kidijiti mmoja (1), washauri bima mtawanyo mmoja (1), benkiwakala bima nane (8), madalali wa bima sita (6) na mawakala 65. Aidha, Mamlaka imesajili na kutoa leseni kwa wadau wapya wa bima 962 kama ifuatavyo; watoa huduma ya afya 138, wakala wa kibenki 35, gereji 210, wakala wa bima 334, washauri bima 144, kampuni ya bima 1, wachunguzi bima 7, watoa huduma za bima kidijiti 17, watathmini na wakadiria hasara 64, watoa bima za afya kwa wote 1, washauri bima mtawanyo 11. Vilevile, Mamlaka imeidhinisha bidhaa mpya nane (8), sawa

na asilimia 160 ya lengo, kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye kipato cha chini.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Shirika la Bima la Taifa lilipanga kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu bidhaa na huduma za shirika; kuboresha utoaji huduma kwa wateja kupitia uandikishaji wa Cheti cha Ubora (ISO 9001:2015) katika ofisi 11 za kanda; kupunguza muda wa malipo ya madai kutoka siku 16 hadi saba (7); kuongeza wateja wapya 324 wa bidhaa za taasisi kutoka wateja 222 mwaka 2023/24; kubuni bidhaa mpya mbili (2) na kuboresha bidhaa tatu (3) ili kuendana na mahitaji ya soko; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 58.94 kutoka shilingi bilioni 38.69; na kuongeza mapato ya taasisi kutoka shilingi bilioni 244.34 hadi shilingi bilioni 314.78.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Shirika limetoa elimu kwa umma kuhusu bidhaa na huduma za bima kupitia kipindi maalumu kwenye vyombo vya habari na kampeni katika mikoa ya Arusha, Dodoma, Singida, Morogoro na Pwani; kuboresha utoaji huduma kwa kuzingatia matakwa ya Cheti cha Ubora (ISO 9001:2015) katika ofisi 11 za kanda, sawa na asilimia 100 ya lengo la mwaka; kupunguza muda wa malipo ya madai kutoka siku 16 hadi siku saba (7) baada ya kupokea nyaraka kamili za madai, sawa na ufanisi wa asilimia 100; kuongeza wateja wapya 1,729 wa bidhaa za shirika, sawa na ufanisi wa asilimia 533.64; kubuni bidhaa mpya moja (1) (*Group Life Education)* ambayo inatoa fursa kwa watanzania kuwekeza kidogo kidogo ili watoto wao wanufaike na kinga ya bima pindi wazazi au walezi wanapopatwa na majanga ikiwemo kifo au ulemavu wa kudumu, sawa na asilimia 50; kuboresha bidhaa tatu (3) za bima ya maisha ambazo ni *Super Education Life Assurance*, *Flex Life Assurance* na *Bima Flex* kuendana na mahitaji ya soko, sawa na ufanisi wa asilimia 100; na kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 203.82, sawa na asilimia 65 ya lengo. Aidha, hadi Machi 2025, Shirika limezalisha faida ya shilingi bilioni 22.06 kabla ya kodi, sawa na asilimia 37.4 ya lengo la mwaka.

**3.4.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi**

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kuendelea kutoa takwimu rasmi za kijamii, kiuchumi na mazingira kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Takwimu, SURA 351; kuchambua, kusambaza na kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 katika ngazi ya halmashauri, majimbo, kata, shehia, mtaa, kijiji na kitongoji; kuendelea na Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2024; kufanya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na Ufuatiliaji wa Kaya wa Mwaka 2024/25; kufanya utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2023/24; na kufanya Sensa ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu Zanzibar ilipanga kujenga majengo ya ofisi katika mkoa wa Pemba, Lindi na Simiyu kwa gharama ya shilingi bilioni 3.4 kila moja kwa ajili ya kuhudumia mkoa wa Pemba, Kanda ya Kusini na Kanda ya Ziwa.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imeendelea kutoa kwa wakati takwimu rasmi za mwenendo wa uchumi ikiwemo Pato la Taifa - GDP, Fahirisi za bei za Taifa za mlaji - NCPI, Fahirisi za Bei za Mzalishaji - PPI, Fahirisi za Uzalishaji Viwandani – IIP, Fahirisi za Bei za Biashara - TPI na takwimu za Mfumuko wa Bei wa Taifa wa kila mwezi. Aidha, Ofisi imeendelea kutoa ripoti mbalimbali za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 ikiwemo Ripoti ya Makadirio ya Idadi ya Watu Ngazi ya Taifa 2023 – 2050; Ripoti za takwimu za msingi za kidemografia, kijamii, kiuchumi na mazingira kwa mikoa 31 Tanzania Bara na Zanzibar; na Ripoti tano (5) za kina (monographs) za sensa ambazo ni vizazi na ndoa, hali ya vifo, hali ya ulemavu, elimu na kujua kusoma na kuandika, na mienendo ya mabadiliko ya idadi ya watu na athari zake katika maendeleo ya nchi. Vilevile, tafiti kuhusu watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka 2024, mapato na matumizi ya kaya binafsi, utafiti wa kilimo wa mwaka 2023/24 na sensa ya uzalishaji bidhaa viwandani zinatarajiwa kukamilika mwaka 2025/26. Kadhalika, Ofisi imesambaza matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kwa makundi 6 katika ngazi ya Taifa, mikoa tisa (9) na halmashauri 18. Pia, mkandarasi kwa ajili ya

ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa ya Pemba, Lindi na Simiyu amepatikana na maandalizi ya awali ya ujenzi yamekamilika.

### 3.4.8 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha

**78. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania ilipanga kutoa leseni 12,456 ikijumuisha leseni mpya 1,126 na kuhuisha leseni 11,330; kufanya kaguzi 12 kwa kuzingatia vihatarishi; kutekeleza operesheni nne (4) za kudhibiti michezo haramu ya kubahatisha; kukusanya mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha ya jumla ya shilingi bilioni 24.89; kuendelea kuelimisha jamii kuhusu athari hasi za michezo ya kubahatisha; na kusimamia uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa. Hadi Aprili 2025, Bodi imetoa leseni 8,466, sawa na asilimia 67.9 ya lengo ikijumuisha leseni mpya 2,008 na zilizohuishwa 6,458; kufanya kaguzi tisa (9) katika michezo ya kasino, kubashiri matokeo na mashine dubwi (Slot Machines), sawa na asilimia 75 ya lengo; na kufanya operesheni tatu (3) za kudhibiti michezo haramu ya kubahatisha, sawa na asilimia 75 ya lengo. Aidha, Bodi imekusanya jumla ya shilingi bilioni 17.42, sawa na asilimia 70 ya lengo la mwaka na kufanya programu tatu (3) za kuelimisha jamii juu ya michezo ya kubahatisha, faida na hasara pamoja na dhana nzima ya kucheza kwa kiasi (responsible gaming). Vilevile, Bodi imeteua kampuni ya Ithuba Tanzania Ltd kuwa mwendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

## 4.0 MCHANGO WA TAASISI ZA WIZARA KATIKA MFUKO MKUU WA HAZINA YA SERIKALI

**79. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/25, taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha zilitarajia kuchangia Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 233.99, Kati ya kiasi hicho, gawio ni shilingi bilioni 224.15 na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 9.84. Hadi Aprili 2025, taasisi zimefanikiwa kuchangia jumla ya shilingi bilioni 322.54, sawa na asilimia 137.8 ya lengo la mwaka, ambapo shilingi bilioni 311.87 zimetokana na gawio, sawa na ufanisi wa asilimia 139.1 na michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi shilingi bilioni 10.67, sawa na ufanisi wa asilimia 108.4.

## 5.0 MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA VIPAUMBELE VYA FUNGU 045 - OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

**80.** ***Mheshimiwa spika,*** kwa mwaka 2024/25, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilipanga kufanya ukaguzi wa rasilimali za umma kwa serikali kuu, mamlaka za serikali za mitaa na mashirika na taasisi za umma; kufanya kaguzi za kiufundi, ufanisi, maalumu, kiuchunguzi, miradi ya maendeleo na mifumo ya TEHAMA; kuimarisha matumizi ya TEHAMA ndani ya ofisi; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi za mikoa.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi na kuwasilisha katika Bunge lako Tukufu jumla ya ripoti 21 za taarifa za hesabu za fedha kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2024. Kupitia kaguzi zilizofanyika, jumla ya ripoti 1,730 zimeandaliwa na kutolewa kwa mchanganuo ufuatao: ukaguzi wa serikali kuu (469), mamlaka za serikali za mitaa na OR-TAMISEMI (787), mashirika na taasisi za umma (273), ukaguzi wa ufanisi (15), kiufundi (12), maalumu (53) na mifumo ya TEHAMA (121). Aidha, Ofisi imekamilisha kuandaa ripoti jumuishi sita (6) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Machi 27, 2025.

## 6.0 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI NA MIKAKATI YA KUKABILIANA NAZO

### 6.1 Changamoto

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2024/25, wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:

i. mwitikio usioridhisha wa wadau wa ununuzi katika sekta ya umma na binafsi kutumia Mfumo wa Ununuzi wa Umma - NeST, na hivyo kuathiri muda wa ununuzi wa vifaa na huduma pamoja na ucheleweshaji huduma na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

ii. kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani na kusababisha ongezeko la gharama za malipo ya deni la serikali na malipo mengine nje ya nchi; na

iii. kuongezeka kwa madeni na michango ya uanachama katika taasisi za kikanda na kimataifa.

**6.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto zilizojitokeza, wizara inaendelea kuchukua hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

i. kuendelea kujenga uwezo kwa wadau wa sekta ya umma na binafsi na kuhamasisha matumizi ya Mfumo wa Ununuzi wa Umma - NeST ili kufanikisha ununuzi kwa wakati;

ii. kutanua wigo wa mikopo kupitia fedha za kigeni zaidi ya sarafu moja (Currency Diversification) ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa dola ya Marekani. Hii itasaidia kupunguza athari za kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu moja maalumu (dola ya Marekani);

iii. kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni; na

iv. kuangalia uwezekano wa kujiondoa uanachama katika baadhi ya taasisi ambazo gharama ya michango ni kubwa kuliko faida za moja kwa moja au fursa za kiuchumi na kidiplomasia ni kidogo.

**7.0 MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26**

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa vipaumbele na majukumu ya wizara, taasisi zake na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2024/25, sasa napenda kuwasilisha Mapendekezo ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2025/26 kwa idhini ya Bunge lako Tukufu.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpango na bajeti ya wizara kwa mwaka 2025/26 umeandaliwa kwa kuzingatia sera, mikakati, sheria, mipango na miongozo mbalimbali ya kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya CCM

ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Hotuba ya Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne; Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 uliofanyiwa mapitio ya muda wa kati; mikakati na makubaliano ya kikanda na kimataifa; na masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabianchi na UKIMWI.

### 7.1 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2025/26

**86. *Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya mafungu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo:

i. kutafuta na kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi trilioni 50.17** kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya serikali;

ii. kuhudumia kwa wakati deni la serikali linalotarajiwa kuiva la jumla ya **shilingi trilioni 14.22**;

iii. kujenga mfumo wa pamoja wa kutoa ankara za malipo ya serikali ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato;

iv. kuboresha, kuunganisha na kuimarisha usalama wa mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha na mali za umma; na

v. kuandaa Sera ya Usimamizi wa Mali za Umma.

### 7.2 Vipaumbele vya Mpango na Bajeti ya Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2025/26

**87. *Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo:

i. kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi, ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA, ukaguzi wa ufanisi na kiufundi ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma;

ii. kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukaguzi wa hesabu za fedha, ufanisi, kiufundi na thamani halisi ya fedha;

iii. kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa Fedha za Umma na kamati za kisekta kuhusu mamlaka na majukumu ya CAG, uchambuzi wa ripoti za ukaguzi pamoja na kutambua mbinu za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo; na

iv. kujenga uwezo wa wakaguzi juu ya matumizi ya mifumo ya TEHAMA inayotumika katika ukusanyaji wa mapato na matumizi, ukaguzi wa wakati halisi (real- time audit), ukaguzi wa ufanisi na kiufundi, ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na mabadiliko ya viwango vya ukaguzi vya kimataifa.

### 7.3 Vipaumbele vya Taasisi Chini ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka 2025/26

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha kwa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo:

#### 7.3.1 Usimamizi wa Kodi na Mashauri ya Kodi

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajia kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ya jumla ya **shilingi trilioni 34.10**. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 32.31 ni mapato ya kodi na shilingi trilioni 1.79 ni mapato yasiyo ya kodi. Aidha, Mamlaka itaendelea kuboresha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa mapato ya serikali ikiwemo TANCIS na IDRAS, pamoja na kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa umma ili kuhamasisha ulipaji kodi kwa hiari na kupunguza upotevu wa mapato unaotokana na udanganyifu wa taarifa za miamala na biashara za magendo.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Rufani za Kodi inatarajia kuendelea kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi 675 (rufaa 585 na maombi 90) yanayotokana na maamuzi ya Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania; kuandaa Juzuu ya Taarifa za Sheria za Kodi Tanzania; na kuhuisha Sheria ya Rufani za Kodi, Sura 408. Aidha, Baraza la Rufani za Kodi

linatarajia kusajili, kusikiliza na kutolea maamuzi mashauri ya kodi 300. Vilevile, Taasisi ya Usuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi inatarajia kuendelea kupokea na kutatua malalamiko ya walipakodi; kutengeneza mfumo wa kuwasilisha malalamiko na taarifa za kodi kwa njia ya simu; na kutoa elimu kwa umma kuhusu majukumu ya taasisi.

### 7.3.2 Mafunzo, Tafiti na Ushauri wa Kitaalam

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, taasisi tano (5) za elimu zilizo chini ya Wizara ya Fedha zinatarajia kudahili jumla ya wanafunzi 97,957. Kati ya idadi hiyo, Chuo cha Usimamizi wa Fedha kinatarajia kudahili wanafunzi 18,400, Taasisi ya Uhasibu Tanzania wanafunzi 33,581, Chuo cha Uhasibu Arusha wanafunzi 27,420, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini wanafunzi 15,556 na Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika wanafunzi 3,000. Aidha, taasisi hizo zinatarajia kuendeleza jumla ya watumishi 339 kitaaluma katika ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu, kufanya tafiti 58 na kutoa huduma elekezi 31.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Taasisi ya Uhasibu Tanzania inatarajia kuendelea na ujenzi wa majengo ya taaluma katika kampasi ya Kigoma na Zanzibar; Chuo cha Uhasibu Arusha kuendelea na ujenzi wa jengo la uhasibu na fedha pamoja na hosteli kampasi ya Dodoma; na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kuendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi awamu ya pili katika Kampasi ya Mwanza na ujenzi wa jengo la taaluma Miyuji, Dodoma.

### 7.3.3 Usimamizi wa Taaluma na Utaalamu wa Masuala ya Fedha

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu inatarajia: Kusajili wahasibu na wakaguzi wa hesabu 300 katika ngazi mbalimbali za uanachama; kutoa mafunzo ya uandaaji na ukaguzi wa taarifa za fedha kwa wahasibu na wakaguzi 14,500; kufanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha kwa taasisi na kampuni 75; kufanya ukaguzi wa ubora wa kazi za ukaguzi wa hesabu kwa kampuni 65; kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 15,120; kutoa mafunzo ya astashahada ya juu ya viwango vya uandaaji wa hesabu katika sekta ya umma kwa wahitimu 150; kuendesha

mitihani ya kitaaluma kwa wahitimu 1,950 wenye sifa za nje ya nchi wanaosimamia miradi ya maendeleo na uwekezaji; na kutoa ushauri wa kiufundi kuhusu matumizi ya viwango mbalimbali katika uandaaji wa hesabu na ukaguzi kwa taasisi na kampuni nane (8). Aidha, Bodi inatarajia kukamilisha uundaji wa mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya ukusanyaji, utambuzi na uhakiki wa taarifa za fedha zilizokaguliwa nchini kwa lengo la kuondoa uwezekano wa kuzalisha taarifa za fedha zaidi ya moja kwa taasisi/kampuni ili kukwepa kodi.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia: Kufanya ukaguzi wa ukidhi wa Sheria ya Bodi kwa taasisi za umma na binafsi 1,000; kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi; kudahili na kuendesha mitihani ya kitaaluma kwa watahiniwa 4,000; kuendesha mafunzo na ushauri wa kitaalamu kwa wataalamu 6,500 wa ununuzi na ugavi; na kufanya maboresho ya Mfumo wa Usajili wa Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi Mtandaoni Toleo la II (ORS).

**7.3.4 Usimamizi wa Ununuzi wa Umma**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma inatarajia: Kujenga moduli mbili (2) katika mfumo wa NeST ambazo ni moduli ya minada ya ununuzi na moduli ya katalogia ya bidhaa na huduma; kufanya kaguzi za ukidhi wa sheria ya ununuzi wa umma na kaguzi za thamani halisi ya fedha kwa taasisi 570; na kujenga uwezo kwa wadau 2,000 kutoka mamlaka za serikali za mitaa kuhusu matumizi ya mfumo wa NeST na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini umepanga: Kuendelea na ujenzi wa ofisi ya Mkoa wa Dar es Salaam; kuwezesha upatikanaji wa ithibati ya kimataifa katika utoaji wa huduma “ISO Certified”; kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa vituo vya kujaza gesi kwenye magari kwa mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Dodoma; kuwezesha uunganishwaji wa mfumo wa kiutendaji wa Wakala wa GIMIS na mifumo mingine ya serikali ya MUSE na GAMIS; na kukamilisha ujenzi wa ofisi, ghala na kituo cha mafuta

katika wilaya ya Mbarali (Mbeya), Masasi (Mtwara) na Korogwe (Tanga).

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma imepanga: Kusajili na kushughulikia rufaa 55 na maombi matano (5); kuandaa Mpango Mkakati wa Mamlaka wa 2026/27 – 2030/31; kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kupitia mfumo wa NeST kwa wazabuni 1,680 na wakuu wa idara na vitengo vya ununuzi, TEHAMA na sheria wapatao 1,500; na kuboresha moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko kupitia mfumo wa NeST.

### 7.3.5 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana imepanga: Kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na faida za masoko ya mitaji kwa watu milioni 15; kuongeza watendaji na wataalamu wa masoko ya mitaji kwa asilimia 10 na kufikia 993; na kushirikiana na wadau wa masoko ya mitaji katika kubuni na kuanzisha bidhaa mpya sita (6). Aidha, Soko la Bidhaa Tanzania linatarajia kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa na mfumo mzima wa uuzaji wa bidhaa kupitia soko la bidhaa na kusimamia mauzo ya bidhaa 11 (ufuta, dengu, choroko, mbaazi, soya, kakao, madini, kahawa, korosho, chai na mifugo).

### 7.3.6 Usimamizi wa Benki na Huduma za Fedha

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Benki Kuu ya Tanzania imepanga: Kudhibiti mfumuko wa bei usizidi asilimia tano (5) na kuhakikisha utulivu wa uchumi; kudhibiti viwango vya riba ili kuakisi mahitaji ya ukwasi katika soko; kudhibiti akiba ya fedha za kigeni ili kuwezesha uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); kuimarisha utulivu wa thamani ya shilingi dhidi ya sarafu za kigeni; na kuboresha mifumo ya malipo ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu nchini.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania imepanga: Kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 69.53; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi shilingi bilioni 30.65 kutoka shilingi bilioni 24.68 kwa mwaka 2024; kutoa mikopo ya

jumla ya shilingi bilioni 300 ikilinganishwa na shilingi bilioni 286.38 kwa mwaka 2024; kuongeza thamani ya mali za benki kufikia shilingi trilioni 1.13 kutoka shilingi bilioni 917.41 kwa mwaka 2024; na kufuatilia marejesho ya mikopo shilingi bilioni 120.00.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Benki ya Maendeleo TIB imepanga: Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 20; kuongeza mali za benki hadi shilingi bilioni 478 kutoka shilingi bilioni 453 mwaka 2024; na kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya benki shilingi bilioni 11.14 na mikopo iliyo ndani ya mizania ya benki shilingi bilioni 25.03. **102.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Benki ya Biashara Tanzania imepanga: Kuzalisha mapato ya shilingi bilioni 316; kukuza faida ya Benki kabla ya kodi ya shilingi bilioni 65; kutoa mikopo ya shilingi bilioni 1,483; kukusanya amana za wateja shilingi bilioni 1,858; kukuza mali za Benki hadi shilingi bilioni 2,274 kutoka shilingi bilioni 1,738 mwaka 2024; kukuza mtaji wa Benki hadi shilingi bilioni 193 kutoka shilingi bilioni 151 mwaka 2024; na kuongeza idadi ya wateja hadi 1,214,059 kutoka wateja 914,059 mwaka 2024.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha - SELF umepanga: Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 48 kutoka shilingi bilioni 45.2 mwaka 2024; kukuza faida kabla ya kodi hadi shilingi bilioni 1.14 kutoka shilingi bilioni 1.09 mwaka 2024; kukuza mtaji hadi shilingi bilioni 61.0 kutoka shilingi bilioni 58.99 mwaka 2024; kuongeza idadi ya wateja hadi 60,000 kutoka wateja 55,743 mwaka 2024; kukusanya marejesho ya mikopo iliyo nje ya mizania ya Mfuko shilingi bilioni 2.0 kutoka shilingi bilioni 1.49 na mikopo iliyo ndani ya mizania shilingi bilioni 53.05 kutoka shilingi bilioni 41.63 mwaka 2024; na kuzalisha mapato ya jumla ya shilingi bilioni 12.13 kutoka shilingi bilioni
8.32 mwaka 2024.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - UTT AMIS imepanga: Kuongeza rasilimali za mifuko hadi shilingi bilioni 3,516.15 kutoka shilingi bilioni 2,971.89 mwaka 2024/25; kuongeza idadi ya wawekezaji hadi 580,000 kutoka 445,163 mwaka 2024/25; na kukuza faida kabla ya kodi

hadi shilingi bilioni 37.40 kutoka shilingi bilioni 27.38 mwaka 2024/25.

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imepanga: Kujenga mfumo wa kielektroniki wa usimamizi wa shughuli za bima mtawanyo; kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kusomana na mifumo mingine ya taasisi za serikali; kufanya ukaguzi wa wadau wa bima 168 (kampuni za bima 20 na matawi 22, madalali 20, mawakala 80, wakala wa kibenki 10, matawi ya wakala wa kibenki 8, na watoa huduma za bima Kidijiti watano (5) na washauri bima mtawanyo watatu (3); kufanya mapitio ya Sheria ya Bima Sura 394; na kusajili na kutoa leseni mpya 100 za huduma za bima.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Shirika la Bima Tanzania linapanga: Kuongeza faida ghafi hadi shilingi bilioni 67.48 kutoka shilingi bilioni 58.94 mwaka 2024/25; kufanya mapitio ya bidhaa nane (8) za bima za mali na ajali pamoja na bidhaa tatu (3) za bima za Maisha; na kuboresha vituo viwili (2) vya kuhifadhi data na urejeshaji huduma baada ya majanga.

**7.3.7 Usimamizi wa Takwimu Rasmi**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imepanga: Kuendelea na Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa Mwaka 2024; kukamilisha utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na Ufuatiliaji wa Kaya wa Mwaka 2024/25; kufanya Utafiti wa Sekta Isiyo Rasmi Nchini; kufanya utafiti wa Kilimo wa Mwaka 2024/25; na kukamilisha ujenzi wa majengo ya ofisi katika mkoa wa Pemba, Lindi na Simiyu.

**7.3.8 Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania imepanga: Kutoa leseni 14,124 ikijumuisha leseni mpya 845 na kuhuisha leseni 13,279; kufanya kaguzi 12 kwa kuzingatia vihatarishi; kutekeleza operesheni nne (4) za kudhibiti michezo haramu; kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 29.89; kuendelea kuelimisha jamii kuhusu athari hasi za michezo ya kubahatisha; na kuwezesha uendeshaji wa Bahati Nasibu ya Taifa.

## 7.4 Mapendekezo ya Bajeti ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Fungu 045 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2025/26

### 7.4.1 Mapato

**109. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, Wizara ya Fedha imekadiriwa kutafuta na kukusanya jumla ya **shilingi trilioni 50.17**. Kati ya kiasi hicho, Mamlaka ya Mapato Tanzania inatarajiwa kukusanya jumla ya **shilingi trilioni 34.10**, misaada shilingi **trilioni 1.07**, mikopo nafuu na ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje **shilingi trilioni 14.95** na maduhuli **shilingi bilioni 53.54**. Aidha, Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi linakadiriwa kukusanya **shilingi milioni 843**, ikiwa ni ukodishaji wa kumbi za mikutano na kodi ya pango kutokana na upangishaji wa majengo ya ofisi yaliyopo katika mikoa mbalimbali nchini.

### 7.4.2 Matumizi

**110. *Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26, mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha yanaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **shilingi trilioni 20.19** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi trilioni 19.43** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara **shilingi trilioni 1.10**, matumizi mengineyo **shilingi trilioni 18.33** na matumizi ya maendeleo **shilingi bilioni 757.79**. Aidha, ninaomba Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 122.52** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi bilioni 110.42** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi bilioni 12.10** matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa matumizi kwa mafungu nane (8) ya kibajeti ya Wizara ya Fedha na Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi umeoneshwa katika **Jedwali Na.1** na mchanganuo wa kina katika **Kiambatisho Na.4.**

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Mafungu ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2025/26**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | MATUMIZI YA MAENDELEO | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|
| **1** | Deni la Serikali | 14,219,350,702,000 | - | 14,219,350,702,000 |
| **6** | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 13,796,941,000 | 1,278,397,000 | 15,075,338,000 |
| **10** | Tume ya Pamoja ya Fedha | 5,110,029,000 | 958,949,000 | 6,068,978,000 |
| **13** | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | 5,162,443,000 | - | 5,162,443,000 |
| **21** | Hazina | 1,768,842,640,000 | 695,432,037,000 | 2,464,274,677,000 |
| **22** | Huduma za Mfuko Mkuu | 3,147,920,108,000 | - | 3,147,920,108,000 |
| **23** | Mhasibu Mkuu wa Serikali | 99,034,314,000 | 6,831,462,000 | 105,865,776,000 |
| **50** | Wizara ya Fedha | 169,583,414,000 | 53,287,560,000 | 222,870,974,000 |
| **JUMLA YA MAFUNGU YA WIZARA** | | **19,428,800,591,000** | **757,788,405,000** | **20,186,588,996,000** |
| **45** | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 110,415,123,000 | 12,103,996,000 | 122,519,119,000 |
| **JUMLA ZA MAFUNGU YOTE** | | **19,539,215,714,000** | **769,892,401,000** | **20,309,108,115,00** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha***

## 8.0 HITIMISHO

**111. *Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru mke wangu mpendwa Bi. Neema pamoja na watoto wetu kwa upendo, uvumilivu, maombi na faraja wanayonipa katika kutekeleza jukumu la usimamizi wa fedha za umma na uchumi jumla wa nchi yetu; jukumu nililopewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nawashukuru sana kwa moyo wa upendo na uvulimivu.

**112. *Mheshimiwa Spika,*** kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb,), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano anaoendelea kunipatia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wizara. Aidha, nawashukuru watendaji wakuu wa wizara na taasisi zake wakiongozwa na Dkt. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bi. Jenifa C. Omolo na Bw. Elijah G. Mwandumbya kwa ushauri na usimamizi makini wa majukumu ya wizara na taasisi. Vilevile, nawashukuru wakuu wa idara, vitengo na wafanyakazi wote wa wizara na taasisi zake, kwa ushirikiano na utekelezaji thabiti wa majukumu yao ya kila

siku. Kwa moyo wa dhati kabisa, napenda pia kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na timu yake kwa kazi nzuri ya kubainisha maeneo yenye upungufu, kupitia taarifa zake na kushauri hatua za kuchukua ili kuboresha usimamizi wa fedha na mali za umma.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Washirika wa Maendeleo kwa michango yao ya hali na mali katika kufanikisha mipango ya wizara na taifa kwa ujumla. Ushiriki wao katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya wizara umejitokeza bayana katika kufikia shabaha ya misaada na mikopo, ujuzi kupitia misaada ya kitaalamu, maboresho ya mifumo ya kisera, kisheria na kitaasisi, uhamasishaji wa shughuli za maendeleo, fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo.

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuwasilisha hoja hii ndani ya Bunge lako Tukufu, waheshimiwa wabunge na umma wa watanzania kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya wizara ambayo ni www.mof.go.tz.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

***Kiambatisho Na.1.***

**Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Mishahara hadi Aprili 2025**

| Fungu | Jina la Fungu | Iliyoidhinishwa | Iliyohuishwa | Iliyotolewa | Iliyotumika | Ufanisi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 1,894,788,000.00 | 1,894,788,000.00 | 1,671,563,000.00 | 1,664,751,700.00 | 99.6% |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 833,157,000.00 | 833,157,000.00 | 605,495,020.00 | 605,495,020.00 | 100.0% |
| | Hazina - Idara na Vitengo | 6,681,481,000.00 | 7,856,481,000.00 | 6,256,550,708.28 | 6,249,463,063.39 | 99.9% |
| 21 | Hazina - Taasisi | 533,710,383,000.00 | 536,461,839,000.00 | 357,710,215,788.62 | 357,710,215,788.62 | 100.0% |
| | Marekebisho ya Mishahara - Serikali | 307,186,724,000.00 | 117,213,906,199.73 | 0 | 0 | 0.0% |
| 22 | Huduma za Mfuko Mkuu | 15,119,603,000 | 15,119,603,000 | 9,474,467,360.20 | 9,474,467,360.20 | 100.0% |
| 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | 7,083,142,000 | 7,083,142,000 | 5,768,386,556 | 5,768,122,796 | 100.0% |
| 50 | Wizara ya Fedha - Idara na vitengo | 8,398,004,000.00 | 8,398,004,000.00 | 7,261,592,310.65 | 7,231,268,495.09 | 99.6% |
| | Wizara ya Fedha - Taasisi | 65,543,616,000.00 | 65,543,616,000.00 | 54,990,326,556.20 | 54,930,002,432.84 | 99.9% |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA** | | **946,450,898,000.00** | **760,404,536,199.73** | **443,738,597,299.95** | **443,633,786,656.14** | **100.0%** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 20,638,564,000.00 | 20,638,564,000.00 | 16,490,345,790.00 | 16,490,345,790.00 | 100.0% |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE** | | **967,089,462,000.00** | **781,043,100,199.73** | **460,228,943,089.95** | **460,124,132,446.14** | 100.0% |

***Chanzo: Wizara ya Fedha***

***Kiambatisho Na. 2.***

**Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi Mengineyo hadi Aprili 2025**

| Fungu | Jina la Fungu | Iliyoidhinishwa | Iliyohuishwa | Iliyotolewa | Iliyotumika | Ufanisi |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Deni la Serikali | 13,131,838,005,000 | 12,020,058,686,000 | 10,215,463,855,000 | 10,198,733,292,000 | 99.8% |
| 6 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 11,151,638,000.00 | 12,013,859,500.00 | 7,240,849,060.89 | 6,829,533,461.92 | 94.3% |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 3,575,157,000.00 | 3,575,157,000.00 | 3,016,374,775.00 | 2,244,099,340.63 | 74.4% |
| 13 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | 3,768,237,000.00 | 5,272,987,000.00 | 3,464,921,721.08 | 3,464,921,721.08 | 100.0% |
| 21 | Idara na Vitengo - Hazina | 54,704,718,500.00 | 54,704,718,500.00 | 49,925,323,300.92 | 49,473,632,472.58 | 99.1% |
| | Hazina - Taasisi | 294,821,633,350.00 | 294,821,633,350.00 | 246,170,161,410.35 | 246,170,161,410.35 | 100.0% |
| | Matumizi Maalumu - Serikali | 238,322,581,150.00 | 434,902,931,220.48 | 369,397,537,176.30 | 369,151,213,958.17 | 99.9% |
| 22 | Huduma za Mfuko Mkuu | 2,614,813,247,000 | 2,144,497,920,921.66 | 1,768,929,444,198.95 | 1,549,673,048,323.04 | 87.6% |
| 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 55,279,317,000 | 89,554,392,012 | 71,121,800,024 | 65,922,626,454 | 92.7% |
| 50 | Wizara ya Fedha - Idara na Vitengo - | 44,213,086,000.00 | 56,083,754,538.16 | 42,448,273,299.04 | 42,384,507,282.00 | 99.8% |
| | Wizara ya Fedha - Taasisi | 30,966,745,000.00 | 34,904,714,000.00 | 26,422,961,524.01 | 26,422,961,524.01 | 100.0% |
| | Madai ya Fidia | 500,000,000.00 | 1,270,000,000.00 | 621,711,477.62 | 397,153,877.62 | 63.9% |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA** | | **16,483,954,365,000.00** | **15,151,660,754,042.30** | **12,804,223,212,968.20** | **12,560,867,151,825.40** | **98.1%** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 80,622,268,000.00 | 80,622,268,000.00 | 77,371,037,333.00 | 70,652,515,000.00 | 91.3% |
| **JUMLA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI** | | **80,622,268,000.00** | **80,622,268,000.00** | **77,371,037,333.00** | **70,652,515,000.00** | **91.3%** |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE** | | **16,564,576,633,000.00** | **15,232,283,022,042.30** | **12,881,594,250,301.20** | **12,631,519,666,825.40** | 98.1% |

***Chanzo: Wizara ya Fedha***

***Kiambatisho Na.3.***

**Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo hadi Aprili 2025**

| Fungu | Jina la Fungu | Chanzo | Iliyoidhinishwa | Iliyohuishwa | Iliyotolewa | Iliyotumika | Ufanisi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | Ndani | 236,611,000.00 | 236,611,000.00 | 236,600,000.00 | 213,780,104.00 | 90.36 |
| | | Nje | 992,840,000.00 | 992,840,000.00 | 992,840,000.00 | 877,870,833.00 | 88.42 |
| 10 | Tume ya Pamoja ya Fedha | Ndani | 1,598,249,000.00 | 1,598,249,000.00 | 500,000,000.00 | 0 | 0.00 |
| | | Nje | 0 | 0 | 0 | 0 | 0.00 |
| 21 | Hazina | Ndani | 440,902,331,000.00 | 551,821,410,252.11 | 407,004,873,053.10 | 403,840,725,019.70 | 99.22 |
| | | Nje | 54,160,669,000.00 | 28,319,021,973.99 | 4,413,558,380.00 | 4,373,518,380.00 | 99.09 |
| 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | Ndani | 1,235,635,000 | 1,235,635,000 | 355,427,000 | 352,397,000 | 99.15 |
| 50 | Wizara ya Fedha | Ndani | 18,244,253,000.00 | 18,949,484,260.10 | 12,683,029,585.58 | 12,682,769,585.77 | 100.00 |
| | | Nje | 20,620,499,000.00 | 16,873,758,529.20 | 14,443,072,075.00 | 14,442,379,701.00 | 100.00 |
| **Jumla - Maendeleo Ndani** | | | **482,837,578,000.00** | **590,715,148,041.41** | **435,223,001,713.68** | **431,532,051,410.47** | **99.15** |
| **Jumla - Maendeleo Nje** | | | **81,830,758,000.00** | **52,242,370,503.19** | **25,660,682,455.00** | **25,269,526,983.00** | **98.48** |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA** | | | **564,668,336,000.00** | **642,957,518,544.60** | **460,883,684,168.68** | **456,801,578,393.47** | **99.11** |
| 45 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | Ndani | 8,828,000,000.00 | 8,828,000,000.00 | 2,577,776,524.00 | 2,142,176,525.00 | 83.10 |
| | | Nje | 2,640,000,000.00 | 2,640,000,000.00 | 2,640,000,000.00 | 2,640,000,000.00 | 100.00 |
| **JUMLA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI** | | | **11,468,000,000** | **11,468,000,000** | **5,217,776,524** | **4,782,176,525** | **91.65** |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE** | | | **576,136,336,000.00** | **654,425,518,544.60** | **466,101,460,692.68** | **461,583,754,918.47** | **99.03** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha***

***Kiambatisho Na.4.***

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2025/26**

| FUNGU | JINA LA FUNGU | MATUMIZI YA KAWAIDA | | | MATUMIZI YA MAENDELEO | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | JUMLA | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | JUMLA | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 = 3+4 | 6 | 7 | 8 = 6+7 | 9=5+8 |
| 001 | Deni la Serikali | - | 14,219,350,702,000 | 14,219,350,702,000 | - | - | - | 14,219,350,702,000 |
| 006 | Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali | 2,366,512,000 | 11,430,429,000 | 13,796,941,000 | 141,967,000 | 1,136,430,000 | 1,278,397,000 | 15,075,338,000 |
| 010 | Tume ya Pamoja ya Fedha | 945,493,000 | 4,164,536,000 | 5,110,029,000 | 958,949,000 | | 958,949,000 | 6,068,978,000 |
| 013 | Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu | - | 5,162,443,000 | 5,162,443,000 | - | - | - | 5,162,443,000 |
| 021 | Hazina | 985,183,709,000 | 783,658,931,000 | 1,768,842,640,000 | 588,911,977,000 | 106,520,060,000 | 695,432,037,000 | 2,464,274,677,000 |
| 022 | Huduma za Mfuko Mkuu | 16,616,460,000 | 3,131,303,648,000 | 3,147,920,108,000 | - | - | - | 3,147,920,108,000 |
| 023 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | 7,468,014,000 | 91,566,300,000 | 99,034,314,000 | 741,381,000 | 6,090,081,000 | 6,831,462,000 | 105,865,776,000 |
| 050 | Wizara ya Fedha | 89,011,587,000 | 80,571,827,000 | 169,583,414,000 | 10,946,552,000 | 42,341,008,000 | 53,287,560,000 | 222,870,974,000 |
| **JUMLA MAFUNGU YA WIZARA** | | **1,101,591,775,000** | **18,327,208,816,000** | **19,428,800,591,000** | **601,700,826,000** | **156,087,579,000** | **757,788,405,000** | **20,186,588,996,000** |
| 045 | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi | 23,058,129,000 | 87,356,994,000 | 110,415,123,000 | 8,828,000,000 | 3,275,996,000 | 12,103,996,000 | 122,519,119,000 |
| **JUMLA MAFUNGU YOTE** | | **1,124,649,904,000** | **18,414,565,810,000** | **19,539,215,714,000** | **610,528,826,000** | **159,363,575,000** | **769,892,401,000** | **20,309,108,115,000** |

***Chanzo: Wizara ya Fedha***

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

Kabla hatujaendelea wapo wageni ambao wapo hapa ndani niwatangaze kwanza kisha tutamleta Mwenyekiti aje asome Taarifa yake, lakini pia ili kumbukumbu za Mheshimiwa Waziri zikae sawa huwa sipongezi kila timu inayoshinda nyingine, huwa napongeza timu iliyopiga hatua fulani kama ni hapa nchini au nje ya nchi na ndiyo maana hamjawahi kunisikia hapa nikiipongeza *Mbeya City* kwa kuifunga *Stand United*. Kwa hiyo, sipongezi kwa magoli napongeza kwa hatua kwa sababu Bunge hili ni Bunge la wananchi siyo Bunge kwa ajili ya ushabiki wa mpira. *(Makofi)*

Kiti cha Spika lazima kiwe na sura hiyo siyo sura ya kuegamia upande wowote wat imu kama ambavyo timu yoyote ambayo itashinda ligi kuu itapongezwa hapa ndani na Kiti cha Spika kwa hiyo sujajua itakuwa ni timu gani sijajua ama timu pia itakayoshinda kombe lingine itapongezwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri uwe na amani kabisa hatupongezi kwa magoli. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika kwanza ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mwingulu Lameck Nchemba Madelu - Waziri wa Fedha, tutaanza na Dkt. Natu Mwamba - Katibu Mkuu, yupo Ndugu Jenifa Omolo - Naibu Katibu Mkuu, Huduma za Hazina, Ndugu Elijah Mwandumbya - Naibu Katibu Mkuu, Usimamizi wa Uchumi, Ndugu CPA Leonald Mkude - Mhasibu Mkuu wa Serikali, Ndugu CPA Benjamin Magai - Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Ndugu Wendy Massoy - Naibu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ofisi ya CAG, Ndugu Yusuph J. Mwenda - Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Amina Msengwa - Mtakwimu Mkuu wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS),* Ndugu Ernest Mchanga - Katibu wa Tume ya Pamoja ya Fedha *(JFC),* karibuni sana. *(makofi)*

Pia yupo Ndugu Majaba S. Magana - Kamishna, Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu *(FIU)*, Dkt. Baghayo Saqware - Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania *(TIRA)*, Ndugu Khadija Said - Naibu Kamishna wa Bima Tanzania *(TIRA)*, Ndugu Kaimu Abdi Mkeyenge - Mtendaji Mkuu wa Shirika la Bima Tanzania *(NIC)*, Ndugu Leonada Mwagike - Mwenyekiti wa Bodi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)*, Ndugu Dennis Simba - Mkurugenzi Mkuu Bodi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma *(PPRA)*, Ndugu James Sando - Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma *(PPAA)*, Profesa Geraldine Rasheli - Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ununuzi na Ugavi Serikalini *(GPSA)*, na Profesa William Pallangyo - Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)*.

Wengine ni Profesa Josephat Lotto - Mkuu wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)*, Profesa Hozen Mayaya - Mkuu wa Chuo cha Mipango, CPA. Kulwa Malendeja - Mtendaji Mkuu wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA)*, Dkt. Tumaini Katunzi - Mkuu wa Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika *(EASTC)*, Ndugu James Mbalwe - Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Ndugu Bahati Ndeserua - Katibu wa Bodi ya Rufani za Kodi *(TRAB)*, Ndugu Mohamed Magati - Katibu wa Baraza la Rufani za Kodi *(TRAT)*, Ndugu Godfrey Malekano - Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa Tanzania *(TMX)*, Ndugu Frank Nyabundege - Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)*, Ndugu Lilian Mbassy - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo Tanzania *(TIB)*, Ndugu Adam Mihayo - Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Biashara Tanzania *(TCB)*, Ndugu Erastus Mtui - Msuluhishi wa Malalamiko na Taarifa za Kodi *(TOST)*, Ndugu David Kafulila - Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi *(PPPC)*, Ndugu Santieli Yona - Mkurugenzi Mkuu Shirika la *Self Microfinance Fund,* ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri wageni wengine sijapata karatasi yao hapa, lakini nawaona na wenyewe wapo hapa ndani karibuni sana wageni wote, basi tunaendelea na ratiba yetu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naona anakuja Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti Mheshimiwa Twaha Mpembenwe. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, utangulizi; kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya Nane cha Kanuni za Kudumu za Bunge kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kuisimamia Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zilizopo chini yake. Aidha, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaipa Kamati jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Hivyo, Kamati ilichambua na kujadili utekelezaji wa bajeti wa mafungu nane ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Mafungu hayo ni kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu sita kama inavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025; katika mwaka wa fedha 2024/2025 mafungu nane ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi trilioni 16.55. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025 jumla ya shilingi trilioni 13.71 zilipokelewa sawa na 86.5% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 10.22 ni kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali,

shilingi bilioni 443.74 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 2.59 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha kwa upande wa fedha za maendeleo shilingi bilioni 460.88 zilitolewa, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 435.22 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 25.66 ni fedha za nje. Jedwali namba moja lililopo kwenye Taarifa ya Kamati linaonesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti za mafungu yote nane yaliyo chini ya Wizara ya Fedha hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mafungu nane; Kamati ilifanya uchambuzi wa mafungu yote nane na kubaini masuala yafuatayo:-

Kwanza, Fungu 01 – Deni la Serikali; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu hili liliidhinishiwa shilingi trilioni 12.020 kwa ajili ya kulipa Deni la Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 1.74 kwa ajili ya kulipa riba ya deni la nje, shilingi trilioni 3.145 kwa ajili ya kulipa riba deni la ndani, shilingi trilioni 4.21 ni kwa ajili ya kulipa deni la ndani lililoiva, shilingi trilioni 2.90 ni kwa ajili ya kulipa deni la nje lililoiva. Aidha, kiasi cha shilingi bilioni 18.33 ni kwa ajili ya kuhudumia deni na shilingi milioni 170 ni kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2025, Fungu hili lilipokea shilingi trilioni 10.22 sawa na 84.99% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho shilingi trilioni 2.57 zimetumika kulipa deni la nje, shilingi trilioni 3.53 zimetumika kulipa deni la ndani, shilingi trilioni 2.48 kulipa riba ya deni la ndani, shilingi trilioni 1.63 kulipa riba ya deni la nje, shilingi bilioni 12.68 zimetumika kuhudumia deni na shilingi milioni 159.25 zimetumika kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mwenendo huo wa ulipaji wa madeni unaashiria kwamba Serikali ina uwezo wa kulipa mikopo yake ya ndani na nje kwa wakati, hii ndiyo Serikali inayoongwana na mchumi namba moja mwenye uwezo wa kuiendesha Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu 006 liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 15.14 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.89 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 12.01 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi milioni 236.61 ni fedha za ndani za maendeleo na shilingi milioni 992.84 ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2025, jumla ya shilingi bilioni 10.14 zimetolewa sawa na 66.99% ya bajeti iliyoidhinishwa kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 1.67 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 7.24 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1.23 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fungu hili linahusika na usimamizi thabiti wa fedha za umma kwa maendeleo jumuishi na endelevu ya kiuchumi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za maendeleo kwa 99.99% yenye lengo la kuboresha usimamizi wa fedha za umma. Aidha, Idara hii husaidia kutekeleza mapendekezo ambayo huwa yanatolewa na CAG. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa wakaguzi wa ndani kwa kuwajengea uwezo wakaguzi 1,155 katika maeneo ya ukaguzi na utumiaji wa mifumo katika mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kufanya ununuzi wa tarakalishi mpakato 75 ambazo zimesambazwa kwa wakaguzi wa ndani katika Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba bado kuna changamoto ya uhaba wa vitendea kazi pamoja na watumishi, hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele cha upatikanaji wa vitendea kazi kwa Fungu hili pamoja na watumishi. Aidha, mifumo ya Serikali yote inapokuwa inajengwa iwe ni lazima inahusisha fungu hili ili kurahisisha zoezi la ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Tume ya Pamoja ya Fedha iliidhinishiwa na Bunge jumla ya shilingi bilioni 6.01 kati ya fedha hizo, shilingi milioni 833.16 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 3.58 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1.59 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya shilingi bilioni 4.12 sawa na

68.62% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotolewa, shilingi milioni 605.495 ni mishahara, shilingi bilioni 3.02 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi 500,000,000 ni fedha za matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Tume inakabiliwa na changamoto kuu mbili; moja ni ukosefu wa Makamishna wa Tume ambao ndio wana jukumu la kusimamia kazi za Tume; na pili ni ukosefu wa jengo la Ofisi kwa Tanzania Bara, hali inayosababisha kutenga zaidi ya shilingi milioni 100 kwa mwaka kwa ajili ya kulipa kodi ya pango. Pamoja na kwamba jengo limepatikana, lakini linahitaji marekebisho makubwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupata Makamishna wa Tume na kuharakisha utolewaji wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa ukarabati wa jengo lililopatikana katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu yaani *FIU;* katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 13 liliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 5.27 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Aprili, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 3.46 sawa na 65.71%. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuratibu utekelezaji wa Mpango kazi wa Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu *(FATF)* ili kuiondoa Tanzania katika orodha ya nchi zilizo katika usimamizi wa karibu wa *Grey List*. Tanzania imeweza kutekeleza vipengele vyote 21 vya mpango kazi huo na hivyo kuondolewa kwenye uangalizi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha mfumo maalum wa kuratibu takwimu za matukio yanayohusiana na utakatishaji fedha haramu kuanzia miamala shuku, makosa tangulizi, makosa ya utakatishaji, utaifishaji wa nyenzo zinazotumika kufanya uhalifu na mali zilizopatikana kwa njia haramu. Lengo ni kuboresha utendaji kazi na kupunguza miamala fiche. Hatua hii inaonesha utayari wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kusikiliza ushauri wa Bunge na kuutekeleza, huyu ndiye Mheshimiwa Rais ambaye Watanzania tunayemuhitaji mwenye

kuheshimu Muhimuli wa Bunge na kuweza kuchukua ushauri kwa maslahi mapana ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Fungu 21 – Hazina; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 21 lilidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.03 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 661.53 ni kwa ajili ya mishahara ikijumuisha bajeti ya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma na shilingi bilioni 784.43 ni matumizi mengineyo na shilingi bilioni 580.14 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2025 fungu hili limepokea jumla ya shilingi trilioni 1.44 sawa na 71.12% kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 363.97 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 665.49 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi 411.42 ni fedha za maendeleo Kamati inaishauri Serikali kupitia fungu hili kuharakisha mchakato wa kuhakiki na kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ili kuondoa madhira wanayokumbana nayo.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 22 – Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu hili liliidhinishiwa kiasi cha shilingi trilioni 2.16 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.12 ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kwa Fungu Namba 022, na shilingi trilioni 2.14 ni kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya shilingi trilioni 1.78 zimepokelewa sawa na 82.35% ya bajeti. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 9.47 ni mishahara na shilingi trilioni 1.77 ni matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine fungu hili linahusika na kulipa mafao ya pensheni kwa wastaafu wa Serikali wanaolipwa kupitia Hazina. Kamati inaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuanza mchakato wa kuhuisha viwango vya mafao kwa wastaafu, pamoja na kujenga mfumo wa wastaafu wa kujihakiki wenyewe ambao unategemewa kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2025.

Mheshimiwa Spika, mfumo huo utasaidia wastaafu kutosafiri umbali mrefu kwa ajili ya kufuatilia mafao yao. Vilevile Serikali inatengeneza mfumo wa kielektroniki wa malipo ya wastaafu

*(Treasury Pensioners Payment System-TPPS)* unaotumika kuandaa, kulipa na kutunza nyaraka na taarifa za wastaafu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuunganisha mfumo huo na mifumo mingine ya *MUSE*, mfumo wa kutengeneza vyeti vya kifo *(Civil Registration System)* pamoja na mifumo ya malipo kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ili kurahisisha utambuzi na ulipaji wa mafao na kuhakikisha wastaafu wanapatiwa huduma kwa haraka na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 103.93. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.08 ni kwa ajili ya mishahara kwa watumishi wa Idara, shilingi bilioni 89. 55 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 7.29 ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 jumla ya shilingi bilioni 83.26 zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na 79.92%. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5.77 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 71.12 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 6.17 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa mafunzo kwa wahasibu waliopo chini ya Fungu hili ili kuwajengea uwezo na kuhakikisha wanaendana na mabadiliko ya viwango vya Kimataifa na teknolojia. Aidha, ni vyema wahasibu wa Serikali wawe na programu ya kuwashikiza katika taasisi binafsi zinazofanya vizuri ndani na nje ya nchi ili kuwapatia uzoefu.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026; makadirio ya matumizi kwa mafungu nane ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara pamoja na mafungu yaliyo chini yake inaomba idhinishiwe jumla ya shilingi trilioni 20.19 sawa na ongezeko la 22.05% kutoka bajeti ya shilingi 16.54 ya mwaka 2024/2025. Kati ya kiasi kinachoombwa, shilingi 14.22 ni kwa ajili ya ulipaji wa deni, shilingi triliomi 4.11 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi trilioni 1.10 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 757. 79 kwa ajili

ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 601.70 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 156.09 ni fedha za nje. Jedwali Namba 2 lililopo kwenye taarifa ya kamati linaonesha mchanganuo wa maombi ya fedha kwa Wizara ya Fedha na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa baadhi ya mafungu; baada ya uchambuzi wa mafungu yote nane, Kamati imebaini na kupendekeza masuala yafuatayo: -

(a) Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali; ili kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa ndani na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika ipasavyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa katika mwaka 2025/2026 Idara hii inakamililisha ujenzi wa mifumo mitatu ambayo ipo chini yake na kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inasomana yenyewe kwa yenyewe. Mifumo hiyo ni: -

(i) Mfumo unaotumika katika kupanga, kufanya ukaguzi na kutoa taarifa kwa wakati *(Government Internal Audit Management Information System);*

(ii) Mfumo unaotumika kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ndani, *CAG, PPRA* pamoja na maelekezo ya Kamati mbalimbali za Bunge *(Government Audit Recommendation and Implementation Information Tracking System);* na

(iii) Mfumo unaosaidia kutambua, kufanya tathmini ya vihatarishi na kupendekeza mikakati ya kudhibiti athari ya vihatarishi hivyo *(Government Enterprise Risk Management Information System)*.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati iliitaka Serikali kuhakikisha kuwa Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi katika taasisi hawatoki tena kwenye taasisi husika za umma na badala yake nafasi hizo zipatikane kwa kuomba ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi, ushindani na uwajibikaji.

(b) Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; kazi kubwa ya fungu hili ni kusaidia kulinda nchi dhidi ya utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi na uhalifu mwingine wa kifedha. Mathalani, katika kipindi cha mwezi Julai, 2024 hadi mwezi Februari, 2025 kitengo hiki kilipokea miamala shuku 1,300,000 yenye thamani ya shilingi trilioni 463. Kamati ilichambua makadirio ya matumizi ya Fungu hili kwa mwaka 2025/2026 na kubaini kwamba bajeti hiyo haitoshelezi ikilinganishwa na majukumu. Awali bajeti ya Fungu hili ilikuwa ni shilingi bilioni 4.16 na hivyo Kamati iliielekeza Wizara kuongeza kiasi cha shilingi 1,000,000,000 ili kuanza mchakato wa kuimarisha Kitengo. Serikali ilikubaliana na Kamati na kuongeza bajeti ya fungu hili kutoka shilingi bilioni 4.6 hadi shilingi bilioni 5.16.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo kazi ya Kamati yako ya Bajeti inayoifanya katika kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Kitengo hiki kinakuwa Mamlaka kamili ili kuongeza mawanda ya kazi na kujitegemea zaidi kama ilivyo kwa nchi nyingine mfano nchi ya Zambia. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa kitengo hiki kinakuwa na wafanyakazi wa kudumu na kuwalipa mishahara kupitia fungu hili na kuachana na utaratibu wa kuazima watumishi kutoka taasisi mbalimbali za umma ambazo mishahara yao hutofautiana wakati wanatekeleza majukumu yanayofanana.

(c) Fungu 021– Hazina; Serikali imekuwa ikiwasilisha mapendekezo ya miradi inayotakiwa kutekelezwa kwa Mfumo wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)*. Hata hivyo, bado Serikali haijafanikiwa kutumia mfumo huu wa utekelezaji wa miradi. Hivyo, Kamati iliitaka Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka 2025/2026 miradi inayotumia mfumo wa *PPP* inaanza kutekelezwa ili kupunguza mzigo wa mahitaji ya fedha za maendeleo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025

pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya fungu hili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu kama yanavoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa utolewaji wa fedha kwa Fungu 45 kwa mwaka wa fedha 2024/2025; Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 113.58. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 20.64 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 80.62 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 11.47 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, fungu hili lilipangiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi 850,000,000. Hadi mwezi Aprili, 2025 fungu lilipokea jumla ya shilingi bilioni 99.08 sawa na 87.89% ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhakikisha fungu hili lilipata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwezesha ofisi hii kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya udhibiti na ukaguzi. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Namba 3 katika Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya msingi yanayobainika katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka 2024/2025; katika mwaka 2024/2025 ofisi imefanikiwa kufanya yafuatayo: -

(i) Kufanya kaguzi 1,485;

(ii) Kukamilishaji Ripoti Kuu sita;

(iii) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi katika Mikoa ya Songwe na Katavi;

(iv) Kuwajengea uwezo Wajumbe 84 wa Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa Fedha (*LAAC, PAC, PIC* na *PBC*); na

(v) Kuanza hatua za awali za ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa ya Mwanza na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Changamoto za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka 2024/2025; Kamati imebaini kwamba fungu hili linakabiliwa na uhaba wa rasilimali fedha ili kutekeleza masuala yafuatayo: -

(i) Kuwajengea uwezo wakaguzi wote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa;

(ii) Kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi ikiwemo ukaguzi wa wakati halisi *(real time audit),* ukaguzi wa kiufundi na ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi; na

(iii) Ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo kompyuta mpakato na vifaa vya kuwezesha ukaguzi wa kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza fedha kwa Fungu 45 ili ofisi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imetengewa jumla ya shilingi bilioni 123.36. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.06 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi bilioni 87.37 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, shilingi bilioni 8.83 ni fedha za ndani za maendeleo na shilingi bilioni 3.78 ni fedha za nje. Aidha, fungu limeidhinishiwa kukusanya Maduhuli yenye thamani ya shilingi 843

kwa ajili ya kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Jedwali Namba 4 lililopo kwenye taarifa ya Kamati linaonesha ulinganisho wa Bajeti ya *NAOT* kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo: -

(i) Kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa Sura ya 437 ili mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki *(Cashlite)* uanze kutumika

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kutumia mifumo ya kielektroniki katika kufanya malipo ili kuzuia upotevu wa mapato yatokanayo na kodi. Malipo ya kielektroniki ni miamala inayofanyika kupitia kadi za malipo, simu za mkononi na malipo ya papo kwa papo. Lengo ni kurahisisha miamala na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu. Kamati inaisisitiza Serikali kufanya mabadiliko katika kifungu cha 8 cha Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa Sura ya 437 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ili kuanzisha sharti la lazima la kufanya malipo kwa njia ya kieletroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa.

(ii) Serikali kupitia upya Muundo wa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Ndani ya Umma

Mheshimiwa Spika, Idara ya Mkaguzi wa Ndani wa Serikali ipo chini ya Wizara ya Fedha ambapo Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali anawajibika kiutendaji na kiutawala kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha. Aidha, Mkaguzi wa Ndani katika taasisi za umma anawajibika kiutawala na kiutendaji kwa Mkuu wa Taasisi husika. Hata hivyo, muundo huu unaonekana kuwa na

changamoto kutokana na sheria kutompa mamlaka Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kuwawajibisha wakaguzi wa ndani pindi wanapobainika kutenda makosa. Aidha, muundo huu haumpi Mkaguzi wa ndani uhuru katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuripoti kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye kimsingi ni mkaguliwa. Muundo huu umekuwa ukisababisha hoja za Mkaguzi Mkuu wa Ndani kutofanyiwa kazi kwa wakati na baadae kujitokeza katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kufanya mabadiliko ya muundo wa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Ndani wa Umma ili Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali awe anawajibika kiutawala kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kiutendaji kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia Kamati ya Ukaguzi ya Kitaifa *(The National Audit Committee)*. Vilevile Kamati inataka Sheria iweke wazi uwajibikaji na uhuru wa Mkaguzi wa ndani wa taasisi za umma kwa kumtaka Mkaguzi wa Ndani kuwajibika Kiutawala kwa Maafisa Masuuli na kiutendaji kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali.

(iii) Kuwezesha kimitaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* na Benki ya Uwekezaji *(TIB)*

Mheshimiwa Spika, jukumu kuu la Benki ya *TADB* ni kuwa chachu ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa ajili ya kufanikisha maendeleo jumuishi ya sekta ya kilimo nchini, na kuchangia katika Dira ya Taifa ya Maendeleo katika kuhakikisha utoshelevu na usalama wa chakula, maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini. Kwa sasa benki hii ina mtaji wa jumla ya shilingi bilioni 924. Hata hivyo, benki hii haipokei amana kama ilivyo kwa benki za biashara. Ili kutimiza kikamilifu dhamira ya *TADB* na kukidhi mahitaji yanayoongezeko la fedha kwa ajili ya kilimo, benki hii inahitaji jumla ya shilingi trilioni 2.95 mpaka kufikia mwaka 2035, hivyo kufanya nakisi ya shilingi trilioni 2.026.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, Benki ya *TIB* ina jukumu la kutoa huduma za fedha kwa miradi ya maendeleo kwa gharama nafuu ili kujenga Taifa lenye uchumi shirikishi, mseto, mahiri na wenye ushindani. Hata hivyo, mwenendo wa ufanisi wa benki hiyo sio wa kuridhisha kwa sababu katika kipindi cha miaka mitatu mapato ya benki yamekuwa yakishuka kutoka shilingi bilioni 62.7 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 35.6 mwaka 2024 kufuatia kushuka kwa kasi ya utoaji wa mikopo kutokana na kiwango hafifu cha mtaji. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2024, mtaji wa benki kwa mujibu wa kanuni za taasisi za fedha *(core capital)* ulikuwa shilingi bilioni 90.226 kiwango ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiwango cha shilingi bilioni 200 kinachotakiwa kwa mujibu wa kanuni za taasisi za fedha za maendeleo zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2021.

Mheshimiwa Spika, kiwango hicho kidogo cha mtaji kinazuia ukuaji wa mizania ya benki kwa sababu benki haina uwezo wa kukopa na kutumia mtaji kama nyenzo ili kuweza kukopesha miradi mikubwa ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mikakati ya Serikali ya kukuza uwekezaji katika sekta ya kilimo na kuongeza viwanda nchini, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa mitaji katika benki hizo ili kuongeza ufanisi na kuwezesha benki hizo kuwa shindani.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)* pamoja na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge. *(Makofi)*

Nawashukuru pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb), Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati wa kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha

2025/2026. Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Natu El-Maamry Mwamba - Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na wataalam wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao katika kujadili, kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Ndugu Charles Kichere - Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe kama majina yao yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, naomba nimshukuru Mwenyekiti wangu, baba yangu, mlezi wangu, Mheshimiwa Oran Manase Njeza kwa ulezi wake, kwa umakini wake na jinsi anavyoweza kuiongoza Kamati ya Bajeti. Ni imani yangu wananachi wa Mbeya Vijijini wanakwenda kumrudisha baba huyo ili aweze kulitumikia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee zaidi naomba niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Kibiti kwa heshima kubwa waliyokuwa wamenipa katika kipindi cha miaka mitano. Nataka niwahakikishie nguvu nanazo, uwezo ninao, na utashi ninao wa kuweza kuendelea kuwatumikia. Ni imani yangu wataendelea kunipa ridhaa katika kipindi kijacho ili mwezi wa kumi na moja nije kuapa hapa kuwa Mbunge tena kwa awamu ya pili kwa Jimbo la Kibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Ndugu Baraka Leonard - Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya mafungu nane ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Fedha yenye jumla ya shilingi trilioni 20.31; kati ya fedha hizo shilingi trilioni 1.12 ni kwa ajili ya mishahara, shilingi trilioni 18.41 kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 610.53 kwa ajili ya fedha za maendeleo ni fedha za ndani na shilingi bilioni 159.36 ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu wa hali ya juu sana uliopitiliza, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

---

**1.0. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kuwasilisha Taarifa ya Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya Nane cha Kanuni za Kudumu za Bunge kinaipa Kamati ya Bunge ya Bajeti jukumu la kuisimamia Wizara ya Fedha pamoja na Taasisi zilizopo

chini yake. Aidha, Kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaipa Kamati jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Hivyo, Kamati ilichambua na kujadili utekelezaji wa bajeti wa Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 na makadirio ya mapato na matumizi ya Mafungu hayo kwa mwaka wa fedha 2025/26. Mafungu hayo ni kama ifuatavyo:-

i. Fungu 001 – Deni la Serikali
ii. Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali
iii. Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha
iv. Fungu 013 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu
v. Fungu 021 – Hazina
vi. Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu
vii. Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali
viii. Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
ix. Fungu 050 – Wizara ya Fedha

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni: -

i. Utangulizi;
ii. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa fedha 2024/25;
iii. Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa fedha 2025/26;
iv. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa fedha 2024/25 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2025/26;
v. Maoni na Mapendekezo ya Kamati; na
vi. Hitimisho

## 2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Mafungu 8 ya Wizara ya Fedha yaliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 16,555,022,808,786.60.** Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025 jumla ya

**Shilingi 13,708,845,494,436.80** zilipokelewa sawa na **asilimia 86.5** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 10,215,463,855,000** ni kwa ajili ya kugharamia deni la Serikali, **Shilingi 443,738,597,299.95** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 2,588,759,357,968.20** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha kwa upande wa fedha za maendeleo **Shilingi 460,883,684,168.68** zilitolewa, kati ya fedha hizo **Shilingi 435,223,001,713.68** ni fedha za ndani na **Shilingi 25,660,682,455** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali namba 1 linaonesha mwenendo wa utekelezaji wa bajeti za mafungu yote nane (8) yaliyo chini ya Wizara ya Fedha hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2025.

**Jedwali Na.1. Utekelezaji wa Bajeti ya Mafungu 8 ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/25**

| Fungu | Bajeti iliyoidhinishwa 2024/25 | Fedha zilizotolewa hadi Aprili, 2025 | Asilimia ya Bajeti Iliyoidhinishwa |
|---|---|---|---|
| **001. Deni la Serikali** | | | |
| Matumizi mengineyo | **12,020,058,686,000.00** | **10,215,463,855,000.00** | **84.99** |
| **006. Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali** | | | |
| Mishahara | 1,894,788,000.00 | 1,671,563,000.00 | 88.22 |
| Matumizi mengineyo | 12,013,859,500.00 | 7,240,849,060.89 | 60.27 |
| Maendeleo Ndani | 236,611,000.00 | 236,600,000.00 | 99.99 |
| Maendeleo Nje | 992,840,000.00 | 992,840,000.00 | 100 |
| **Jumla Ndogo** | **15,138,098,500.00** | **10,141,852,060.89** | **66.99** |
| **010. Tume ya Pamoja ya Fedha** | | | |
| Mishahara | 833,157,000.00 | 605,495,020.00 | 72.67 |
| Matumizi mengineyo | 3,575,157,000.00 | 3,016,374,775.00 | 84.37 |
| Maendeleo Ndani | 1,598,249,000.00 | 500,000,000.00 | 31.28 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jumla Ndogo** | **6,006,563,000.00** | **4,121,869,795.00** | **68.62** |
| **013. Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu** | | | |
| Matumizi mengineyo | 5,272,987,000.00 | 3,464,921,721.08 | 65.71 |
| **Jumla Ndogo** | **5,272,987,000.00** | **3,464,921,721.08** | **65.71** |
| **021. Hazina** | | | |
| Mishahara | 661,532,226,199.73 | 363,966,766,496.90 | 55.02 |
| Matumizi mengineyo | 784,429,283,070.48 | 665,493,021,887.57 | 84.84 |
| Maendeleo Ndani | 551,821,410,252.11 | 407,004,873,053.10 | 73.76 |
| Maendeleo Nje | 28,319,021,973.99 | 4,413,558,380.00 | 15.59 |
| **Jumla Ndogo** | **2,026,101,941,496.31** | **1,440,878,219,817.57** | 71.12 |
| **022. Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali** | | | |
| Mishahara | 15,119,603,000.00 | 9,474,467,360.20 | 62.66 |
| Matumizi mengineyo | 2,144,497,920,921.66 | 1,768,929,444,198.95 | 82.49 |
| **Jumla Ndogo** | **2,159,617,523,921.66** | **1,778,403,911,559.15** | **82.35** |
| **023. Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali** | | | |
| Mishahara | 7,083,142,000.00 | 5,768,386,556.00 | 81.44 |
| Matumizi mengineyo | 89,554,392,012.00 | 71,121,800,024.00 | 79.42 |
| Maendeleo Ndani | 1,235,635,000.00 | 355,427,000.00 | 28.76 |
| Maendeleo Nje | 6,056,750,000.00 | 5,811,212,000.00 | 95.95 |
| **Jumla ndogo** | **103,929,919,012.00** | **83,056,825,580.00** | **79.92** |
| **050. Wizara ya Fedha** | | | |
| Mishahara | 73,941,620,000.00 | 62,251,918,866.85 | 84.19 |
| Matumizi mengineyo | 93,498,268,538.16 | 70,114,657,778.29 | 74.99 |
| Maendeleo Ndani | 18,949,484,260.10 | 12,683,029,585.58 | 66.93 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Maendeleo Nje | 16,873,758,529.20 | 14,443,072,075.00 | 85.59 |
| **Jumla Ndogo** | **203,263,131,327.46** | **159,492,678,305.72** | 78.45 |
| **Jumla Kuu** | **16,555,022,808,786.60** | **13,708,845,494,436.80** | **86.5** |

***Chanzo:*** *Randama za Mafungu*

**2.1. Uchambuzi wa Mafungu Nane (8)**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa Mafungu yote 8 na kubaini masuala yafuatayo:-

**2.1.1. Fungu 01 – Deni la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Fungu hili liliidhinishiwa **Shilingi 12,020,058,686,000** kwa ajili ya kulipa deni la Serikali. Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 1,737,816,590,000** kwa ajili ya kulipa riba ya Deni la nje, **Shilingi 3,146,667,964,000** kwa ajili ya kulipa riba Deni la ndani, **Shilingi 4,214,961,950,000** ni kwa ajili ya kulipa deni la ndani lililoiva, **Shilingi 2,902,114,261,000** ni kwa ajili ya kulipa deni la nje lililoiva. Aidha, kiasi cha **Shilingi 18,327,921,000** ni kwa ajili ya kuhudumia deni na **Shilingi 170,000,000** ni kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Aprili 2025, Fungu hili lilipokea **Shilingi 10,215,463,855,000** sawa na **asilimia 84.99** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho **Shilingi 2,573,610,645,000** zimetumika kulipa deni la nje, **Shilingi 3,527,418,750,000** zimetumika kulipa deni la ndani, **Shilingi 2,475,712,329,000** kulipa riba ya deni la ndani, **Shilingi 1,625,881,444,000** kulipa riba deni la nje, **Shilingi 12,681,440,000** zimetumika kuhudumia deni na **Shilingi 159,247,000** zimetumika kwa ajili ya matangazo ya minada ya kuuza dhamana za Serikali. Kamati inaipongeza Serikali inayoongozwa na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuwa mwenendo huo wa ulipaji wa madeni unaashiria kwamba Serikali ina uwezo kulipa mikopo yake ya ndani na nje kwa wakati.

**2.1.2. Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Fungu 006 liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 15,138,098,500.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,894,788,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi**

**12,013,859,500** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shillingi 236,611,000** ni fedha za ndani za maendeleo na **shillingi 992,840,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 10,141,852,060.89** zimetolewa sawa na **asilimia 66.99** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,671,563,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 7,240,849,060.89** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 1,229,440,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Fungu hili linahusika na usimamizi thabiti wa fedha za umma kwa maendeleo jumuishi na endelevu ya kiuchumi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za maendeleo kwa **asilimia 99.99** yenye lengo la kuboresha usimamizi wa fedha za umma. Aidha, Idara hii husaidia kutekeleza mapendekezo ambayo huwa yanatolewa na CAG. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa wakaguzi wa ndani kwa kuwajengea uwezo wakaguzi 1,155 katika maeneo ya ukaguzi na utumiaji wa mifumo katika mwaka 2024/25 pamoja na kufanya ununuzi wa tarakalishi mpakato 75 ambazo zimesambazwa kwa wakaguzi wa ndani katika Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba bado kuna changamoto ya uhaba wa vitendea kazi pamoja na watumishi. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele cha upatikanaji wa vitendea kazi kwa Fungu hili pamoja na watumishi. Aidha, mifumo ya Serikali yote inapokuwa inajengwa iwe ni lazima kuhusiha Fungu hili ili kurahisisha zoezi la ukaguzi.

**2.1.3. Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2024/25 Tume ya Pamoja ya Fedha iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 6,006,563,000** kati ya fedha hizo, **Shilingi 833,157,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 3,575,157,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 1,598,249,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi 4,121,869,795** sawa na **asilimia 68.62**

ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotolewa, **Shilingi 605,495,020** ni mishahara, **Shilingi 3,016,374,775** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi 500,000,000** ni fedha za matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Tume inakabiliwa na changamoto kuu mbili. Moja ni ukosefu wa Makamishna wa Tume, ambao ndio wana jukumu la kusimamia kazi za Tume na pili ni ukosefu wa jengo la Ofisi kwa Tanzania Bara, hali inayosababisha kutenga zaidi ya **Shilingi milioni 100** kwa mwaka kwa ajili ya kulipa kodi ya pango. Pamoja na kwamba jengo limepatikana lakini linahitaji marekebisho makubwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha mchakato wa kupata Makamishna wa Tume na kuharakisha utolewaji wa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa ukarabati wa jengo lililopatikana katika mwaka wa fedha 2025/26.

**2.1.4. Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU)**
**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Fungu 13 liliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,272,987,000** kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Aprili 2025, Fungu hili lilipokea jumla ya **Shilingi 3,464,921,721.08** sawa na **asilimia 65.71.**

**Mheshimiwa Spika,** Kitengo hiki kilikuwa kinakabiliwa na changamoto ya Taasisi za Umma kutokukipa ushirikiano kikamilifu. Kamati iliishauri Serikali kutanzua changamoto hiyo. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa Kitengo cha FIU kwa kushirikiana na vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria vikiwemo Jeshi la Polisi, Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na rushwa, Mamlaka za Kuzuia Dawa za Kulevya, Mamlaka za kuzuia ujangili na biashara haramu ya wanayamapori zilizopo Tanzania Bara na Zanzibar zinakutana kila baada ya miezi miwili hadi mitatu kwa lengo la kujadili changamoto, kuimarisha ushirikiano na kuzuia uhalifu kwa kuhakikisha uchunguzi wa makosa tangulizi unafanyika sambamba na kufuatilia mazalia ya uhalifu pamoja na utakasishaji fedha haramu kwa washitakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati inaipongeza Serikali kwa kuratibu utekelezaji wa Mpango kazi wa Kikosi Kazi cha Kimataifa

cha Kudhibiti Utakasishaji wa Fedha Haramu (FATF) ili kuiondoa Tanzania katika orodha ya nchi zilizo katika usimamizi wa karibu wa *Grey List*. Tanzania imeweza kutekeleza vipengele vyote 21 vya mpango kazi huo na hivyo kuondolewa kwenye uangalizi.

Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuboresha mfumo maalumu wa kuratibu takwimu za matukio yanayohusiana na utakasishaji fedha haramu kuanzia miamala shuku, makosa tangulizi, makosa ya utakasishaji, utaifishaji wa nyenzo zinazotumika kufanya uhalifu na mali zilizopatikana kwa njia haramu. Lengo ni kuboresha utendaji kazi na kupunguza miamala fiche. Hatua hii inaonyesha utayari wa ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*** katika kusikiliza ushauri wa Bunge na kuutekeleza.

**2.1.5. Fungu 21 – Hazina**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Fungu 21 liidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,026,101,941,496.31**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 661,532,226,199.73** ni kwa ajili ya mishahara ikijumuisha bajeti ya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wa umma na **Shilingi 784,429,283,070.48** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 580,140,432,226.10** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo**.** Hadi kufikia Aprili, 2025 Fungu hili limepokea jumla ya **Shilingi 1,440,878,219,817.57** sawa na **asilimia 71.12.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 363,966,766,496.90** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 665,493,021,887.57** ni fedha za matumizi mengineyo na **Shilingi 411,418,431,433.10** ni fedha za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kupitia Fungu hili kuharakisha mchakato wa kuhakiki na kulipa madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ili kuondoa madhira wanayokumbana nayo.

**2.1.6. Fungu 22 – Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25 Fungu hili liliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,159,617,523,921.66.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,119,603,000** ni kwa ajili ya mishahara ya maafisa wa umma wanaolipwa kupitia Fungu 022, na **Shilingi 2,144,497,920,921.66** ni kwa ajili ya Huduma za Mfuko Mkuu**.** Hadi

kufikia Aprili 2025, jumla ya **Shilingi 1,778,403,911,559.15** zimepokelewa sawa na **asilimia 82.35** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 9,474,467,360.20** ni mishahara na **Shilingi 1,768,929,444,198.95** ni matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na majukumu mengine Fungu hili linahusika na kulipa mafao na pensheni kwa wastaafu wa Serikali wanaolipwa kupitia Hazina. Kamati inaipongeza Serikali ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuanza mchakato wa kuhuisha viwango vya mafao kwa wastaafu, pamoja na kujenga Mfumo wa Wastaafu wa kujihakiki wenyewe ambao unategemewa kuanza kutumika tarehe 1 Julai, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo huo utasaidia wastaafu kutosafiri umbali mrefu kwa ajili ya kufuatilia mafao yao. Vilevile, Serikali imetengeneza mfumo wa kielektroniki wa Malipo ya Wastaafu *(Treasury Pensioners Payment System*-TPPS) unaotumika kuandaa, kulipa na kutunza nyaraka na taarifa za Wastaafu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuunganisha mfumo huo na mifumo mingine ya MUSE, mfumo wa kutengeneza vyeti vya kifo *(Civil Registration System)* pamoja na mifumo ya malipo kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii ili kuharakisha utambuzi na ulipaji wa mafao na kuhakikisha wastaafu wanapatiwa huduma kwa haraka na kwa wakati.

**2.1.7. Fungu 23: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 103,929,919,012.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 7,083,142,000** ni kwa ajili ya Mishahara kwa watumishi wa Idara, **Shilingi 89,554,392,012** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 7,292,385,000** ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 83,256,825,580** zimetolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo sawa na **asilimia 79.92.** Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 5,768,386,556** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 71,121,800,024** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi 6,166,639,000** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutoa mafunzo kwa wahasibu waliopo chini ya Fungu hili ili kuwajengea uwezo na kuhakikisha wanaendana na mabadiliko ya viwango vya Kimataifa na teknolojia. Aidha, ni vyema wahasibu wa Serikali wawe na programu ya kuwashikiza katika Taasisi binafsi zinazofanya vizuri ndani na nje ya nchi ili kupata uzoefu.

**2.1.8. Fungu 50: Wizara ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/25, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 203,263,131,327.46** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo**.** Kati ya kiasi hicho, **Shilingi 73,941,620,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 93,498,268,538.16** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 35,823,242,789.30** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 159,492,678,305.72** zimetolewa sawa **asilimia 78.45.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 62,251,918,866.85** ni mishahara, **Shilingi 70,114,657,778.29** ni matumizi mengineyo, **Shilingi 12,683,029,585.58** ni fedha za ndani za maendeleo na **Shilingi 14,443,072,075.00** ni fedha za nje.

## 3.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

### 3.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Fedha pamoja na mafungu yaliyo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 20,186,588,996,000** sawa na ongezeko la **asilimia 22.05** kutoka bajeti ya **Shilingi 16,539,877,005,257** mwaka 2024/25. Kati ya kiasi kinachoombwa, **Shilingi 14,219,350,702,000** ni kwa ajili ya ulipaji wa Deni, **Shilingi 4,107,858,114,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 1,101,591,775,000** kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 757,788,405,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 601,700,826,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 156,087,579,000** ni fedha za nje. Jedwali namba 2 linaonyesha mchanganuo wa maombi ya fedha kwa Wizara ya

Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**Jedwali Na. 2: Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2025/26**

| Fungu | Matumizi Mengineyo | Mishahara | Miradi ya Maendeleo (Ndani) | Miradi ya Maendeleo (Nje) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | 14,219,350,702,000 | - | - | - | 14,219,350,702,000 |
| 06 | 11,430,429,000 | 2,366,512,000 | 141,967,000 | 1,136,430,000 | 15,075,338,000 |
| 10 | 4,164,536,000 | 945,493,000 | 958,949,000 | - | 6,068,978,000 |
| 13 | 5,162,443,000 | - | - | - | 5,162,443,000 |
| 21 | 783,658,931,000 | 985,183,709,000 | 588,911,977,000 | 106,520,060,000 | 2,464,274,677,000 |
| 22 | 3,131,303,648,000 | 16,616,460,000 | | | 3,147,920,108,000 |
| 23 | 91,566,300,000 | 7,468,014,000 | 741,381,000 | 6,090,081,000 | 105,865,776,000 |
| 50 | 80,571,827,000 | 89,011,587,000 | 10,946,552,000 | 42,341,008,000 | 222,870,974,000 |
| **Jumla** | **18,327,208,816,000** | **1,101,591,775,000** | **601,700,826,000** | **156,087,579,000** | **20,186,588,996,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha*

**3.1.1. Uchambuzi wa baadhi ya Mafungu**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa mafungu yote 8, Kamati ilibaini na kupendekeza masuala yafuatayo:-

a) **Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa ndani na kuhakikisha rasilimali za umma zinatumika ipasavyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa katika mwaka 2025/26 Idara hii inakamililisha ujenzi wa mifumo mitatu ambayo ipo chini yake na kuhakikisha kuwa mifumo hiyo inasomana yenyewe kwa yenyewe.

Mifumo hiyo ni:-

i. Mfumo unaotumika katika kupanga, kufanya ukaguzi na kutoa taarifa kwa wakati *(Government Internal Audit Management Information System-GIAMIS);* ii. Mfumo unaotumika kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa ndani, CAG, PPRA pamoja na maelekezo ya Kamati mbalimbali za Bunge (*Government Audit Recommendation and Implementation*

*Information Tracking System-GARIITS);* na iii. Mfumo unaosaidia kutambua, kufanya tathmini ya vihatarishi na kupendekeza mikakati ya kudhibiti athari ya vihatarishi hivyo *(Government Enterprise Risk Management Information System-GERMIS)*.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati iliitaka Serikali kuhakikisha kuwa Wajumbe wa Kamati ya Ukaguzi katika Taasisi hawatoki tena kwenye Taasisi husika za Umma na badala yake nafasi hizo zipatikane kwa kuomba ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi, ushindani na uwajibikaji.

b) **Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**
**Mheshimiwa Spika,** kazi kubwa ya Fungu hili ni kusaidia kulinda nchi dhidi ya utakasishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na silaha za maangamizi na uhalifu mwingine wa kifedha. Mathalani, katika kipindi cha mwezi Julai 2024 hadi mwezi Februari, 2025 Kitengo hiki kilipokea miamala shuku **1,300,000** yenye thamani ya **Shilingi trilioni 463**. Kamati ilichambua makadirio ya matumizi ya Fungu hili kwa mwaka 2025/26 na kubaini kwamba bajeti hiyo haitoshelezi ikilinganishwa na majukumu. Awali bajeti ya Fungu hili ilikuwa ni **Shilingi 4,162,443,000** na hivyo Kamati iliielekeza Wizara kuongeza kiasi cha **Shilingi 1,000,000,000** ili kuanza mchakato wa kuimarisha Kitengo. Serikali ilikubaliana na Kamati na kuongeza bajeti ya Fungu hili kutoka **Shilingi 4,162,443,000** hadi **Shilingi 5,162,443,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Kitengo hiki kinakuwa Mamlaka kamili ili kuongeza mawanda ya kazi na kujitegemea zaidi kama ilivyo kwa nchi nyingine mfano nchi ya Zambia. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Kitengo hiki kinakuwa na wafanyakazi wa kudumu na kuwalipa mishahara kupitia Fungu hili na kuachana na utaratibu wa kuazima watumishi kutoka sehemu Taasisi mbalimbali za Umma ambazo mishahara yao hutofautiana wakati wanatekeleza majukumu yanayofanana.

c) **Fungu 021 – Hazina**
**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikiwasilisha mapendekezo ya miradi inayotakiwa kutekelezwa kwa Mfumo wa Ubia kati ya

Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP). Hata hivyo, bado Serikali haijafanikiwa kutumia mfumo huu wa utekelezaji wa miradi. Hivyo, Kamati iliitaka Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka 2025/26 miradi inayotumia mfumo wa PPP inaanza kutekelezwa ili kupunguza mzigo wa mahitaji ya fedha za maendeleo kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Fungu hili ndio lina jukumu la kusimamia Sera za fedha nchini, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo ili wananchi wengi waachane na matumizi ya fedha taslimu na kufanya miamala ya malipo ya ununuzi wa bidhaa na huduma:-

i. Kufanya mapitio ya gharama za uhamishaji wa fedha na kufanya malipo kwa njia ya kielektroniki ili kuhakikisha zinakuwa nafuu na kuwavutia wananchi kufanya miamala kwa njia ya kielektroniki; na

ii. Kuhakikisha Mwongozo wa gharama na tozo ya huduma pamoja na Miongozo kuhusu gharama za miamala ya fedha kutoka benki moja kwenda benki nyingine (bank to bank) unatekelezwa kikamilifu.

d) **Fungu 50 – Wizara ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha moduli ya uchakataji wa uchakavu wa mali na moduli ya uondoaji wa mali chakavu katika Mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS). Hata hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa Balozi zote zimesajili mali zao katika Mfumo huu ili kutambua mali zilizopo pamoja na thamani zake. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza ushauri uliotolewa katika mwaka wa fedha 2023/24 wa kuandaa Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mali za Umma.

## 4.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA FUNGU 45 - OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Waziri wa Fedha pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kufanya mashauriano kuhusu utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ina jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu yafuatayo:-

i. Kukagua Hesabu za Wizara, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizopo nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi wa mapato na matumizi ya fedha za umma Bungeni;

ii. Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara, Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmashauri;

iii. Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha uwepo wa uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na

iv. Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za umma, na mali za umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

### 4.1. Mwenendo wa utolewaji wa Fedha kwa Fungu 45 kwa mwaka wa Fedha 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 113,578,832,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 20,638,564,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 80,622,268,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **Shilingi**

**11,468,000,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Fungu hili lilipangiwa kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 850,000,000**. Hadi mwezi Aprili, 2025 Fungu limepokea jumla ya **Shilingi 99,079,159,647** sawa na **asilimia 87.89** ya bajeti yote. Kamati inampongeza ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*** kwa kuhakikisha Fungu hili linapata fedha za kutosha kwa ajili ya kuwezesha ofisi hii kutekeleza majukumu yake ya kikatiba ya udhibiti na ukaguzi. Mchanganuo wa utolewaji wa fedha ni kama unavyoonekana kwenye jedwali namba 3 hapo chini.

**Jedwali Na: 3. Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 Hadi Kufikia Aprili, 2025.**

| **Aina ya Matumizi** | **Bajeti iliyoidhinishwa 2024/25** | **Fedha iliyotolewa hadi Aprili, 2025** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 20,638,564,000 | 16,490,345,790 | 79.90 |
| Matumizi Mengineyo | 80,622,268,000 | 77,371,037,333 | 95.97 |
| Maendeleo Ndani | 8,828,000,000 | 2,577,776,524 | 29.20 |
| Maendeleo Nje | 2,640,000,000 | 2,640,000,000 | 100.00 |
| **JUMLA** | **112,728,832,000** | **99,079,159,647** | **87.89** |

**Chanzo**: *Randama Fungu 45, 2025*

### 4.2. Masuala ya Msingi yaliyobainika katika Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

#### 4.2.1. Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka 2024/25

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25 ofisi imefanikiwa kufanya yafuatayo:-

i. Kufanya kaguzi 1,485;
ii. Kukamilishaji Ripoti Kuu sita (6);
iii. Kuendeleza ujenzi wa Mfumo w Uvunaji wa Taarifa za Fedha (ADLS) awamu ya tatu kwa ajili ya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali;

iii. Kutoa mafunzo kwa Watumishi 713 kuhusu nyanja mbalimbali za ukaguzi;
iv. Kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi katika Mikoa ya Songwe na Katavi;
v. Kuwajengea uwezo Wajumbe 84 wa Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa Fedha (LAAC, PAC, PIC na PBC); na
vi. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa majengo ya Ofisi katika mikoa ya Mwanza na Ruvuma.

**4.2.2. Changamoto za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika mwaka 2024/25**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba Fungu hili linakabiliwa na uhaba wa rasilimali fedha ili kutekeleza masuala yafuatayo:-

i. Kuwajengea uwezo wakaguzi wote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa;
ii. Kuongezeka kwa mawanda ya ukaguzi ikiwemo ukaguzi wa wakati halisi (real time audit), ukaguzi wa kiufundi na ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi; na
iii. Ununuzi wa vitendea kazi ikiwemo kompyuta mpakato na vifaa vya kuwezesha ukaguzi wa kiufundi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza fedha kwa Fungu 45 ili ofisi iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**4.3. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/26 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kukamilisha utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) uliorejewa mwaka 2023/24 ambao unajielekeza katika kuimarisha kazi za ukaguzi wa Sekta ya Umma nchini. Kimsingi, Ofisi imelenga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

a) Ukaguzi wa mapato na matumizi, ukaguzi wa mifumo ya TEHAMA, ukaguzi wa ufanisi na ukaguzi wa kiufundi ili

kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali za umma;

b) Uimarishaji wa matumizi ya mifumo ya TEHAMA, upatikanaji wa vitendea kazi, ujenzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili kuboresha mazingira ya kuongeza tija na ufanisi wa utendaji kazi;

c) Kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi wa fedha za Umma na za Kisekta ili kuelewa Mamlaka, Majukumu, ripoti za CAG pamoja na kutambua mbinu za kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo; na

d) Kuwajengea uwezo Wakaguzi kwenye maeneo ya Mifumo ya TEHAMA inayotumika katika ukusanyaji wa mapato na matumizi, ukaguzi wa wakati halisi (real-time audit); ukaguzi wa ufanisi, ukaguzi wa kiufundi, ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi pamoja na uelewa wa mabadiliko ya viwango vya ukaguzi vya Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2025/26 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imetengewa jumla ya **Shilingi 123,362,123,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 23,058,129,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 87,356,994,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 8,828,000,000** ni fedha za ndani za maendeleo na **Shilingi 3,275,996,000** ni fedha za nje. Aidha, Fungu limeidhinishiwa kukusanya Maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 843,004,000** kwa ajili ya kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

**Jedwali Na 4: Ulinganisho wa Bajeti ya NAOT kwa Mwaka wa fedha 2024/25 Na Makadirio ya Bajeti Kwa Mwaka wa fedha 2025/26.**

| Maelezo | Bajeti iliyoidhinishwa (2024/25) | Makadirio ya Mwaka (2025/26) | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Maduhuli | 850,000,000 | 843,004,000 | -6,996,000 | -0.82 |
| **Matumizi ya Kawaida** | | | | |
| Mishahara | 20,638,564,000 | 23,058,129,000 | 2,419,565,000 | 11.72 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Matumizi Mengineyo | 80,622,268,000 | 87,356,994,000 | 6,734,726,000 | 8.35 |
| Jumla ya matumizi ya kawaida | 101,260,832,000 | 110,415,123,000 | 9,154,291,000 | 9.04 |
| **Matumizi ya Maendeleo** | | | | |
| Fedha za ndani | 8,828,000,000 | 8,828,000,000 | 0 | 0.00 |
| Fedha za Nje | 2,640,000,000 | 3,275,996,000 | 635,996,000 | 24.09 |
| Jumla ya fedha za Maendeleo | 11,468,000,000 | 12,103,996,000 | 635,996,000 | 5.55 |
| **Jumla Kuu** | **113,578,832,000** | **123,362,123,000** | **9,783,291,000** | **8.61** |

**Chanzo**: *Randama ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, 2025*

**4.4. Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/26**

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya fedha zote zinazoombwa na Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2025/26 ni **Shilingi 20,309,108,115,000.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,124,649,904,000** ni kwa ajili ya mishahara, **Shilingi 18,414,565,810,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **Shilingi 610,528,826,000** kwa ajili ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo na **Shilingi 159,363,575,000** ni fedha za nje.

**Jedwali Na. 5. Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mafungu yaliyochini yake kwa mwaka 2024/25**

| Fungu | Matumizi Mengineyo | Mishahara | Miradi ya Maendeleo (Ndani) | Miradi ya Maendeleo (Nje) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | 14,219,350,702,000 | - | - | | 14,219,350,702,000 |
| 06 | 11,430,429,000 | 2,366,512,000 | 141,967,000 | 1,136,430,000 | 15,075,338,000 |
| 10 | 4,164,536,000 | 945,493,000 | 958,949,000 | - | 6,068,978,000 |
| 13 | 5,162,443,000 | - | - | - | 5,162,443,000 |
| 21 | 783,658,931,000 | 985,183,709,000 | 588,911,977,000 | 106,520,060,000 | 2,464,274,677,000 |
| 22 | 3,131,303,648,000 | 16,616,460,000 | - | - | 3,147,920,108,000 |
| 23 | 91,566,300,000 | 7,468,014,000 | 741,381,000 | 6,090,081,000 | 105,865,776,000 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 50 | 80,571,827,000 | 89,011,587,000 | 10,946,552,000 | 42,341,008,000 | 222,870,974,000 |
| **Jumla** | 18,327,208,816,000 | 1,101,591,775,000 | 601,700,826,000 | 156,087,579,000. | 20,186,588,996,000 |
| **45** | 87,356,994,000 | 23,058,129,000 | 8,828,000,000 | 3,275,996,000 | **122,519,119,000** |
| **JUMLA KUU** | **18,414,565,810,000** | **1,124,649,904,000** | **610,528,826,000** | **159,363,575,000** | **20,309,108,115,000** |

***Chanzo:*** *Randama za Mafungu ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya CAG,2025*

## 5.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26, Kamati ina maoni na Mapendekezo yafuatayo:-

### 5.1. Kufanya mabadiliko kwenye Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa Sura ya 437 ili Mfumo wa malipo kwa njia ya kielektroniki *(Cashlite)* uanze kutekelezwa

**Mheshimiwa Spika**, kwa muda mrefu Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuhusu kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kutumia mifumo ya kielektroniki katika kufanya malipo ili kuzuia upotevu wa mapato yatokanayo na kodi. Malipo ya kielektroniki ni miamala inayofanyika kupitia kadi za malipo, simu za mkononi na malipo ya papo kwa papo. Lengo ni kurahisisha miamala na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu. Kamati inaisisitiza Serikali kufanya mabadiliko katika Kifungu cha 8 cha Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa Sura ya 437 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 438 ili kuanzisha sharti la lazima la kufanya malipo kwa njia ya kieletroniki wakati wa kufanya manunuzi ya huduma na bidhaa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano Serikali inaweza kuweka ukomo wa malipo ya fedha taslimu wa kiwango cha chini pamoja na kupunguza gharama za kufanya miamala ili kutohamasisha matumizi ya fedha za taslimu kwenye malipo ya manunuzi ya bidhaa na huduma.

**5.2. Serikali kupitia upya Muundo wa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Ndani ya Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Idara ya Mkaguzi wa Ndani wa Serikali ipo chini ya Wizara ya Fedha ambapo Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali anawajibika kiutendaji na kiutawala kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha. Aidha, Mkaguzi wa Ndani katika Taasisi za Umma anawajibika kiutawala na kiutendaji kwa Mkuu wa Taasisi husika. Hata hivyo, muundo huu umeonekana kuwa na changamoto kutokana na Sheria kutompa mamlaka Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali kuwawajibisha wakaguzi wa ndani pindi wanapobainika kutenda makosa.

Aidha, muundo huu haumpi Mkaguzi wa ndani uhuru katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuripoti kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambaye kimsingi ni mkaguliwa. Muundo huu umekuwa ukisababisha hoja za Mkaguzi Mkuu wa ndani kutofanyiwa kazi kwa wakati na baadae kujitokeza katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Serikali kufanya mabadiliko ya muundo wa Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali pamoja na Sheria ya Ukaguzi wa Ndani ya Umma ili Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali awe anawajibika kiutawala kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na kiutendaji kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia Kamati ya Ukaguzi ya Kitaifa (The National Audit Committee). Vilevile Kamati inataka Sheria iweke wazi uwajibikaji na uhuru wa Mkaguzi wa ndani wa Taasisi za Umma kwa kumtaka Mkaguzi wa Ndani kuwajibika Kiutawala kwa Maafisa Masuuli na kiutendaji kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa
Serikali.

**5.3. Kuwezesha kimitaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) na Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB)**

**Mheshimiwa Spika,** jukumu kuu la Benki ya TADB ni kuwa chachu ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi, wa kati na mrefu kwa ajili ya kufanikisha maendeleo jumuishi ya sekta ya kilimo nchini, na kuchangia katika Dira ya Taifa ya Maendeleo katika kuhakikisha utoshelevu na usalama wa chakula, maendeleo ya uchumi na

kupunguza umaskini. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2015, TADB imefanikiwa kutoa mikopo ya **Shilingi 971,890,000,000** ikinufaisha zaidi ya wakulima 1,948,801 na biashara 686 (biashara endelevu ni 478). Kwa sasa Benki hii ina mtaji wa jumla ya **Shilingi 924,000,000,000.** Hata hivyo, benki hii haipokei amana kama ilivyo kwa benki za biashara. Ili kutimiza kikamilifu dhamira ya TADB na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya fedha kwa ajili ya kilimo, benki hii inahitaji jumla ya **Shilingi 2,950,000,000,000,** hivyo kufanya nakisi ya **Shilingi 2,026,000,000,000.**

**Mheshimiwa Spika,** Benki ya TIB ina jukumu la kutoa huduma za fedha kwa miradi ya maendeleo kwa gharama nafuu ili kujenga Taifa lenye uchumi shirikishi, mseto, mahiri na wenye ushindani. Hata hivyo, mwenendo wa ufanisi wa benki hiyo sio wa kuridhisha kwa sababu katika kipindi cha miaka mitatu mapato ya benki yamekuwa yakishuka kutoka **Shilingi 62,700,000,000** mwaka 2022 hadi **Shilingi 35,600,000,000** mwaka 2024 kufuatia kushuka kwa kasi ya utoaji wa mikopo kutokana na kiwango hafifu cha mtaji. Hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2024, mtaji wa benki kwa mujibu wa Kanuni za Taasisi za fedha (core capital) ulikuwa **Shilingi 90,226,000,000** kiwango ambacho ni kidogo ikilinganishwa na kiwango cha **Shilingi 200,000,000,000** kinachotakiwa kwa mujibu wa Kanuni za Taasisi za Fedha za Maendeleo zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania mwaka 2021. Kiwango hicho kidogo cha mtaji kinazuia ukuaji wa mizania ya benki kwa sababu benki haina uwezo wa kukopa kwa kutumia mtaji kama nyenzo ili kuweza kukopesha miradi mikubwa ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia mikakati ya Serikali ya kukuza uwekezaji katika sekta ya kilimo na kuongeza viwanda nchini, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha inatoa mitaji katika benki hizo ili kuongeza ufanisi na kuwezesha benki hizo kuwa shindani.

### 5.4. Kutungwa kwa Sera ya Kodi

**Mheshimiwa Spika,** Sera ni mkakati au mwongozo unaotumiwa na Serikali kupanga na kutekeleza ukusanyaji wa kodi. Sera inatoa maelekezo ya aina ya kodi na namna zitakavyokusanywa, viwango vya kodi pamoja na matumizi ya mapato yanayotokana na kodi. Pamoja na kwamba kuna Sheria mbalimbali za kodi

nchini, Tanzania haina sera ya kodi moja inayotoa muongozo wa masuala mbalimbali kama vile; utolewaji wa vivutio na misamaha ya kodi, utozaji, kuchochea ukuaji wa uchumi na ukuaji wa sekta mbalimbali pamoja na usimamizi wa kodi za ndani na za Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa Sera hiyo kunasababisha nchi yetu kutokuwa na viwango vya kodi vinavyotabirika pamoja na kuongeza vitendo vya ukwepaji wa kodi. Hivyo, Kamati inaona kwamba kuna umuhimu wa kuandaa Sera ya kodi ili kutoa mwongozo wa masuala yote ya kodi.

**5.5. Kuboresha Utendaji Kazi wa Wakala wa Huduma ya ununuzi Serikalini (GPSA)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura ya 245. Baadhi ya Majukumu makubwa ya GPSA ni kama ifuatavyo:-

i. Kutoa huduma mbalimbali kwa Taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali, zikiwemo ununuzi wa pamoja wa magari, mafuta, na vifaa vya ofisi;
ii. Kusaidia Taasisi kupata bidhaa kwa bei nafuu na ubora unaokubalika;
iii. Kutoa huduma za ugomboaji na uondoshaji wa mizigo; na
iv. Kusaidia katika taratibu za forodha na usafirishaji wa mizigo ya Serikali kutoka bandarini, viwanja vya ndege, na mipakani.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala umejiwekea utaratibu wa kugomboa mizigo kwa kuzingatia muda wa siku 7 kwa mizigo ya bandarini na siku 3 kwa mizigo ya uwanja wa ndege. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba kwa muda mrefu GPSA imekuwa ikichelewesha ugomboaji wa mali hasa magari. Mfano, Mfuko wa Mahakama katika mwaka 2023/24 uliagiza magari 19 kupitia wakala lakini hadi sasa wamepokea magari 13 tu, licha ya magari yote kulipiwa na kukamilika kwa taratibu za ugomboaji kwa wakati. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuboresha ufanisi wa GPSA ili kuhakikisha hauathiri utendaji kazi wa Taasisi nyingine.

**6.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuhitimisha kwa kukushukuru wewe Mhe. Dkt. Tulia Akson, Mb Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) pamoja na Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza vema Bunge. Nawashukuru pia Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Mb Waziri wa Fedha na Mhe. Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao wakati wa kuchambua utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26. Aidha, napenda kumshukuru Dkt. Natu El-Maamri Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Manaibu Katibu Wakuu, Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao katika kujadili, kuchambua na kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Ndg. Charles Kichere Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ushirikiano wake kwa Kamati wakati wa kujadili utekelezaji wa majukumu ya Ofisi yake kwa mwaka 2024/25 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwapongeza wajumbe wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Twaha Mpembenwe, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb- Mjumbe

10. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Stella Alex Ikupa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, Mb- Mjumbe
13. Mhe. Shally Josepha, Raymond, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb- Mjumbe
15. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb - Mjumbe
16. Mhe. Rashid Abdallah Rashid, Mb - Mjumbe
17. Mhe. Bahati Khamis Kombo, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb- Mjumbe
19. Mhe. Omar Ali Omar, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Bahati Keneth Ndingo, Mb - Mjumbe
21. Mhe. Yahya Ally Mhata, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** mwisho si kwa umuhimu, nimshukuru Ndg. Baraka Leonard Katibu wa Bunge kwa niaba ya Watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu uliowezesha kufanikisha shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu nane (8) ya Wizara ya Fedha pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2025/26 kama yalivyowasilishwa na Waziri wa Fedha yenye jumla ya **Shilingi 20,309,108,115,000** ambapo **Shilingi 1,124,649,904,000** ni mishahara, **Shilingi 18,414,565,810,000** ni matumizi mengineyo na **Shilingi 769,892,401,000** ni matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
04 Juni, 2025

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Tunakushukuru sana kwa usomaji wa kipekee kabisa ambao kwa kweli leo umeleta jambo la tofauti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimejulishwa hapa kwamba pia yupo Gavana wa Benki Kuu, Ndugu Emmanuel Tutuba, karibu sana, pole naona jina lako lilikuwa limesahaulika kidogo kwenye orodha, lakini tunafurahi kukuona karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu wageni wengine walisha tambulishwa, wageni wengi tunaowaona sasa hapa ndani ni wa Mheshimiwa Mbunge wa Iramba Magharibi, Waziri wa Fedha, sasa nitawatangaza kwa makundi halafu mtasimama wote kwa pamoja.

Nimejulishwa hapo kwanza yupo Mkuu wa Wilaya *(DC),* karibu sana; nimejulishwa yupo *DAS* (Katibu Tawala) karibu sana; na Mkurugenzi, karibu sana; *(Makofi)*

Wapo pia tunaita Makatibu wa Kata? Wanaitwa Makatibu Kata? Haya Makatibu Kata msimame wote pamoja, siyo Makatibu Kata wa Chama Cha Mapinduzi, Makatibu Watendaji sasa sijakumbuka jina lao, anhaa Watendaji wa Kata?

Haya Watendaji wa Kata wasimame wote kwa pamoja, ahsante sana; Waratibu na Maafisa Elimu wa ngazi ya Kata; Maafisa Tarafa, karibuni sana; Walimu Wakuu, Walimu Wakuu naona bado hawajapata nafasi ya kuingia humu ndani, lakini wataingia baadaye tutawatambua. *(Makofi)*

Hawa wageni wengine wako 420 hawa ni viongozi wa Chama Cha Mapinduzi ngazi zote kutoka Iramba Magharibi wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wilaya. *(Makofi)*

Mwenyekiti wa Wilaya amekaa sehemu gani? Enhee haya karibuni sana Bungeni. Sasa mkiwa bado mmesimama hivyo…*(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri kwani nimesema na wewe usimame? Naona umesimama. Haya hapo nimeambiwa wapo viongozi wa Chama Cha Mapinduzi kata zote na viongozi wote wa Serikali, Wilaya, Kata, haya karibuni sana Bungeni. Karibuni sana tunafurahi kuwaona watu kutoka Iramba Magharibi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine hawa watakapokuwa wamewapisha wataendelea kuingia na tutaendelea kuwatangaza wageni wenu.

Sasa tunaanza uchangiaji kama ilivyo ada tutaanza na Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha na mimi nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa fursa hii na neema ya uhai, lakini kipekee niseme moja kwa moja naunga mkono hoja ya bajeti hii ya Wizara ya Fedha na kwa kuwa mimi ni sehemu ya Kamati ya Bajeti naunga mkono Taarifa yetu na mapendekezo yetu ya kwenye Taarifa ya Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri - Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri - Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu - Dkt. Natu na Mlipaji Mkuu wa Serikali Naibu Makatibu Wakuu, Wakuu wote wa taasisi chini ya Wizara hii ya Fedha, wakuu wote wa vitengo na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa namna ambavyo wamefanya kazi yao nzuri katika kipindi chote sisi tulipokuwa tunahudumu Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ulitupa kazi kwenye Kamati hii wametupa ushirikiano wa kutosha, Serikali imekuwa sikivu, mapendekezo yetu yote wamekuwa wakiyatekeleza ninasimama hapa nikiwa nafahari kubwa kwamba kwa kweli kwa kipindi cha miaka mitano Wizara hii imetekeleza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jumamosi iliyopita kama Bunge tumefanya tukio kubwa la kutoa Tuzo ya Heshima kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo imetokana na kazi nzuri ya Serikali ya Awamu ya Sita, lakini kwa kadri ambavyo uliwasilisha taarifa ile na sababu zilizopelekea Bunge kutoa tuzo ile ni utekelezaji wa miradi ya kisekta ya

kimkakati na ya huduma za jamii, lakini kazi ile imetokana na uratibu wa Wizara hii ya Fedha ya kutekeleza majukumu yao ya utafutaji wa vyanzo vya fedha vya ukusanyaji na ugawaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia kazi nzuri waliyofanya hususani ya utafutaji na ukusanyaji, nasimama hapa nianze kwa kuipongeza Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kipindi chote cha miaka hii mitano tumeona kila mwaka kulikuwa na ongezeko la makusanyo ya mapato, lakini kipekee kwa miezi hii tisa ambayo taarifa rasmi iliwasilishwa niipongeze mamlaka hii kwa kuweka rekodi kwa kuvuka lengo la makusanyo ya mapato kila mwezi kwa kipindi chote cha miezi tisa mpaka saa hivi na miezi 11 ambayo imewezesha kuifanya Serikali yetu ya Awamu ya Sita kuvuka malengo kwa zaidi ya 78% kulinganisha na mwaka 2020/2021. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapoipongeza Mamlaka hii ya Mapato chini ya uongozi wa Kamishna Yusuph Mwenda, makamishna wote, lakini na watumishi wote wa *TRA* kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuongeza ukusanyaji wa mapato lakini napongeza jitihada zao za ubunifu, napongeza jitihada zao za kuwahudumia wafanyabiashara, napongeza jitihada zao za kuweka mazingira wezeshi, lakini kipekee pia hata ziara za Kamishna Mkuu ambazo kweli tumeona kwa mara ya kwanza kupitia mikoa yote ya Tanzania, kuwasikiliza wafanyabishara. Sisi Kamati ya Bajeti tuna matumaini *Finance Bill* ijayo itakuwa nyepesi zaidi kwa sababu mwenyewe Kamishna amesikiliza wafanyabiashara, lakini kupitia *think tank* ya Wizara ya Fedha tunaamini kabisa itakuwa ni *Finance Bill* ya *4Rs* - maridhiano, utahimilivu, itazingatia maboresho, itazingatia na vyanzo vipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa jambo hili ni endelevu na tunazungumzia bajeti ya mwaka 2025/2026 napenda niishauri Wizara ya Fedha kwa namna ya kuongeza mapato zaidi kwa kuwa sisi tulitembelea Bandari ya Dar es Salaam tumeona namna gani maono ya Mheshimiwa Rais ya kukaribisha sekta binafsi pale kupitia kampuni ya *DP World* na ada zilivyoongeza mapato kupitia mamlaka hii. Sasa nilikuwa napendekeza *TRA* iendelee

kuzitazama hata bandari hizi ndogo ndogo zile zingine zirasimishwe kupitia ushirikiano na Serikali bandari bubu kwa mfano hapa ninaposimama sisi Mkoa wa Pwani tuna Bandari ya Kisiju, tuna Bandari ya Nyamisati, lakini tuna Bandari ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Bandari ya Bagamoyo pale nataka nimshukuru na kumpongeza meneja wetu mpya wa Wilaya - Bwana Baraka lakini nataka niseme pana malalamiko naiomba *TRA* ikae na wadau pale kuhusu tozo au kodi ya kuingiza madumu ya mafuta katika Bandari ya Bagamoyo kwa kiwango ambacho kiliwekwa pale ni shilingi 10,000 lakini maeneo mengine Bandari ya Mbweni, Bandari ya Kunduchi, Bandari ya Pangani inaonekana kama kiwango ni bei shilingi 8000 mpaka shilingi 7000. Kwa hiyo inaonesha Bandari yetu ya Bagamoyo inakuwa si shindani na hivyo kupungua kwa mizigo inayoingia kwenye Bandari ya Bagamoyo ambayo inasababisha pia kupungua hata mzunguko wa fedha kwenye bandari yetu pale na Mji wa Bagamoyo, lakini hata kwa wafanyabiashara wa eneo la Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe Kamishna Mkuu ajaribu kuangalia na kuja atutembelee Bagamoyo na kukaa na wafanyabiashara na kusikiliza ili kuweza kupata mfumo mpya wa utozaji kodi katika biashara hii ya mafuta, lakini tuiombe pia Serikali iendelee kurasimisha biashara zingine kuingia kwenye Bandari yetu ya Bagamoyo kwa sababu ni bandari ya kimkakati kwa sasa na tunafurahi kwamba ilani inayokuja Serikali imepanga kujenga Bandari mpya ya Bagamoyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo tunapendekeza pia uboreshaji wa miundombinu pale kwenye Bandari ya Bagamoyo Ofisi ya *TRA* kulikuwa na Jengo la *Customs* zamani lina miaka zaidi ya 100 ni jengo la urithi wa dunia, lakini tunatamani sasa *TRA* iangalie inaweza kuboresha vipi miundombinu ya pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee pia niimpongeze Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali; *CAG* Ndugu Kichere, ofisi yangu ya zamani kwa kazi nzuri waliyoifanya na namna pia Serikali

ilivyoiwezesha ofisi hii maana yake ninapozungumza hapa zaidi ya 90% ya bajeti yao wameshapewa, kwa hiyo ni wazi kwamba kazi nzuri ya *CAG* imetokana uwezeshaji huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilishauri Serikali, Mheshimiwa Waziri kwenye Kamati kupitia hizi *TRAT* na *TRAB* tulikushauri kwa namna ambavyo mashauri ya kesi yapo kwenye mamlaka hizi walau ulitekeleza mwaka wa fedha wa mwaka jana umefanya uteuzi na nisimame hapa kupongeza *TRA* na *TRAB* na Mahakama ya Rufaa walau kwa kupunguza kidogo kwa sababu mwaka wa fedha 2023 tuliona kwamba mashauri yalikuwa zaidi shilingi trilioni 10. Ni mashauri siyo kama fedha inaibiwa ni mashauri shilingi trilioni 10.49 lakini kwa mwaka wa fedha huu 2024 kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* mashauri sasa yamefika shilingi trilioni 9.8 lakini bado *CAG* amependekeza Serikali iziwezeshe hizi mamlaka kwa fedha, kwa rasilimali watu ili wasikilize mashauri haya kwa haraka na hii kodi inayobishaniwa iweze kukusanywa na kuleta tija na kuweza kufanya kazi ambayo imekusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru na wewe binafsi kwa kutupa heshima ya kuwa Wajumbe wa Kamati hii ya Bajeti, kwa maelekezo yako ya mara kwa mara, kwa namna ambavyo tumeweza kuisimamia Serikali ambapo leo tunajivunia pengine mwaka huu wa fedha tutaona rekodi mpya kwamba Serikali imevuka lengo iliyojiwekea ya kukusanya mapato yote na kwa kuweka rekodi ya mwezi Desemba shilingi trilioni 3.5 makusanyo ya juu kabisa tangu mamlaka hii imeanzishwa mwaka 1996. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kupongeza pia Serikali kwa kusikiliza kilio cha wastaafu wa nchi hii kwa kuja na mifumo ya uboreshaji wa uhakiki, lakini pia kuanza mchakato wa kuhuisha viwango vya malipo ya wafanyakazi wastaafu wanaolipwa kupitia Hazina. Huu ndiyo usikivu wa Serikali yetu, mmesikiliza mengi ya ushauri, mmeimarisha Kitengo *cha Internal Auditor* katika Serikali na ulikuwa ushauri wa Kamati yetu, mmeanzisha mamlaka ya *Tax Ombudsman* ya kusikiliza walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikushukuru Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kunipa heshima ya kuwa balozi wa kodi binafsi na kwa kuitumikia nafasi hii kwa Bunge hili kwa kuendelea kuhamasisha wananchi wadai risiti na wafanyabiashara waendelee kutoa risiti, lakini kipekee kwa kutuwezesha kuona namna kodi inayokusanywa matumizi yake tumepata kutembelea miradi mbalimbali ya kimkakati na ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nina furahi kwamba nimepata fursa kutokana na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali hii kutembelea miradi mingi sana katika awamu hii kuliko awamu yoyoye ambayo nimepata kuhudumu kwenye Ubunge huu wa Viti Maalum na niwashukuru wanawake wa Mkoa wa Pwani kwa fursa hii waliyonipa ya kuwa Mbunge wao wa Viti Maalum kwa vipindi kadhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiweka nchi yetu kwenye ramani ya maendeleo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Riziki Said Lulida, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, ajiandae.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru na Mwenyezi Mungu nimshukuru zaidi kwa kutujalia kupata afya njema na kutuwezesha kuwepo hapa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa sana ya kuhakikisha nchi inakwenda katika utulivu na amani na kutulia kwake na uvumilivu na ukimya ambao ameamua, basi hili ni jibu tosha kuwa yeye anapenda amani ndani ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nitazungumzia njia kuu za mapato ambazo inabidi zisimamiwe na Wizara. Tunahitaji mapato zaidi, sasa hivi Tanzania tujifunze kwa wenzetu baadhi wanaofanya mabadiliko makubwa ya kiuchumi, hatutaki tena kuchukua

mahela kutoka nje ambayo inakuwa kama ni kukopakopa nako kama ni masimango, lakini Mwenyezi Mungu kutokana na *trend* wanayokwenda nayo ya kiuchumi, nasema Mwenyezi Mungu azidi kuwabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika nchi hii tuna maeneo manne ambayo tunabidi tuyasimamie, katika kilimo tunaingiza fedha za kigeni hasa katika mazao kama ya korosho. Korosho tunaita ni *green gold* lazima yapewe kipaumbele ili tuzidi kuzalisha na kupata mapato zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uchukuzi hizi bandari zetu zinatuletea pesa za kigeni kwa meli zinazoingia na kwa kweli hali ya kiuchumi ndani ya uchukuzi nayo inakwenda vizuri, lakini nitaizungumzia Wizara ya Maliasili.

Mheshimiwa Spika, mimi ni balozi na katika kuwa balozi nina balozi mwenzangu ambaye ni Mwigulu Nchemba huyu ni balozi wa watu wenye ulemavu. Hii Wizara naomba na balozi mwenzangu na wewe unisikilize kwa makini na uje unipe majibu mazuri, kwanza wewe ni msikivu, nilikushauri suala la watu wenye ulemavu na kupata gawio lao katika kupitia Wizara na pamoja vijana hatuna cha kusema zaidi ya kukuombea Mwenyezi Mungu urudi tena katika Bunge hili mwezi wa 11 na kujiombea sisi sote tuweze kurudi katika wakati huo na hili ninaloliomba kwako naomba ukalifanyie kazi na nina imani utaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili inaingiza Pato la Taifa 22.5% lakini katika hii Wizara, Utalii peke yake unaingiza 17% lakini katika eneo la utalii inaingiza fedha za kigeni 30%. Hili eneo ninataka liboreshwe ili hizi pesa za kigeni badala ya kupata 30% tuna uwezo wa kupata hata 50%. Tujifunze tuona wenzetu wa Seychelles utalii peke yake inawaingizia karibu 75% ya uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nazungumza hivi? Mheshimiwa Rais alileta *Royal Tour,* hii *Royal Tour* imeleta wageni wa kutosha, watalii wanaoingia Tanzania ni wa kutosha wengi na watalii hawa wamevutiwa na *spirit* aliyokuja nayo Mheshimiwa Rais ya

kuitangaza Tanzania duniani kote. Sasa tuna cha kujifunza hapa, watalii wanataka kuja hapa wakiwa na pesa zao za kigeni, wanahitaji malazi bora, wanataka barabara bora, miundombinu bora, mawasiliano bora ili na wao wazidi kuja wengi na wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko katika vita ya kiuchumi, nchi zote za jirani zinafanya utalii, lakini utalii wa Tanzania umetukuka. Sasa nakuomba balozi wangu wa watu wenye ulemavu mimi ni mlemavu mwenzio, ninakuomba kitu kimoja angalau ukakifanyie kazi na ukiletee majibu. Leo pesa zote makusanyo yanayokusanywa na Ngorongoro, *TANAPA* yanakuja Mfuko Mkuu, zikija huku kurudisha kule inakuwa ni *issue,* bahati mbaya mimi ubalozi wangu lazima niusemee humu ndani tunahitaji wakusanye na watoe gawio kwenu, hapa msiwe na kigugumizi na tutahakikisha pato unalolitegemea la 30% la *forex* litaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilioni *clip* moja watalii wamekuwa *stuck* katika daraja huko kipindi cha mvua na walipofika pale wanaongea wanaomba duniani wasaidiwe wako katika mazingira magumu, leo ndani ya mbuga ni sehemu ambayo ni hatarishi, kuna wanyama wakali ikiwemo simba na tembo. Sasa ukiwaacha watalii wakiwa katika mazingira yale kwa kweli balazi mwenzangu naomba uniheshimieshe kwa hili nakuomba tafadhali na bahati nzuri mkae chini tu muwe na *MOU* tunataka sisi hela hii mtupatie, watawapeni *at the right time*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Sheria ya Ununuzi kuna kitu kinaitwa *you have to buy at the right time, with the right quality, quantity and price with the environment.* Sasa kama tunakaa tunagemea watalii wanakuja, lakini barabara mbovu, wenzetu wata-*take advantage* ya kutuangamiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kiwambie nilikuwa balozi wa kuhakikisha Geti la Gologonjwa halifunguliwi kwa kutaka Serengeti ipate mapato, leo Serengeti inapata mapato makubwa, lakini nakwambia hili kwa vile nimelifanyia tafiti. Katika kulifanyia tafiti nina imani kuwa hela mnazozihitaji kwa kupitia

mashirika yetu *TANAPA*, Ngorongoro zitakuwa kubwa. Mashirika yako mengi, lakini haya mawili kwa vile hela zinakwenda Mfuko Mkuu zinakwenda kwa kusuasua kurudishwa kule kwao kwa kweli inawapa shida kubwa. Imani yangu umenisikia na utaifanyia kazi na bado nakwamini balozi mwenzangu kuwa utalifanyia kazi. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Spika, la pili Tanzania tuna NGOs 9840 na katika hizi NGOs 9840 wanasema wanaingiza pesa ambazo ni shilingi trilioni 2.4. Mimi maswali yangu Mheshimiwa Waziri na Gavana wa Benki Kuu ambao ninyi mnadhamana ya kusimamia pesa za Tanzania zinazoingizwa nchini, je, mnazikagua hizi pesa? Lakini vilevile je, zinaingia katika mpango mkakati wa matumizi bora ya nchi? Maana yake leo tunavyopata pesa kama zile tunataka tujue kilimo zimekwenda kiasi gani, tunataka tujue uvuvi zimeenda kiasi gani maana yake kama hamzisimamii hizi hela zinaingia katika movement na tumeona hizi pesa zinaingia katika movement, Congo wametengeneza M23. Hii M23 sasa hivi inaifanya nchi haitawaliki kwa vile hela za kutakatisha zimeingia kule na zinafanya vitu ambavyo havina maendeleo na mashiko ya nchi. Nina imani katika hizi pesa ambazo zinaingia kama hamzifanyii tathmini na kujua zinakwenda wapi na mkazifanyia ukaguzi zitaingia no reforms, no election. Watatumia nguvu kubwa ya kufanya matumizi hayo kwa vile nini wanajua hapo ndiyo eneo ambalo tutaigusa nchi hii na kuingiza katika tafaruku.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu Mheshimiwa Rais aweze kusimamia hili na ninyi sisi watendaji sote kwa pamoja tusiruhusu kuileta mianya ambayo itatufanya nchi hii iingie katika machafuko. Imani yangu mimi ninapenda sana nchi iwe na amani. Watu wa kwanza wanaoathirika katika machafuko ni walemavu. Mimi siwezi kukimbia, hivyo, nitakuwa mimi ninahangaika, wanawake na watoto watahangaika hapa. Hivyo, watu wanaotaka kuleta machafuko kama hayo tusikubali. Watanzania lazima tuungane kwa pamoja tusimame na amani na utulivu na hili Mwenyezi Mungu ninaamini itawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia maendeleo ya Mikoa ya Lindi na Mtwara, kwa nini? Mikoa mingine ninaona inakimbia katika maendeleo, lakini hata mipango ya pesa ambazo zinakwenda katika mikoa hiyo zinakuwa chache. Sasa sisi sote tunazungumza ni kama watoto wa familia moja, watoto wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaomba katika maeneo ambayo tunayazungumzia kila siku lazima yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunahitaji barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Mtwara mpaka Namtumbo ziimarishwe, kwa nini ninazungumza? Hii sasa hivi barabara ya kutoka Lindi mpaka Mozambique ni barabara ya kimataifa. Watu wa Mozambique wanategemea mizigo yao kuchukua kutoka Tanzania, lakini leo kama wamechukua mizigo kutoka Tanzania unaupeleka Mozambique katika mazingira yale kwa kweli hatujaifanyia haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tusimame na bandari ndogo ndogo, nimeona mwenzangu amezungumza hapa. Leo Lindi tuna bandari ndogo. Tukismama na bandari ya Lindi tukasimama na Comoro kwa kweli uchumi tutakaoupata hii tunayosema tunategemea shilingi trilioni 50 ambazo zimeshaweza kukusanywa mpaka leo nina imani Mheshimiwa Waziri wewe ni mchumi na wewe ni mwanasheria utazisimamia tutaweza kuvuka mapato yatazidi kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, mimi ninasema tena Wizara ya Madini, Wizara ya Kilimo, na Wizara ya Utalii tusimame kwa pamoja Wabunge tuangalie na tuone tuweze kuisimamia na watendaji wakakae kusimamia hizi Wizara ili uchumi bora wa Tanzania hii uweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitaizungumzia tena Lindi; Lindi ni kisiwa, leo Mkoa wa Lindi kipindi cha masika mtu wa Liwale hawezi kutembea, huwezi kwenda Liwale hata kwa gari,, mpaka hata Waziri alikwenda wakati ule Mheshimiwa Bashungwa alikwenda kwa helkopta. Sasa yeye alikwenda kwa helkopta, je, wananchi wa Lindi wanafanya nini.

Mheshimiwa Spika, hivyo, ninomba katika bajeti zenu hata kama pengine mlikuwa mmeitoa bajeti ndogo ninaomba bajeti ya Mkoa wa Lindi barabara zake ni mbaya, huwezi kulinganisha na mikoa mingine yote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ninakushukuru sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri - balozi kwa watu wenye ulemavu. Leo ninaona walemavu wako vizuri na wanakupenda, wanasema ahsante sana. Mwenyezi Mungu awabariki nyote. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Riziki Lulida, nilikuacha umalizie mchango. Nimesikia hapo umeitaja *M23*.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Nimetaja nini?

**SPIKA:** Kisha nikakusikia umetaja chama fulani hivi na jambo lao na kama unaweza kuzihusianisha hivi. Nimeelewa kama ulikuwa unazihusianisha hizi mbili?

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunirekebisha. Amenambiaje? Sijamsikia vizuri.

**SPIKA:** Kumbe uko tayari kwa marekebisho. Basi mchango wako kuhusu lile eneo la *M23* ukikilinganisha na chama cha siasa kilicho hapa nchini ninayaondoa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana, tuko pamoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya Mheshimiwa Juma Hamad Omar ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja muhimu hii ya Wizara ya Fedha na kabla sijasahau ninaunga mkono hoja ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, ukisoma taarifa ya Waziri moja ya jukumu kubwa la Wizara ya Fedha ni kutafuta vyanzo vya fedha na kukusanya mapato.

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wote humu ndani kwenye majimbo yetu tuna miradi ya maendeleo ambayo inaendelea kutekelezwa. Tuna miradi ya maji, tuna miradi ya afya, tuna miradi ya elimu, tuna barabara, lakini miradi yote hii haiwezi kutekelezwa kama hakuna fedha. Kama fedha hazijatafutwa, hazijakusanywa miradi yote hii niliyoitaja haiwezi kutekelezeka itabaki kwenye makaratasi na itakuwa maneno matupu.

Kwa hiyo, Wizara hii ina jukumu kubwa sana la kubuni vyanzo na kuhakikisha mapato yanakusanywa ili miradi ya maendeleo iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, ukitembelea tovuti au *website* ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ambayo ndiyo taasisi kubwa inayosimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani hapa nchini ukiingia kwenye tovuti yao ukaangalia takwimu za makusanyo, ukilinganisha na malengo ya makusanyo kwa mwaka huu wa fedha tulionao ambao unaisha mwezi huu na ukienda kwenye tovuti hiyo utakuta kwamba kuna takwimu za robo ya kwanza, robo ya pili na robo ya tatu na takwimu zote hizo zinaonesha Mamlaka ya Mapato Tanzania imevuka malengo ya makusanyo yake, yaani imefikia 100% na zaidi kwa baadhi ya miezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitumie fursa hii kwa kweli nimpongeze Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, Ndugu Yusuph Mwenda na Menejimenti yote ya *TRA* na wafanyakazi wote kwa jitihada kubwa ambazo zimeonekana kwa vitendo kwa takwimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuweza ku-*maintain* kufikisha 100% ya makusanyo *against* malengo tangu mwaka huu wa fedha ulioanza kwa *at least* kwa robo tatu hizi (miezi tisa ya kwanza) ni jambo ambalo linaonesha kabisa kuna menejienti nzuri na kuna kitu kikubwa ambacho kinafanyika ndani ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pongezi hizi kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ninazitoa hasa kuwapongeza kwa kuendana na dhamira na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo aliyatoa *clearly* kabisa kwamba anataka Mamlaka ya Mapato Tanzania ikusanye mapato kwa walipakodi kwa *approach* ya urafiki na majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *feedback* ambayo tunaipata kwa walipakodi ambao ndiyo wapigakura wetu ni kwamba kuna *improvement* kubwa sana ya Mamlaka ya Mapato ukilinganisha na miaka ya nyuma kwa namna ambavyo wanatengeneza urafiki na walipakodi. Wanakaa na walipakodi na kunapokuwa na changamoto yoyote wanaitatua kwa njia ya majadiliano na maelewano tofauti na miaka ya nyuma ambapo kulikuwa na hali kama ya *enmity* kama uadui kati ya Mamlaka ya Mapato na walipakodi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi niwapongeze *TRA* kwa kusikiliza na kutembea kwenye maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kuwataka Mamlaka ya Mapato wawe marafiki wa walipakodi na hii ndiyo *feedback* ambayo tunaipata kutoka kwa wapigakura wetu wafanyabiashara kwamba kuna *improvement* kubwa hata kama hatujafika kabisa 100% tunakotaka kwenda, lakini kuna *improvement* kubwa sana ya namna ambavyo Mamlaka ya Mapato wana-*approach* walipakodi wetu.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuunga mkono hoja ya Wizara hii na hasa nilipozungumzia umuhimu wa ukusanyaji wa mapato na mapato yanaenda kufanya nini, sisi sote kama Wabunge kwa mfano mimi jimboni kwangu bado nina miradi ya maendeleo ambayo inahitaji fedha ili iweze kukamilika au kutekelezeka, bado nina barabara inayounganisha Mkoa wa Tabora inapitia jimboni kwangu Bukene mpaka kufika Mkoa wa Shinyanga, barabara hii inahitaji fedha iweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka kadhaa tumekuwa tukipata fedha kidogo sana, kwa hiyo, tunatengeneza kilometa chache sana. Sasa suluhisho lake ili tuweze kuitengeza

kwa haraka na kwa ukubwa ni tupate fedha na fedha zinatokana na makusanyo yanayosimamiwa na Wizara hii hususani kupitia taasisi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nina miradi ya afya; kuna vituo vya afya vinaendelea kujengwa. Leo hii tumepewa taarifa kwamba baadhi ya majimbo yamepata fedha za kwanza za miradi ya kimkakati ya vituo vya afya, lakini majimbo mengine wiki hii fedha zinaweza kuingia. Sasa fedha hizi ili zipatikane inabidi zikusanywe, ni lazima zikusanywe na Mamlaka ya Mapato chini ya Wizara ya Fedha ndiyo tuwe nazo ndiyo tuzipeleke huko kwenye vituo vya afya kwa sababu itabakia maneno na kwenye makaratasi tu bila kuwa na fedha.

Mheshimiwa Spika, nina miradi ya barabara, nina miradi ya maji ambayo yote hii inahitaji fedha. Kwa hiyo, kuna kila umuhimu wa Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hoja ya Wizara hii kwa sababu Wizara hii ndiyo inabuni na ndiyo inasimamia ukusanyaji wa mapato ili miradi yetu itekelezeke ili iende ikafanyike na isibakie tu maneno kwenye bajeti. Kwa hiyo, ndiyo umuhimu mkubwa wa Wizara hii wa kubuni vyanzo vya mapato na kusimamia ukusanywaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kushauri ambalo pia limetajwa kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri ni matumizi ya mifumo katika usimamizi wa malipo ya fedha za umma kwenye taasisi zetu. Haina ubishi kwamba matumizi ya mifumo yanaongeza ufanisi kwenye taratibu za malipo, makusanyo kwenye taasisi zetu, lakini tumeweka mifumo mizuri kama *MUSE* na mifumo mingine, lakini kwenye baadhi ya maeneo tuna tatizo kubwa la uwezo au ujuzi wa wale watumiaji wa mifumo.

Mheshimiwa Spika, kuwa na mfumo ni jambo moja, lakini uwezo wa wale watumiaji wa mfumo ni jambo lingine. Kwa hiyo, unaweza ukawa na mfumo mzuri, lakini watumishi wa umma ambao wanaopaswa kutumia hiyo mifumo wanapokuwa hawana uwezo stahiki ile mifumo haileti ile tija ambayo tulikuwa tunaitegemea.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya *scenario* kwenye halmashauri zetu huko fedha zinakuja za maendeleo, zinapaswa kwenda vijijini kutekeleza kazi fulani, lakini unakuta zinachelewa kwa sababu ya mifumo ya ulipaji na mifumo ya matumizi na wakati mwingine ukifuatilia unakuta ni uwezo wa mtumiaji wa mfumo tu, afisa aliyepo pale namna ya kutumia ule mfumo hana funzo, hana uwezo, hana nini kwa hiyo unakuta kwamba malipo yanachelewa miradi inachelewa kwa sababu tu ya mapungufu ya uwezo wa watumiaji wa mifumo.

Kwa hiyo, ninaunga mkono mojawapo ya vipaumbele vya Wizara ya Fedha kwamba kutoa mafunzo ya utumiaji wa mifumo kwa maafisa wetu wanaotumia mifumo ya malipo na matumizi katika maneo yao ya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa 100%, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, atafutiwa Mheshimiwa Juma Hamad Omar na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege ajiandae.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango wangu, lakini nikushukuru sana kwa kipindi chote nilichokuwa katika Bunge la Kumi na Mbili nimehudumu katika Kamati ya bajeti. Ninashukuru kwa kuniamini kwa kipindi chote, lakini ninakushukuru wewe kwa miongozo yako uliyoitoa katika Kamati yetu ambayo iliwezesha Kamati yetu kufikia matarajio yake ambayo yalipaswa sisi tuyafanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niunge mkono hoja iliyoko mbele yetu ya Wizara ya Fedha nikimpongeza Waziri, Mheshimiwa Mwigulu, Naibu Waziri - Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu, Watendaji wote na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri mlizozifanya kwa kipindi chote tulichokuwa katika Kamati yetu kwa kutupa ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano mzuri tuliokuwa nao katika Kamati yetu na kusababisha taarifa zetu za Kamati zimekuwa na tija kwa ajili ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi nzuri anazozifanya za kutuletea maendeleo pamoja na kutafuta fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa zimefanyika kupitia Wizara ya Fedha ambayo kazi yake ni kukusanya fedha na kutafuta fedha; na fedha nyingi zimetafutwa. Niipongeze *TRA* chini ya Kamishna wetu Yusuph Mwenda kwa kuvunja malengo kwa kila mwaka na kusababisha miradi mingi katika majimbo yetu kutekelezwa na hata miradi ya kimkakati ikiwemo Daraja la Kigongo – Busisi ambalo limejengwa kwa fedha za makusanyo ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa nipongeze Fungu Namba 23 limetekeleza kazi yake vizuri ikiwemo kuwasilisha michango ya kisheria kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wakati na hili limejidhihirisha katika Kamati yetu. Walituletea mchanganuo wa taarifa zote ikiwemo *PSSSF* pamoja na *NHIF* kwa jinsi walivyopeleka fedha bila kuchelewa. Pamoja na hayo lakini kumekuwa na changamoto ya ucheleweshaji wa uhuishaji wa michango ya watumishi na mwajiri kunakosababishwa na kutokusomana kwa Mfumo wa *MUSE* na mifumo ya malipo kwenye mifumo ya Hifadhi ya *PSSSF, ZSSF, NHIF* na *WCF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Mheshimiwa Rais alivyoomba mifumo yote iweze kusomana iweze kuleta tija kutokana na gharama ilivyotumia, lakini kuunganishwa na mifumo hii niliyoitaja itasababisha kuboresha utoaji huduma kwa watumishi pamoja na wastaafu, lakini katika fungu hili hili pia kuna kupungua kwa ari ya utendaji kazi kwa baadhi ya watumishi wa Hazina Ndogo ambako kuna kunachangiwa na uchakavu wa miundombinu pamoja na magari, lakini nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa mwaka huu unaokwisha mmejenga jengo zuri sana la Hazina Ndogo katika Mkoa wa Geita ambapo na mimi nilishiriki

kwenda kuzindua hilo jengo nikimuwakilisha Mwenyekiti wangu wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyokuwepo watumishi wa Mkoa wa Geita huduma hii walikuwa wanaipata Mkoa wa Mwanza, lakini nikuombe sasa kituo kinachofuata mtujengee jengo la Hazina Ndogo katika Mkoa wetu wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee Fungu Namba 45 ambalo ni la Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Fedha zimepelekwa vizuri, katika bajeti yetu hadi kufikia mwezi Aprili fedha zilipelekwa kwa 88% lakini pamoja na hayo kumekuwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo wakaguzi wote kwa mujibu wa viwango vya kimataifa, uhaba wa vitendea kazi ikiwemo vifaa vya kuwezesha ukaguzi wa kiufundi, lakini kuongezeka kwa maeneo ya ukaguzi ikiwemo ukaguzi wa wakati halisi *(real time audit)* na ukaguzi wa kiufundi na ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Wizara ya Fedha iliwatengea kwenye matumizi ya kawaida shilingi bilioni 80, lakini ilipeleka shilingi bilioni 70, sawa na 88% hadi kufikia mwezi Aprili. Hii kazi ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amekuwa akitoa ushirikiano na Ofisi ya *CAG* na kwa mwaka huu wa fedha kwenye mapato yale ya kawaida yasiyo ya mishahara wametengewa shilingi bilioni 87.3 kuna ongezeko la shilingi bilioni saba, niwapongeze sana, lakini fungu hili linahitaji kuendelea kuongezewa ukomo, tunajua mlizingatia ukomo katika mwaka huu ndio maana mmeongezea shilingi bilioni saba, lakini fungu hili lina kazi kubwa kama nilizoziainisha. Endapo kazi hizi zitatekelezwa tutapunguza ubadhirifu wa matumizi ya fedha katika miradi inayotekelezwa kama miradi hii itakaguliwa kwa wakati, kama kutakuwa na ukaguzi wa mabadiliko ya tabianchi, tutazuia vile vihatarishi ambavyo vingeweza kuweza kutokea na kuweza kunusuru fedha za kuweza kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze kwa kuiwezesha kimtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo ya Tanzania *(TADB)* ambayo jukumu lake la msingi ni kuongeza chachu katika utoaji wa mikopo ili kuweza kufanikisha maendeleo jumuishi ya sekta ya kilimo nchini na kuchangia Dira ya Taifa ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunajua zaidi ya 65% ya Watanzania ni wakulima na kazi kubwa imefanywa na benki hii toka ilipoanzishwa mwaka 2015 shilingi bilioni 971 zilinufaisha wakulima milioni 1.9 pamoja na biashara 686. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, biashara hizi zimeendelea kukopwa na kusaidia kurasimisha sekta zisizo rasmi katika wafanyabiashara ambapo itasaidia kuongeza wigo wa walipa kodi; lakini benki hii inakabiliwa na mtaji kwa sababu mtaji wake ni shilingi bilioni 924 na haipokei amana yoyote kama zilivyo benki za biashara. Hivyo, sasa niungane na maoni ya Kamati kwa kuhimiza ili iweze kutimiza dhamira yake, benki hii iweze kupewa mtaji wa jumla ya shilingi 2,900,000,000,000 ili tuwe na naksi ya shilingi 2,000,000,000. Tutaongeza wigo, tutawakopesha wavuvi pia katika sekta hii ya kilimo; tutawakopesha wafugaji ambao kundi hili bado limesahaulika katika sekta hii ya kilimo ambapo wafugaji wengi wapo wafanyabiashara ya mifugo ambao hawalipi kodi, tukiwapatia mikopo itawasaidia kuwarasimisha na kuongeza wigo wa ulipaji kodi. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge dada yangu Leah Komanya, kwanza mchango wake ni mzuri sana, lakini kupitia eneo hilo hilo la Benki ya Kilimo kwa

maana ya Serikali, kwa maana ya Wizara ya Fedha ilivyoongeza mtaji kwa Benki ya Kilimo. Nilidhani sasa iko haja ya Wizara hii kuona umuhimu wa kupeleka Benki hii ya Kilimo kwenye maeneo ambayo ni wazalishaji wakubwa hususan Mkoa wa Ruvuma ambako tumekuwa wazalishaji, tumeongeza kwa miongo mitano kwa uzalishaji wa mazao ya nafaka nchini Tanzania. Kwa hiyo, itasaidia kuendelea kukuza sekta hii ya kilimo na wakopaji ambao ni wakulima watakopa kwa ukaribu na kwa kufanya uwekezaji wenye tija zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Leah Komanya unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa hii na naweka msisitizo pia kwa kuwezesha wakulima hawa, tutaongeza fedha za kigeni ambapo mazao yatapelekwa nje na kupata fedha za kigeni pia na kuongeza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Hamad Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege, Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni ajiandae.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nitumie fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu. Wewe umekuwa ni Mheshimiwa Spika wa viwango na siku zote nakuwa nakuambia katika nyumba hii wewe ni *dictionary* wa Kanuni za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu uzoefu huo ulionao ndio maana Umoja wa Mabunge Duniani wakakuteua kama Rais wao. Chonde chonde wananchi wa Uyole tunawaombeni kwa heshima na taadhima mturejeshee Spika huyu au mturejeshee Mbunge huyu ili tuweze kumpa tena Uspika na *Inshallah* aendelee tena na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka nitumie fursa hii kumpongeza sana Waziri na pacha wake na Naibu Waziri. Mimi nilibahatika kufanya kazi ya Naibu Waziri katika kipindi cha Mzee

Ruksa na nilitumika miaka saba niko pale kutoka 1985 mpaka 1992. Nimefanya kazi na Mawaziri watatu wa Fedha, wa kwanza kabisa alikuwa ni Mheshimiwa Cleopa David Msuya ambaye kwa heshima zote amezikwa hivi karibuni na wananchi wake wa Mwanga na Serikali. Waziri wa pili alikuwa Mheshimiwa Stephen Kibona aliyekuwa Mbunge wa Ileje, yeye kwa kweli Mungu amjalie mahala pema peponi, alifariki wakati yuko anaitetea Tanzania katika mikutano wa fedha ya *World Bank* na *IMF,* tukapokea maiti hapa.

Mheshimiwa Spika, wa tatu nilifanya kazi na marehemu Profesa Kighoma Malima. Kwa hiyo, nina uzoefu sana wa kufanya kazi katika Wizara hii kama Naibu. Nafikiri kama kuna Manaibu Waziri *the longest sub* ni mimi hakuna mwingine na baada ya hapo nilipata nafasi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba siku zote Mawaziri wa Fedha na wataalam wao wanakuwa *very conservative* yaani wanakuwa ni watu si roho mbaya, lakini ni watu wana misimamo yao, akishashika msimamo huwezi kumpinda tofauti na Waziri Mwigulu na Mheshimiwa Naibu Waziri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Mwigulu tumeona ni daktari unampinda, unamshauri anashaurika. Nafikiri kama sikosei 80% ya mapendekezo ya *Finance Bill* (Sheria ya Fedha) ya mwaka 2024/2025 aliyachukua na ndiyo maana yake tumekwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawaomba jamani na naomba chonde chonde wananchi wa Singida Mashariki na wananchi wa Kojani kule Pemba wawachague tena Mawaziri hawa ili waweze kuwa Wabunge na *Inshallah* pengine Mwenyezi Mungu atawajalia tena kuwa Waziri na Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu na kumpongeza kwa kuwa na uono wa kuwachagua hawa watu wawili, lakini na yeye pia kwa kuwa na uono mkubwa, maana hawa ni washauri wake, lakini *ultimately*

yeye ndiyo anayekata shauri. Kila Mbunge hapa ni shahidi katika jimbo lake jinsi ya *landmarks, landmark* maana yake ya jinsi ya mambo aliyofanya Mheshimiwa Rais. Ukienda kule Singida Magharibi yapo, ukija Pemba kule Ole yapo, ukienda Iramba yapo, ukienda Ole yapo, ukienda Kojani yapo, ukienda kwa rafiki yangu hapa Ally Kassinge yapo jimboni kwake. Kwa hiyo, kila Mbunge hapa ni shahidi wa matokeo ya maendeleo aliyoleta Mheshimiwa Rais, nasema Mungu amjalie miaka mitano tena na *Inshallah* basi aendelee *pace* na *speed* hii hii ili nchi hii iwe kabisa ni nchi ambayo imepiga hatua sana kimaendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka nizungumze mambo mawili; moja suala la pensheni ambayo inalipa Wizara hii. Kuna kipindi kile cha awamu ya kwanza alichotawala Baba yetu Hayati Mwalimu Nyerere; kuna kipindi cha awamu ya pili alichotawala Mzee Rukwa, kipindi hiki ni mishahara ilikuwa ni midogo sana. Mimi nakumbuka nikiwa Naibu Waziri mwaka 1987 kama sikosei nilileta azimio hapa la kupandisha mshahara wa Rais, maana wakati huo ilikuwa mshahara wa Rais unazungumzwa hapa hapa Bungeni na unapandishwa hapa.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka tukampandisha Mzee Ruksa mshahara wake sasa sikilizeni vizuri hapo, tukampandisha Mzee Ruksa mshahara wake kutoka nafikiri shilingi 30,000 mpaka ikafika shilingi 50,000. Sisi wengine huku mishahara yetu ilikuwa shilingi 20,000 mpaka shilingi 30,000. Pensheni ya mwisho au ile pensheni ya kila mwezi wakati huo inategemea na mshahara wa mwisho. Sasa kama mshahara wa mwisho ni mdogo ina maana pia pensheni yako ya kila mwezi inakuwa ndogo. Sasa kilichotokea baada ya kustaafu Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Pili akaja Mheshimiwa Mkapa ikaanza kupanda mishahara ya wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, leo hii wale watu waliofanya kazi katika awamu hizo mbili, awamu ya kwanza na awamu ya pili huwezi kuamini pensheni yao wanayochukua kila mwezi ni chini ya kima cha chini. Sijui kama inaeleweka hapo, ni chini ya kima. Mimi ni mmojawapo nakwenda kuchukua pensheni ya kila mwezi, sitaki

kusema hapa lakini ni chini ya kima cha chini napata shilingi 140,000.

Mheshimiwa Spika, kuna wanajeshi wengine huko makanali na wale waliopigana vita wanapata chini ya shilingi 120,000. Sasa mtu anayetoka Makunduchi akaja kuchukua pensheni ya shilingi 120,000 nadhani hiyo ni nauli yake tu; lakini Mawaziri waliostaafu hivi karibuni baada ya kipindi cha Mheshimiwa Rais Mkapa wanapata. Sasa ninaloshauri hapa, nadhani najua mnalifanyia kazi huko nchi nyingine pensheni wana-*index as per cost of living,* hali ya maisha inapobadilika na *inflation* inapobadilika pensheni wanairekebisha. Kwa vyovyote isiwe chini ya kima cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu mzee, huyu mwanajeshi aliyefanya kazi *in the spirit of perfection and dedication* katika hali ya kutekeleza mambo yake kiuadilifu na kwa ukamilifu mnampa pensheni hiyo, jamani tufike mahala hili tulirekebishe.

Mheshimiwa Spika, la pili nitakalochangia ni suala la deni. Kwanza, nashukuru sana kwamba deni letu ni himilivu, tuna uwezo sasa wa kulipa deni la nje na deni la ndani, hatuna wasiwasi na kwa nini tulikopa? Tulikopa kwa sababu ni wazi kwamba idadi ya watu inaongezeka katika nchi hii, tunazungumzia milioni 60, nafikiri katika mwaka 2050 tutakuwa karibu watu milioni 100. Kwa hiyo, mahitaji yanaongezeka, mahitaji ya kujenga miundombinu yanaongezeka, mahitaji ya hospitali, mahitaji ya shule, mahitaji ya kila kitu yanaongezeka. Kwa hiyo, lazima tukope, haina matatizo lakini msishangae kwamba sisi tunakopa kidogo na deni letu ni himilivu kuliko nchi nyingine hizo tunazoita nchi za matajiri.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mifano hapa, kwa mfano Japan ni nchi ya viwanda, lakini ukichukua uwiano wa deni na pato la Taifa. Japan wanazungumza 266.2%; Marekani uwiano wa deni na Pato la Taifa unazungumzia 107.6%; inafuatia Ufaransa 115.7%. Sasa kwa maana ya sisi kukopa tumekopa kidogo sana ukija katika uhusiano huo. Katika Kusini mwa Janga la Sahara, Tanzania ni moja katika nchi ambayo haijakopa sana

ukilinganisha na wenzetu. Uwiano wetu wa deni *vs* Pato la Taifa ni kama sikosei 39%, sasa hiyo ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, na katika yale makundi manake hawa wanaokopa madeni unaweza ukawaweka makundi manne. Moja kundi lenye lililokuwa halina mzigo mkubwa ni nchi ya Botswana peke yake, lakini ya pili ni nchi ambazo ina mzigo hafifu wa deni hii ni pamoja na Tanzania. Kundi la tatu ni nchi zenye deni kubwa lina mzigo mkubwa, deni ni kubwa kidogo, hii ziko nchi kama 16. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna nchi ambayo imedhoofu lahali yaani lile deni tena limefika mahala limewaelemea mpaka linawaumiza, mpaka wanaokopesha wanafika mahali wanasema mamlaka ya kukusanya kodi na sisi tuiendeshe sisi ili tupate kukata deni letu, ziko nchi za namna hiyo. Mimi sitaki kuzitaja hapa kwa sababu ni nchi ambazo ni jirani zetu. Nitataja kidogo kwa mfano, Malawi, Zambia, Zimbabwe hizo ni nchi zenye mzigo mkubwa sana sisi hatumo katika hao. Kwa hiyo, nasema bado deni letu ni himilivu na kwamba tumekopa kwa ajili ya mahitaji yetu na pamoja kuongeza uchumi wetu. Sasa nasema hilo ni jambo la busara.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nitumie nafasi hii kuiunga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha, lakini Waziri wa Fedha asingefika mahali hapa kama si msaada mkubwa au kama si maono makubwa ya Mheshimiwa Mtukufu Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge ili tuwarahisishie watu wanaofuatilia kumbukumbu zetu, mchangiaji amemtaja Rais wa Awamu ya Pili kwa kutumia jina lake lingine lile la Mzee wa Ruksa, lakini alikuwa ni Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Josephat Simkamba Kandege atafuatiwa na Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi niwe miongoni mwa wachangiaji wa leo.

Kwanza, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kunijalia afya ya kuweza kusimama na kuweza kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya katika kuhakikisha kwamba pamoja na misukosuko ambayo dunia imepitia, lakini Tanzania imeendelea kuwa imara katika sekta ya uchumi. Naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu wote hakika Wizara imepata watendaji ambao wamekuwa msaada mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, na mimi ni miongoni mwa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti, naipongeza Wizara kwa sababu wamekuwa wasikivu sana. Michango mingi ambayo imetolewa na Kamati yetu ya Bajeti wameisikiliza na ushauri wamepokea na kwenda kufanyia kazi, hivyo nina kila sababu ya kuwapongeza.

Mheshimiwa Spika, mimi ninaomba nijikite katika Fungu 21 - Hazina na najikita katika fungu hili kwa sababu ndio waliokuwa na jukumu la kusimamia sera za fedha hapa nchini Tanzania. Kwa hiyo, wana wajibu wa kuhakikisha kwamba masuala yote ya sera yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo naomba nijikite ni juu ya matumizi ya fedha taslimu. Huu umekuwa ni wimbo ambao tumekuwa tukiusema mara nyingi na Mheshimiwa Rais naye amekuwa akielekeza kwamba, sisi kama Taifa lazima ifike wakati ambao tuondokane na matumizi ya fedha taslim au tuanze kwa kupunguza. Kwa hiyo, naomba niungane na mchango ambao tumeutoa kama Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ninyi mmekuwa mkitembea duniani. Ukienda katika nchi za wenzetu, ukisema unatoa dola 1000, 2000, watu wanakushangaa za nini hizo? Lazima twende ambavyo dunia inataka twende, lakini kubwa kwa nini watu wetu hawapendi kutumia malipo kwa njia ya kieletroniki, ni kwa sababu gharama ni kubwa. Pale ambapo unafanya *transaction* ukija ukafatilia gharama ambazo zinatozwa ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gharama ni kubwa pale ambapo unafanya *transaction* ukija ukafuatilia gharama ambazo zinatozwa ni kubwa sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali wahakikishe kwamba wanafanya mapitio ili gharama za kulipa kwa kutumia njia za mtandao zinashuka na niukweli usiyopingika kama ukipata nafasi ukienda kuomba *bank statement* kama umekuwa uki-*transact* kwa kutumia miamala hii umemtumia mtu, mara umepokea ukianza kupitia zile *charges* ambazo unatozwa ni nyingi sana na ndiyo maana mtu akiona kama anataka kutuma fedha analinganisha je, niite *bolt* au nichukue bodaboda nimpelekee mtu *cash* kulikoni gharama ambazo natozwa kwa kutuma kwa kutumia mitandao ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali gharama juu ya matumizi ya fedha taslimu ziko wazi la kwanza hii inasaidia wale watu ambao wanataka kukwepa kodi kwa kutumia pesa taslimu, lakini pia hata mtu ambaye anataka kutoa rushwa ni rahisi kwa kutumia pesa taslimu.

Mheshimiwa Spika, kwa mtu ambaye anataka kutakatisha fedha kama ambavyo Taifa tulikuwa na changamoto kubwa sana naomba tusirudi huko, lakini hata mtu anapotaka kumuibia mwenzake atamwibia fedha ambayo ni taslimu katika hali ya kawaida kwa utumaji kwa kutumia mitandao siyo rahisi inadhibiti wizi. Kwa hiyo, niiombe Serikali kubwa zaidi tuhakikishe kwamba gharama zinapungua ili watu wetu wahamasike kutumia *cashless* badala ya kwenda kutumia hii habari ya noti na gharama zingine ziko wazi.

Mheshimiwa Spika, ukiwa na noti ku-*print* ni gharama siyo kwamba zinatolewa bure ni gharama, lakini hata utunzaji wa noti na sarafu nao ni gharama. Inafikia kipindi Benki Kuu wanalazimika kuchapisha fedha zingine kwa sababu ambazo ziko kwenye mzunguko zimechakaa. Kwa hiyo, niiombe Serikali tuhakikishe kwamba kama taifa ukienda kwa majirani siyo vizuri kutaja ukipanda hata *taxi* unavyotaka kulipa *cash* anakwambia nikupe *pin* uweze kulipia, hayo tuyaige mambo mazuri. Ukiona mwenzako anafanya vizuri hakuna ubaya kuiga hayo mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba nishauri ni upande wa *BOT*. Wamekuja vizuri sana kuhakikisha kwamba kama Taifa hii habari ya *dollarization* tunaondokana nayo, lakini kuna sehemu ambayo naamini watalamu ni vizuri wakaenda kuchakata, wakaja na suluhu ambayo itakuwa inasaidia sisi kama Taifa. Ukisema kwa *service* ambazo natoa nje ya nchi halafu nataka u-*quote* kwa shilingi duniani hawatuelewi yaani unampata mtalii anafanya *booking* huko Marekani unamtumia kwamba shilingi ndiyo ambayo itumike kama *quotation* hawatuelewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama taifa tunahitaji dola kwa sababu siyo kwamba vitu vyote tunazalisha hapa nchini kwa hiyo uwepo utaratibu madhubuti wa kuhakikisha kwamba dola hizo zinaingia Serikalini tusijetukalazimika ku-*create black market*. Kwa sababu tunalazimisha watu kwamba lazima alete shilingi jambo hilo halipo dunia ya hivyo haipo.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya sana mnawaambia watu ambao wanashughulika na utalii mna-*quote exchange rate* ambayo inatolewa na *BOT*. Wakati ukienda kwenye mabenki yetu, ukienda kwenye *bureau* zetu hakuna hata sehemu moja ambapo utakuta *quotation* ambayo iko ya Benki Kuu ndiyo ambayo inatumika. Sasa tafsiri yake ni nini? Tunalazimisha *black market*.

Mheshimiwa Spika, mtu anachukua fedha, anaenda ku-*change* vichochoroni, halafu kwa sababu wewe ume-*quote*

kwenye bei ya *exchange rate* ya *BOT,* maana yake kama Serikali mnapata hasara na hasa taasisi za Serikali kama *TANAPA* kwa sababu mnacho-*quote* ni kile ambacho hakipo duniani.

Kwa hiyo, hakuna sababu ya kuhakikisha taasisi za Serikali zinapata hasara kwa barua au waraka ambao umetolewa na Benki Kuu *in blanket,* hakuna jambo ambalo linaweza likawa moja lika-*fit* yote *(one size fix all)* haipo. Kwa hiyo, naomba kama Serikali mlichakate hili ili muone kama taifa tunahitaji dola, isijeikawa kwamba waraka mmoja unasaidia kwa watu wote.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo naomba nitoe mchango, naomba niipongeze Serikali, Waziri wa Fedha umekuwa msikivu sana juu ya uanzishaji wa *tax ombudsman,* lakini bila kuwa na sheria ambayo itasababisha akafanye kazi zake itakuwa ni kama tumeanzisha taasisi ambayo haisadii lolote. Ni vizuri upitie mchakato muitazame sheria ile ili iwe na manufaa juu ya uanzishaji wa ofisi hii, vinginevyo itakuwa haitusaidii kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, jambo jema pale ambapo anayelalamikia suala la kodi au analalamikia jinsi ambavyo labda hakutendewa haki awe na sehemu ambayo anaiamini kwamba nikipeleka malalamiko yangu nitasikilizwa na haki itatendeka kabla ya kwenda kwenye rufaa za kodi na taasisi zingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo naomba niunge mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemus Henry Maganga na Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kabla sijasema sana naomba nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo ameifanya nchi yetu iendelee kukua kiuchumi, lakini iendelee kuwa na uimara wa pesa za kigeni na tuendelee kuwa

na nchi ambayo inakopesheka na inayoweza kufanya miradi yake yenyewe. Kwa hiyo Mheshimiwa Rais pongezi za watu wa Sumve zikufikie moja kwa moja.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini naomba nisiwe mchoyo wa fadhila nimpongeze sana kaka yangu Mheshimiwa Mwigulu kwa namna ambavyo anasimamia Wizara hii na namna ambavyo amejitahidi kwa kazi kubwa aliyoifanya katika muda huu ambapo amekuwa Waziri wetu wa Fedha, lakini pia Naibu wake, ndugu yangu Mheshimiwa Chande kwa namna ambavyo umekuwa mtu mwema, umekuwa msaidizi mwema kwa Mheshimiwa Waziri na wakati mwingine mtu anaweza akakuona wewe akaona kama amemuona Waziri vile, amekuwa anafanyakazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo naomba sasa nijielekeze kwenye hoja yangu ya msingi. Unapokuwa Waziri wa Fedha unajua fedha, Wizara ya Fedha kwa dunia ya sasa pesa ni kila kitu yaani unahusika na maisha ya watu moja kwa moja na ili Serikali ipate pesa ni lazima ikusanye ushuru, hakuna pesa inapatikana nje ya utaratibu huo lazima tukusanye ushuru ili tuwe tuna pesa ya heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunazo sababu za msingi kabisa za kuhakikisha Mamlaka yetu ya Mapato *(TRA)* inaendelea kuimarishwa, inaendelea kufanya kazi vizuri ili Serikali yetu iweze kupata pesa ya kuendesha miradi ya maendeleo. Kwa kusema hayo naomba kwa sasa nimeangalia ripoti ya *TRA* ya robo ya mwezi wa kwanza mpaka Machi, wameongeza kiasi cha ukusanyaji wa mapato, lakini kiasi cha ukusanyaji wa mapato kimeongezeka kwa miezi tisa mfululizo yaani tumekusanya huu mwezi wa kwanza mpaka wa tatu zaidi ya trilioni saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo inavyoonekana Mamlaka yetu ya Mapato inafanya kazi vizuri mpaka sasa, ongezeko la ukusanyaji wa pesa ni heshima kwa nchi yetu, lakini ni nafuu kwa Watanzania wote na kwa nafasi hiyo naomba nimpongeze Kamishna wa *TRA*, Ndugu Mwenda kwa namna ambavyo ameifanya Mamlaka hii ya Mapato kwa muda mfupi kuendelea kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato imefanya vizuri muda mwingi tangu Mheshimiwa Rais aiingie madarakani kila mara makusanyo yanapanda, lakini sasa yamepanda zaidi na zaidi kwa hiyo hongereni sana Mamlaka ya Mapato, lakini ipo kazi kubwa tunatakiwa kuendelea kuifanya, tunatakiwa tuongeze wigo wa walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado Watanzania wanaolipa kodi mbali na kwamba idadi ya mapato yanaongezeka wanaolipa kodi bado ni wachache sana. Kuna kazi kubwa ya kufanya kwenye Mamlaka yetu ya Mapato, ipo sababu ya watumishi wetu wa Mamlaka ya Mapato kuendelea kupata msasa na ushauri wa namna bora ya kuifanya nchi yetu ikusanye mapato zaidi na zaidi. Haiwezekani sisi na ukuaji wetu wa uchumi huu tuendelee kuwa na mapato ya shilingi trilioni 20 ngapi tunatakiwa kuwa mapato makubwa zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mamlaka yetu ya Mapato inatakiwa iwekeze zaidi kwenye kukuza wigo wa mapato, lakini ipo kazi kubwa tunatakiwa kuifanya, kuna kitu mimi kwa uzoefu nimekiona, mimi nafanyakazi ya biashara biashara kidogo.

*Kuna hawa watu sijui tusemeje kidiplomasia, lakini tuna wafanyabiashara wengi kutoka nje ya nchi, wengi wao wamejaa kwenye biashara zetu, kwenye mzunguko wetu wa biashara wanatoka Bara la Asia na hawa watu tunawaita Wachina wapo sana kwenye biashara zetu na ni wajasiriamali wazuri wameingia kwenye biashara, wako aggressive, wanafanyabiashara. (Makofi)*
**[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, ni kwa ushauri tu kwa Wizara ya Fedha na *TRA* kwa uzoefu wangu mdogo na tunayoyasikia ni wazoefu sana kwenye kukopa kodi, mna kazi kubwa sana ya kufanya. Yaani kutoa risiti na kulipa kwenye akaunti ni ugomvi mkubwa, yaani unapomwambia naomba akaunti nilipe atajitahidi akushawishi alipwe *cash* lakini unapomuomba risiti atakupa mpaka elimu kwa nini uchukue na kwa nini usichukue? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yaani inafika wakati anakwambia nikikupa risiti nitakuuzia shilingi 200,000 nisipokupa risiti tutatoa hii ya *TRA* nitakupa ukaenayo wewe, kwa hiyo, mimi utanipa tu nisikupe risiti. Sasa hii elimu ya ujasiri wa kukwepa kodi Watanzania tulikuwa hatuna, tunaanza kupandikizwa elimu ya ujasiri wa kukwepa kodi na kujua kwamba hii 18% nikiipeleka *TRA* yaani wewe hutaishika, lakini mimi sasa hivi nikupe kwa laki na nusu hii 18% yako ubakinayo kila mmoja aendelee na maisha yake unipe *cash*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nini tunapaswa kufanya kama nchi ili kuboresha ukusanyaji wa mapato? Lazima tutoke, kuna mchangiaji ametushauri hapa tutoke kwenye *cash economy,* ni lazima tutoke huko kama kweli tuko *serious* na tunataka tuweze kukusanya mapato vizuri na Taifa liendelee mbele, lazima tutoke mtu anahesimika kwa sababu ana *cash* hii ni imeishakuwa ni ushamba, lazima tutoke kwenye *cash economy*, ni lazima malipo mengi yafanyike kwa utaratibu wa kieletroniki, tutafanya hivyo kwa kuimarisha mifumo yetu ya malipo, ni lazima tuimarishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ifikie wakati mtu awe na uwakika kwa sababu ukienda hata kwenye hoteli unakula, umemaliza kula nalipa ukisema tu nalipa kwa simu unaona yule muhudumu amebadirika sura yaani kila mmoja anata alipwe *cash*. Naomba risiti unaona mtu anarudi nyuma wakati mwingine hata alikuwa ana kitu anakwambia hana. Sasa hiyo elimu kwa wafanyabiashara lazima iende, elimu kwa Watanzania lazima iende, elimu kwa watumishi wetu wa Mamlaka ya Mapato lazima iende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumie muda mwingi pia kuwaelimisha watu wanaolipa kodi, wafahamu umuhimu wa kulipa kodi, lakini wafahamu pia umuhimu wa kutoka kwenye hizi njia za *cash*. Watu wengi wanakimbilia huko kama mzungumzaji alivyosema Mheshimiwa Kandege, kwamba makato yanakuwa mengi, lazima tuweke makato rafiki ili kila mmoja awe salama, hakuna mtu anapenda kutembea na mahela, unatembea umebeba

hela una hela una *wallet* yale mambo ya kizamani, sijui *wallet* imetuna hivi ni mambo hayo yanatakiwa yatoke huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwe tuna pesa kwenye simu zetu pesa kwenye kadi zetu unakoenda kokote unalipa unapata risiti, nchi inapata pesa tukipunguza makato karibu kila mtu atatumia huo utaratibu. Kuna wakati tunafanya biashara sisi unakuta bandarini kuna wakati unashindwa kupeleka mzigo mtandao umegoma, hii haitakiwi kuwepo lazima mitandao yote ya kupokea mapato, mitandao yote ya kupokea mizigo ihakikishe inakuwa imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini mabenki yanakuwa muda wote wenyewe hawatuambii kwamba unapeleka hela wanakwambia mtandao haupo au mfumo kwa nini tusijifunze huko wao wanafanya nini? Yaani kwa nini mitandao yao ni imara? Mamlaka yetu ya Mapato ndiyo baba wa nchi hii, ndiyo mama wa nchi hii, anakusanya pesa sisi twende mbele, tumuhimarishe, tuhimarishe watoza ushukuru wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua hakuna jamii inapenda watoza ushukuru, lakini ili muishi lazima awepo mtu awasaidie kutoza ushuru, atoze ushuru, watu hawapende kulipa ushuru, lakini watozwe ili nchi iende, lakini ili nchi iende watu walipe kodi lazima tuweke mifumo rafiki ya ulipaji kodi na ili tuweze kupambana na uchumi wa dunia ya sasa tupambane na wale wanaitwa wakati mwingine mabeberu, tupambane na masharti magumu kutoka nje ya nchi yetu ni lazima tujitosheleze wenyewe. Watanzania lazima tuwe na morali ya kujitosheleza wenyewe tuwe matajiri wenyewe, tutumie pesa zetu wenyewe sasa ili tuzitumie lazima tuzikusanye vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na mambo hayo limezungumzwa suala hapa la wastaafu na nadhani mzungumzaji ameshauri vizuri sana. Serikali yetu mbali na kwamba tunafanya vizuri kwenye maslahi ya watumishi na tunaboresha mifumo yetu lazima hili tuliangalie suala la wastaafu, kwenye suala la pensheni *message* tunazo nyingi sana. Hata mimi nilivyokuwa hapa tu kuna mstaafu

mwingine kutoka Jimboni kwangu kanitumia *message* tusemee pensheni yetu bado iko chini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wastaafu ni wachache sana, wazee wetu hawa ambao wamefanyakazi kubwa ni lazima tuone namna gani sera zetu za pesa, sera zetu za nchi zinawaangalia na kuwafanya kwamba ustaafu au kustaafu isiwe ni tatizo; kustaafu iwe ni heshima ili kila mmoja ataniwe kustaafu kwa sababu anajua nikistaafu napumzika kazi maisha yanaendelea kuwa mazuri, isije ikatokea kwamba mtu anajua nikistaafu naenda kwenye mateso basi mtu ajitahidi asistaafu wakati mwingine aongeze hata umri, wakati mwingine awe king'ang'anizi kwenye jambo fulani, nadhani hiyo Mheshimiwa Waziri na timu yako nakupitia Wizara nyingine najua siyo la Wizara yako tu moja mnaweza kulifanya kwa uzuri na kufanya nchi yetu iendelee kuwa bora na Watanzania tuishi kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba uniruhusu niunge mkono bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kasalali umesema mwenyewe, lakini nikajua utajiambia wewe mwenyewe, naona wewe mwenyewe tena ukaenda ukapinda kwa mbele. Umewataja hapo watu kutoka Asia halafu ukawataja wengine maalum na ukaonesha kama wao wanawafundisha ujasiri Watanzania wa kukwepa kulipa kodi. Sasa wacha nikupe nafasi uyaondoe ni kukwepa tu awe Mtanzania awe mwingine wote ni kukwepa ili tusiingie huo mkanganyiko wa kuanza kutafutana kidiplomasia. *(Makofi)*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba maneno hayo yaondolewe kwenye *Hansard.* *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, atafuatiwa na Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hii Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu, muumba wa mbingu na nchi kwanza kupata nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu ambayo kila mtu hapa ndani anaitegemea, ukweli ni kwamba bila Wizara hii yaani huwezi ukafanya chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameonesha kuwa Rais wa pekee mpiganaji na kila mmoja hapa tumekuwa tukiulizana mambo ya wilayani yanaenda vizuri kwa maana ya kwamba mama amesimama imara kuhakikisha kwamba anaipigania nchi yetu na kutupambanania kuhakikisha kwamba Taifa letu linapiga hatua.

Mheshimiwa Spika, tatu nikushukuru Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Waziri wa Fedha, ukweli ni kwamba mnajitahidi kadri ya uwezo na Mungu aendelee tu kuwapa uwezo na fikra za mbali zaidi ili kusudi tuweze kuenenda na mambo yanayotakiwa kwenye ulimwengu wa sasa wa kidigitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru wananchi wangu wa Mbogwe ambao ndiyo wamenituma hapa niweze kusimama ndani ya Bunge lako kuwasilisha mawazo yao, lakini pia kuchangia hii hotuba ya Wizara ya Fedha, maana kila kitu tunahitaji pesa kwa hiyo kikubwa hapa kwanza Waziri naomba unikubalie ni kweli kwamba watu wengi hawalipi kodi, ukiangalia vizuri kiuhalisia watu wengi kweli hawalipi kodi, wanakwepa sana, wafanyabiashara wadogo na wakubwa hasa maeneo ya mjini, Kariakoo huko unakuta mtu anafanyabiashara na kama alivyopita huyu mzungumzaji anakupa na elimu kabisa nikikupa risiti nitakuuzia shilingi milioni mbili ila nisipokupa risiti nitakuuzia shilingi milioni 1.5.

Mheshhimiwa Spika, Waziri kwa hiyo wewe ndiyo refa wa hii Wizara, ukisimama vizuri wewe na vyombo vyako hakika tutapita hapa tunapopafikiria kwenye shilingi trilioni 50, lakini ukisimama legelege wanasemaga yaani mtu ukiwa legelege na mambo yataenda legelege tu, kwa hiyo, kuna kila sababu taratibu na miongozo mnayoitengeneza kwenye Wizara hii lazima iwe na

makali kidogo kwa sababu suala la kulipa yaani kutumia ni rahisi, lakini kulipa yaani ni kazi ngumu sana, lakini kwa vile hata kwenye maandiko matakatifu hili limo kwamba kulipa kodi ni muhimu kwa vile hata kwenye maandiko matakatifu hili limo kwamba kulipa kodi ni muhimu kwa sababu watu tunataka maendeleo na hatuwezi kupata maendeleo kiukweli bila kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna kila sababu Waziri kuangalia kwamba ni utaratibu upi utumie kusudi watu na Watanzania wote tulipe kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi nimpongeze kaka yangu Dkt. Doto Mashaka Biteko, wakati anaingia kwenye Wizara ya Madini, ulipaji wa kodi ulikuwa chini sana, lakini alikaa kama Waziri akatengeneza timu na mpaka sasa hivi kwenye madini huko na mimi ni-*declare interest* ni mfanyabiashara wa madini, tunalipa haki wote sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna dhambi kujifunza kwa Biteko kwamba yeye alifanyaje akafanikisha vipi (kutoa mapato yaliyokuwa yanakusanywa kwenye dhahabu mapaka kufika mpaka sasa hivi pale tulipo). Ina maana alitengeneza miongozo lakini ikiwemo na kukaa na wafanyabiashara kwamba nini na nini tufanye, ili kusudi tuache kukwepa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna kila sababu Waziri pamoja na Naibu wako na watendaji wote kwa sababu wapo hapa mbali ninaongea nikiwa ninajua vyombo vyote vipo hapa. Kuna kila sababu kila mtu kwenye eneo lake kukaa na wafanyabiashara, mkoa ama wilaya akawauliza wafanyabiashara hawa wa ndani ni nini ambacho kinachowafanya wakwepe kodi na wao wanazo sababu za msingi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, Waziri ninaomba nikushauri, wewe ni msimamizi wa benki. Hii biashara sasa hivi tunafanya na mataifa mbalimbali kwenye nchi zetu *(East Africa Community)* biashara tunafanya kwa pamoja. Unakuta mwenzio amechukua benki ile ile amefanyiwa 8%. Wewe huyo wa Dodoma hapo ama Mbongwe umepewa 22%, sasa vita inaanzia pale. Bahati mbaya

zaidi sisi wafanyabiashara huwa hatufichani. Tukikaa kwenye dawati la biashara lazima uulize wewe meneja amekupa mkopo wa riba gani. Sasa vita inaanzia hapo wenzako ana 8% wewe una 22%. Hapo kwanza unaanza kujisikia vibaya, hapo tu kwenye *butcher* wewe aumeshapunjwa 12%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna kila sababu ya kuanza kutengeneza mifumo kwa vile mimi wananiona hawa ni wa nini, acha tuanze sasa kukwepana, lakini lazima tujifunze kwa wale waliotutangulia. Kwa mfano, kwenye mafuta, Wizara ya mafuta sisi tuna mashine za *EFD*. Sasa hivi huwezi ukatoa mafuta bila risiti. Sasa ni kazi kwenu Wizara hii na ninyi kutengeneza *performance* ya kuangalia ni jinsi gani kwenye sabuni huku, kwenye maduka mtumie mifumo gani kama walivyotu-*tight* sisi wauza mafuta hata kama ukiwa unafaulisha ina maana unalipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kawaida sana Mheshimiwa Waziri kuna kila sababu hata ya kukaa na wafanyabiashara a kuwawekea mifumo kama hizi ni kamera, ili bidhaa zinapokuwa zinauzwa zinaonekana kwamba *stock* mteja amechukua boksi ngapi za sabuni ama nguo ngapi. Huo ni ushauri wa kwanza, kwa sababu tunaweza tukaongea maneno mengi sana kama hatuna fedha ki ukweli hatuwezi kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri unakumbuka nilikuuuliza swali mwaka 2023 kwamba ni kwa nini sisi Shilingi yetu haipandi? Sasa huu ni wakati muafaka pamoja na kwamba mnafanya vizuri zaidi, lakini niwakumbushe tu Wizara hii kuna kila sababu kufikiria kama wachumi na wasomi wetu Wizara ya Fedha, tutumie mifumo ipi ili kuendana na wenzetu majirani?

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi huwa ninaumia sana, mimi ninafanya biashara sana. Ukitoka Rusumo tu ukiingia Rwanda kama una shilingi milioni 100 yako uka-*change* faranga za Rwanda yaani unabakiza mfuko mdogo tu. Sasa unafikiria kwa nini sisi tunafanyiwa vitu kama hivi? Pia hata ukiondoka hapa ukaenda na shilingi milioni 100 ukifika tu Kenya mpakani uka-*change* fedha zako hata kama usiponunua kwenda na kurudi tayari unakuwa umeshakula hasara. Kwa hiyo, kuna kila sababu

hapo Mheshimiwa Waziri na Ienyewe kuliangalia ili kusudi muweze kupandisha shilingi yetu na uchumi wetu uweze kupanda kidogo. Tukipandisha uchumi ina maana vitu vyote vinashuka chini. Madeni tunakuwa nayo uwezo wa kuyashusha chini, vilevile kila kitu vitakaa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri hapa ambalo ninapenda nikushukuru nikukumbushe ulinipatia akili mwaka 2022 na mpaka sasa hivi wilaya yangu inajitegemea. Walimu zamani walikuwa wanafuata mishahara Bukombe, sasa hivi wanapata hapohapo Masumbwe. Wameniomba Halmashauri ya Mbogwe inahitaji tena ofisi nyingine pamoja na matawi ya benki kwa maana *NMB* na *CRDB.* Makao Makuu ya Mbongwe kutoka Masumbwe Mjini kwenda Mbogwe ni kilometa zaidi ya 50. Kwa hiyo, mwalimu atoke Ikungwigazi pamoja na Ngemo akiwa anafuata mshahara tu inam-*cost*.

Kwa hiyo, ninaomba uniweke kwenye bajeti yako hii tena matawi ya benki yaweze kuongezwa makao makuu ya wilaya yangu, ili kusudi wananchi waliopo maeneo hayo waweze kufaidika na Serikali hii pamoja na mimi Mbunge mwenyewe ambaye ninaenda kumalizia muda wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri, hii mifumo kweli Serikali tunaipongeza inajitahidi sana kutupatia fedha, lakini mmeweka mifumo hapa katikati wengi hawajui kuitumia hii mifumo. Mimi nina Mfuko wa Jimbo, nina fedha sasa hivi zina miaka miwili. Nimeahidi, nimepita kila maeneo, lakini kila wakifanya kwenye mifumo, fedha sawa zimo lakini hazitoki. Kwa hiyo, na penyewe kuna kila sababu Mheshimiwa Waziri kuliangalia na kuwapatia semina hawa Watumishi wa Serikali kwa maana ya Watendaji wa Kata, tena uzuri unao hapahapa wa jimboni kwako unaweza ukaanza nao na wao wakaenda kuambukiza kwenye wilaya nyingine huko, ili kusudi fedha zisiwe zinakwama kwenye mifumo hii ya *NeST. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine Mheshimiwa Waziri ninapenda kukupongeza kweli unapambana lakini hapa kwenye *NeST* angalia vizuri baba yangu, ili kusudi mambo yaende vizuri

zaidi. Kweli tunahitaji fedha hasa, lakini swali la kwanza kabisa ni vyema hapa kwenye kukusanya tu ndio unatakiwa ukae vizuri wewe pamoja na wenzako ili kuiwezesha Serikali yetu iweze kupiga hatua, halafu na kazi nyingine zifanyike.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninapenda nikushukuru wewe, pia niwashukuru wananchi wangu wa Mbogwe wote wapigakura. Tukiwa tunaelekea tumebakiza Bajeti Kuu na penyewe ninaimani nitapata nafasi. Niwaombe tu viongozi wangu humu ndani wazidi kunipanga na kuniamini na kwa kweli sasa hivi nimekomaa na mimi ninajiona nipo *fit*, nipo vizuri. Hakuna jambo litaharibika katika kuishauri Serikali kwa sababu jukumu la Mbunge ni kazi tatu nimeona na mimi nimesimama imara kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakumbuka wakati ninaingia humu ndani Wilaya ya Mbogwe ilikuwa haikusanyi kabisa. Mliniambia kama Serikali kwamba nikasimame kuhakikisha maovu yote ya yanapoonekana jimboni ninatoa taarifa hapa na Serikali inafuatilia. Ninawapongeza Serikali ambao wamenipatia ushirikiano ndani ya miaka hii mitano, kwa kweli wakinipatia miaka mitano mingine ina maana mambo yatazidi kuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimuombe huyu msimamizi tumeambiwa kuna Mkurugenzi wa Kusimamia Fedha Haramu. Hili jambo Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana. Huku ninamalizia.

Mheshimiwa Spika, hili jambo ni muhimu sana Mheshimiwa Waziri. Kweli kabisa hizi fedha haramu zipo. Unajuaje zipo wewe ni mtaalam na msomi. Unaweza ukamuona mtu anajenga ghorofa lakini hajulikani anafanya biashara gani. Kwa hiyo, kuna kila sababu anapoonekana mtu kwamba anafanya maendeleo fulan,i lazima tujue kwamba huyu anafanya biashara gani, Serikali ametulipa kodi ya *design* gani? Hakuna kuoneana huruma katika mambo ya fedha haramu kwa sababu tunafahamu wapo watu wanaouza madawa ya kulevya, pia wapo watu ambao wanaibia wengine na wanafanya maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nikushukuru mama yangu. Mungu akubariki sana Spika wetu, Mbunge na Rais wa Mabunge yote Duniani. Ahsante sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Elibariki Kingu, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kupewa nafasi hii adimu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Fedha na nianze kwa kuwapongeza sana kwa kazi nzuri sana ambayo mmeifanya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Fedha. Kwa kweli mmefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuthibitisha kwamba wamefanya kazi nzuri unaweza ukaona hata mapato ya Serikali yalivyoongezeka, lakini unaweza ukaona Bajeti ya Serikali wakati wanaingia ilikuwa chini ya shilingi trilioni 29, sasa hivi ni zaidi ya shilingi trilioni 50. Hiyo ni ishara ya kazi nzuri mliyoifanya kwa kweli tunawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Wizara kwa sababu Wizara hii ndio wasimamizi wa hesabu zote za Serikali na ndio wasimamizi wa wahasibu na wakaguzi wa ndani na wa nje. Katika kipindi hiki tumeshuhudia ripoti ya *CAG,* ripoti zake zimeonesha uimarikaji wa uwajibikaji na usimamizi mzuri wa fedha za umma. Ripoti hizo zimeonesha kutokana na ukiangalia taarifa za *CAG* zinazoridhisha zimeendelea kuimarika na zimekuwa ni nyingi kabisa na sasa hivi zile hati chafu zimekuwa kama ni historia, hazipo. Hii ni ishara kwamba kazi nzuri imefanywa na inaendelea kufanywa na hii Wizara Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee mimi ninaomba nizipongeze taasisi ambazo zimeonesha umahiri mkubwa wa kutayarisha hesabu za fedha vizuri na kwa viwango vizuri vya kimataifa. Moja ya taasisi hizo ni taasisi unayoiongoza wewe, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limefanya vizuri sana. Katika mashindano

ya vitabu vizuri vya uhasibu, Bunge tuliongoza tukashinda, kwa hiyo tumefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninakupongeza lakini ninaipongeza Wizara kwa kusimamia vizuri na kuhakikisha kazi inafanyika vizuri. Pia *CAG* ninampongeza kwa namna anavyofanya kazi ya ukaguzi. Kazi ni nzuri na ndio maana tunasema waendelee kuongezewa uwezo na fedha na rasilimali, ili aendelee kufanya kazi vizuri na uwajibikaji Serikalini uendelee kuimarika zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninapenda nitoe mapendekezo machache; la kwanza, sasa hivi kumekuwa na taasisi nyingi zile ambazo zilitakiwa zijitegemee, zilitakiwa zizalishe, zikusanye mapato yao, zijiendeshe kibisahara, taasisi hizo nyingi zimekuwa zinarudi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kutegemea mishahara kutoka Hazina. Sasa hii ya kutegemea zaidi mishahara kutoka Hazina inazifanya zile taasisi zibweteke, zisifanye kazi vizuri. Zipo taasisi nyingi za namna hiyo.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri mkalifanyie kazi mzichambue. Zile zinazoweza kusimama zenyewe, zisimame zenyewe. Wakala wanaoweza kusimama wenyewe, wasimame wenyewe badala ya kutegemea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali. Hili ni suala muhimu na ninafikiri litasaidia sana kupunguza mzigo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ninamuomba Mheshimiwa Waziri, kwanza ninawapongeza maana yake nimesikiliza taarifa yako nzuri na taarifa ya kamati imeonesha vizuri. Kwanza mafunzo ambayo mmeyatoa kwa wahasibu ni wengi nimesikia, mmetoa mafunzo mengi, lakini ninataka kuongezea kusema kwamba, bila mafunzo na wahasibu hawa kupata mafunzo ya kila wakati, bila wakaguzi wa hesabu hawa kupata mafunzo ya kila wakati hawawezi kutekeleza majukumu yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika utayarishaji wa vitabu vya uhasibu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa kuna mabadiliko kila siku yanajitokeza na mabadiliko haya yana-*necessitate*

kwamba lazima wahasibu wafundishwe kila wakati ili waweze ku-*comply* na hizo *standards. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukaweka mfano, kwa mfano, *IPSAS-17* kiwango hiki cha utayarishaji wa hesabu za kimataifa za taasisi kwa kuzingatia viwango vya kimataifa. Kwa upande wa Serikali *IPSAS-17* inataka mali za Serikali zile za kudumu zifuate taratibu fulani, lakini ukiangalia ukichukua taarifa za taasisi mbalimbali zilizofanya zikiwemo Wizara wameshindwa ku-*comply* vizuri na hii *standard IPSAS-17.*

Mheshimiwa Spika, wengine katika ku-*calculate depreciation* unakuta kwa mfano gari linatakiwa liwe *depreciated* kwa miaka mitano liwe limekwisha na likiisha linatakiwa liwe na *zero,* labda kama limebaki linabaki tu *carrying value unless* wanafanya *revaluation.* Wao unakuta wana *depreciate,* wanafika miaka mitano wanaendelea ku-*depreciate,* mpaka inaenda kwenye *negative.* Ukichukua taasisi nyingi ukiwauliza kwa nini hii ipo hivi? Wanakwambia ni kwa sababu ya mfumo. Sasa, hatuwezi kusema kwa sababu ya mfumo. Mfumo upo kwa ajili ya kuwasaidia kuweza kuandaa mahesabu, siyo kwa ajili ya kwamba mfumo unawajibika, wewe kazi yako ni kuchambua kile kilichotoka kwenye mfumo uone kama kina-*comply* na viwango, uweze kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ni vizuri muendelee kutoa mafunzo kama ulivyosema kwenye ripoti yako, mtoe mafunzo zaidi kwa wahasibu, hawa wakaguzi waweze kujua na ku-*comply* na *standards* hizi za kimataifa ili Tanzania iwe ni mfano katika utayarishaji wa mahesabu. Ninayasema haya kwa sababu mimi mwenyewe ni mtaalam wa hesabu na nimepitia mahesabu yale nimeona namna ambavyo yanakwenda yanavyofanywa vizuri na hii taasisi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nilitaka kushauri, sasa hivi kutokana na kwamba tuna mifumo mizuri ya kufunga hesabu, ule muda tuliokuwa tunautumia kufunga hesabu baada ya tarehe 30 mwezi Juni mpaka hadi tarehe 30 mwezi Septemba miezi mitatu, ni muda mrefu sana. Tumeshauri kwa muda mrefu

kwamba sasa muangalie huu muda upunguzwe, ninajua mmeupunguza lakini bado hamjapunguza kisheria. Kwa hiyo, hebu angalieni ile Sheria ya Fedha, punguzeni ule muda basi wapewe mwezi mmoja au miwili kwa sababu sasa hivi sesabu zinafungwa kwenye mifumo. Basi wafunge ili kusudi *CAG* aende kuanza kukagua mapema.

Mheshimiwa Spika, ule muda ambao *CAG* anapewa ule wa miezi sita badala ya miezi sita kuanzia mwezi wa tisa, urudishwe nyuma kusudi ripoti yake ile tuweze kuipata mapema na iweze kujadiliwa na Bunge na uwajibikaji uendelee kuimarika zaidi na hiyo itatufanya tufanye maamuzi kwa wakati na kuhakiksha kwamba kila kitu kinakwenda vizuri.

Kwa hiyo, mimi ninapendekeza mpitie Sheria ya Ukaguzi wa Hesabu *(CAG)* ile ya *NAO* ili tuweze kurekjebisha, tufupishe ule muda. Pia, mpitie Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2020 mpaka sasa hivi, ili kususdi tupunguze muda na uwajibikaji uweze kuimarika. Hilo litasaidia sana kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni hii mifumo; hii mifumo tunaomba ambayo Mheshimiwa Waziri ameisema ni vizuri sana mifumo iwe inaonana na ni vizuri kwa sababu mifumo yenyewe inagharimu fedha nyingi tunazozitumia katika kuweza kutayarisha hiyo mifumo. Sasa mifumo ile ikionana itaturahisishia sana kuweza kufanya kazi na njia nyingine ambayo itatusaidia sana tunaposema mifumo ni pamoja na ku-*manage* uchumi wetu, kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anajulikana anafanya nini na tuwe na mfumo wa namna hiyo. Sisi tunasema tukiwa na sera hii jumuishi ikitekelezwa ipasavyo, hali ya uchumi wa nchi yetu itakuwa ni nzuri, tutaweza kusimamia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *financial inclusion* ni kitu muhimu mno na bila kuifanya hivyo tutaendelea kuwa na *informal sector* na hivyo kutakuwa na upotevu mwingi wa mapato sasa hivi yapo nje ya mfumo, lakini pia watu wengi wanakwepa kodi kwa sababu tunatumia hiyo *cash system.* Tungekuwa wote tupo kwenye

mfumo jumuishi wa fedha, ninaamini mambo yangekwenda vizuri na kila kitu kingekwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa mimi niombe kushukuru na nimpongeze tena Waziri, watendaji wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Waendelee kuisimamia Serikali, mahesabu na fedha za umma ili kusudi Taifa letu liweze kuendelea. Tuweze kupata fedha za maendeleo, tuweze kuleta maendeleo katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, mimi nina uhakika kwamba kila kitu kinakwenda vizuri, uwazi umeiongezeka na uwajibikaji umekuwa vizuri. Hongereni sana na ninaunga mkono hoja. Ninawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni walioingia, leo tuna wageni wengi kidogo.

Wageni sita wa Mheshimiwa Jacquline Msongozi ambao ni jamaa zake kutoka Songea, Mkoa wa Ruvuma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba ambaye ni Waziri wa Fedha na hawa ni familia yake kutoka Dodoma; yupo Ndugu Jugulu Madelu ambaye ni kaka wa Mheshimiwa; Ndugu Sam Madelu - kaka wa Mheshimiwa; Ndugu Shaban Madelu - kaka wa Mheshimiwa; Ndugu Peter Madelu - mjomba wa Mheshimiwa; Ndugu Happiness Madelu - dada wa Mheshimiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

Anao wageni wengine Mheshimiwa Waziri ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Maafisa kutoka Wizara na Taasisi zake, wote wasiame kwa pamoja. *(Makofi)*

Haya sijui wamekaa upande gani, haya ninaona wengine walikuwa wameshatambulishwa wengine bado. Haya ahsanteni sana. *(Makofi)*

Nimeambiwa wapo pia Waheshimiwa Madiwani, haya ahsante sana; Sekretarieti ya Wilaya, karibu sana. *(Makofi)*

Haya viongozi wengine kwa sababu nilikuwa nimeshawataja pale awali, viongozi wote ambao ni wa Chama Cha Mapinduzi wasimame wote kwa pamoja, kwa sababu makundi mengine nilikuwa nimeshayataja awali. *(Makofi)*

Haya ahsante sana, lakini nimeambiwa hapa wapo watumishi kutoka Idara ya Elimu ya Awali na Msingi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia miongoni mwa watoto wanaolelewa na kusomeshwa na Mheshimiwa Waziri wakiongozwa na mlezi, Bi. Mwasambili, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. Nafikiri hawa watakuwa wametambulishwa wote. *(Makofi)*

Haya wageni wa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na hawa ni familia yake kutoka Jijini Dodoma; yupo Ndugu Mariam Chande ambaye ni mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu sana, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Hassan Hamad, mtoto wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana; Ndugu Naifat Hamad, mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana; Ndugu Umul Ayaman Hamad, mtoto wake; haya Ndugu Islam Simba, mtoto wake; haya Ndugu Ally Mohamed, kaka wa Mheshimiwa; Ndugu Mbwana Chande, kaka wa Mheshimiwa; Ndugu Seif Ismail, kaka wa Mheshimiwa; Ndugu Masoud Abdallah, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa; karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ambaye ni Waziri wa Kilimo na hawa ni Chama cha Ushiriki wa Wakulima wa Zabibu Mbarara kutoka Uganda, karibuni sana,

karibuni sana wageni wetu kutoka Uganda, naamini mnazungumza Kiswahili kwa hiyo mmeelewa. *(Makofi)*

Wageni 25 wa Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya ambao ni waumini wa Parokia ya Kisasa na pia ni timu ya *netball* kutoka Jijini Dodoma, wakiongozwa na Paroko Sosteness Ndendya, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni walimu wa shule za msingi kutoka Nsimbo na Manispaa ya Mpanda Mjini, Mkoani Katavi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wanachuo watatu wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, Kampasi ya Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 43 na walimu wanne wa Shule ya Msingi *Southern Highlands* kutoka Mafinga Mkoa wa Iringa, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Eribariki Immanuel Kingu atafuatiwa na Mheshimiwa Hamad Hassa Chande, Mtoa Hoja ajiandae.

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie kwa heshima yako kama Spika wetu, ninataka niwaambie Watanzania na kupitia Bunge lako hili Tukufu maneno machache yafuatayo katika sekta ya uchumi ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu ameisimamia kwa kipindi cha miaka minne toka amekuwa Rais, ili kusudi waone kwa nini Wajumbe wa Mkutano wa Chama Cha Mapinduzi wamempendekeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan awe mgombea wao kupiti tiketi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mashaka kwamba Waziri Dkt. Mwigulu na Naibu wake wamefanya kazi kubwa sana katika

Wizara hii ya Fedha, na ni watu wanyenyekevu sana na ni watu wasikivu sana. Kaka zangu ninawapongeza sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika *Fiscal and Monetary Policy* ya nchi yetu, Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanikiwa kutekeleza kwa vitendo *Fiscal and Monetary Policy* ambayo imepelekea Taifa letu kuweza ku-*maintain inflation* kwa kiwango cha 3.5% mpaka 3.7%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie, hii ni rekodi iliyovunjwa katika Mataifa yote ya Afrika Mashariki. Ukiangalia *Inflation Rate* katika mataifa ya *East Africa* sitaki kuyataja, ina-*range* kuanzia 6.3%; kuna mataifa ya *inflation rate* ya 17% na kuna mengine mpaka 45%. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhihirisha kwa vitendo kwamba Serikali anayoiongoza imeweza kuwajali Watanzania kuhakikisha *consumption power* ya umma walionayo na kipato walichonacho, mambo ya mahitaji ya *goods and service* kwenye Taifa letu, Serikali yake imedhihirisha uwezo mkubwa sana katika kulinda *stability* ya uchumi wa Taifa letu. Pongezi nyingi ziende kwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, ukuaji wa uchumi katika Taifa letu, ukiangalia kutokana na *shock* kubwa iliyopo ya kiuchumi duniani ambayo ilisababishwa na *Covid–19,* lakini pia ikaendelezwa na vita vilivyopo katika mataifa yenye nguvu ambayo ni wasambazaji wakubwa wa mafuta duniani, lakini Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza ku-*maintain* ukuaji wa uchumi kwa 5.6%, jambo ambalo rekodi hii pia imeendelea kuvunja rekodi katika mataifa ya *East Africa*. Nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika sekta ya uchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hiyo imepelekea ndani ya kipindi cha miaka hii na kupita mwaka uliopita, Kituo cha Uwekezaji cha *TIC* kimeweza kurekodi miradi yenye *value* ya shilingi bilioni 9.3. Kiuchumi hii ina tafsiri gani? Hii ina tafsiri kwamba sera

zinazotekelezwa za *Fiscal and Monetary Policy* ambazo zimeweza ku-*regulate* mambo ya *taxation*, ambazo zimeweza kuchochea suala la *employment*, ndiyo maana umeona kasi kubwa ya wawekezaji kutoka nje wameingia katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *impact* yake ni nini? Katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tumetengeneza ajira zisizopungua milioni nane. Tafsiri yake ni kwamba pasingekuwa na mazingira mazuri ya sera za kiuchumi za *Fiscal and Monetary Policy* ambao watekelezaji wake wakubwa ni Benki yetu Kuu ya Tanzania, na kwa muktadha huu niruhusu nitoe pongezi zangu za dhati kwa Gavana wetu Ndugu Tutuba wa Benki Kuu kwa ujasiri na uzalendo mkubwa alioufanya katika kusimamia mabenki Tanzania. Kwa sababu *stability* ya utoaji wa mikopo imeendelea kuendana na kasi ya ukuaji wa uchumi, jambo ambalo lime-*stabilize microfinance* za uchumi wetu, jambo ambalo limepelekea makusanyo ya mapato kuongezeka katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiri kwamba nitumie nafasi hii kukipongeza sana Chama Cha Mapinduzi, chama kilicho na Serikali madarakani. Juzi tulipokuwa kwenye vikao vya chama tumeona wamekuja na ilani ambayo inapelekea kutoa maelekezo ya ku-*digitalize* uchumi wa nchi na nimekuwa mchangiaji mzuri sana ambaye nimekuwa nikipingana sana na mambo ya *cash economy* katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahali popote duniani, Serikali zozote zinazotaka kuongeza *tax base* katika nchi zinasisitiza sana mambo ya *cashless economy*. Tukiweza ku-*digitalize* uchumi wetu tutaweza kuzi-*monitor transaction* katika nchi, tutaweza kujua nani anafanya shughuli gani na nani halipi kodi. Serikali itaweza kuongeza *tax base* ya kukusanya kodi katika Taifa letu, na hivyo kuongeza mapato katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja kwa nia njema, mimi ninapokuwa sina dereva *sometime* hapa Dodoma, *transaction* ninazozifanya kwenye *taxi* za hapa Dodoma natumia zaidi ya shilingi 60,000 kwa siku. Niulize swali Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni *taxi* ngapi zilizopo kwenye nchi yetu zinzofanya kazi ambazo

zina *device* za kielektroniki ambazo mtu akilipa pesa anapewa risiti na Serikali inapata kodi?

Mheshimiwa Spika, kuna mambo madogo sana ambayo kama Taifa letu tunayadharau lakini yanaweza yakawa *tax base* ya kuwasaidia *TRA* kuweza kuingiza mapato. Kama mnashindwa kuwatambua, twende mfano mdogo taasisi ya *Uber* ambayo imesajili *Uber* kwa malaki na malaki katika Taifa letu. Tunashindwaje kuchukua *statistics* za waendeshaji wa magari haya ya *taxi* kupitia watu wa *Uber? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda katika Taifa la Uingereza, utapanda *taxi* utachanja kadi Serikali itapokea kodi. Nenda kwenye Taifa la Ukraine, nenda mataifa yoyote duniani. Kwa takwimu nilizozifanya kwenye kodi ya haya ma-*taxi* peke yake, tunaweza tukapoteza zaidi ya shilingi bilioni 24 kwa mwaka, fedha ambazo zingeweza kupatikana zikawasaidia Watanzania katika sekta za maji, kilimo na sekta zingine katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, nataka nitumie Bunge lao Tukufu kumpongeza sana Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, pamoja na *economic setback* ya dunia, bado Taifa letu limeweza kufanya *strategic investment* ya miradi ambayo imekuwa *financed* na Wizara ya Fedha na fedha zimetoka. Miradi ambayo imekuja ku-*spillover impact* chini na kuchochea ukuaji wa Uchumi, kwa mfano kukamilika kwa Mradi wa *SGR*.

Mheshimiwa Spika, leo Dodoma kwa siku inaweza ikapokea wageni wasiopungua 2,000 mpaka 3,000, jambo ambalo linapelekea mapato kwenye hoteli, mapato kwenye vyakula, mapato kwenye viwanja vya ndege, mapato kwenye *taxi* ninazoziongelea. Lazima tumuunge mkono Rais wetu na tumtie moyo kwa kazi kubwa ya kizalendo aliyoifanya ya ku-*stabilize* uchumi wa Taifa letu na kufanya uchumi wetu uweze kukua kwa kasi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ninalotaka kushauri; tunaye Mtanzania ana kampuni inaitwa *Diversity Health and Social Care Limited* iko Uingereza, anaitwa Paschal. Mtanzania huyu uliponipa

kibali cha kwenda Uingereza miezi miwili iliyopita, mimi pamoja na Wizara ya Afya tulienda kumtembelea Mtanzania huyu kwenye ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, nataka niliambie Bunge lako Tukufu, Mtanzania huyu akiwa Uingereza kampuni yake imeweza kuwa *one of the best* kampuni katika Taifa la Uingereza katika ku-*recruit* watu kwenye sekta ya afya. Wastani kwa mwaka, kila mwaka analeta idadi ya kuchukua watu 200 kutoka Tanzania katika sekta ya afya kwenda kufanya kazi Uingereza na ni kazi rasmi kwa sababu ana vibali vya Serikali ya Uingereza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwa sababu gani? Wapo Watanzania ambao wameshindwa kwenda kufanya kazi Uingereza kwa kukosa mitaji midogo midogo. Ninatoa wito kwa Wizara ya Fedha, Waziri wa Fedha, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi imetoa maelekezo kwenye ilani, tuchochee na kukuza ajira za vijana na ndivyo agizo hili linatekelezwa na vyuo vyetu kuzalisha vijana wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni aibu, Taifa letu tunaletewa nafasi vijana wakapate ajira Uingereza, wanashindwa kwenda kisa wameshindwa kuwa na fedha za *visa*, wameshindwa kuwa na fedha za tiketi. Kwa nini Waziri wa Fedha usizungumze na mabenki vijana hawa wakasaidiwa fedha na mabenki, wakienda kupata ajira Uingereza watakapolipwa mishahara wakalipwa hizo fedha tukasaidia kupata ajira kwenye Taifa letu?

Mheshimiwa Waziri ninakuomba, utakapokuja ku-*windup*, kama hutatoa maelekezo kaka yangu, mimi bwana sitakushukia shilingi lakini wewe tunakwenda njia moja. Tutakuja kuzungumza nyumbani na nitakusema kinyumbani, kwa sababu tutakuwa tumewasaidia watoto wa Kitanzania kuweza kupata ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni hii ninayoizungumza *annual tan over* yake kwa Uingereza ni karibia bilioni 160. Mtanzania huyu ameajiri watu wengi na tulipokutana alitwambia anashindwa

kuwachukua Watanzania kwa sababu wanakosa hata hela za kulipa tiketi ya ndege.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalize kwa kuwaomba wananchi wa Uyole huko Mbeya, chonde chonde wananchi wa Uyole, tunawaomba sisi Wabunge wote, Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi na Wabunge kutoka vyama rafiki vya upinzani, Spika huyu ambaye ni dada yenu kutoka huko Mbeya na sisi ni dada yetu, amefanya mambo makubwa kwa Bunge, amefanya mambo makubwa kwa nchi. Chonde chonde Wana-Uyole, turudishieni dada yetu. Tunawapa kila kitu kinachostahili katika mustakabali wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. Wana-Uyole wamenisikia, tunaomba waturudishie wewe. Sisi tuna kazi na wewe kwa miaka mitano ijayo, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA**: Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususani barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba - Waziri wa Fedha, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni “Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.”

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Fedha, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi 10 iliyopita, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imesimamia kwa ufanisi ukusanyaji mapato na utekelezaji wa miradi mingi ya miundombinu ya

barabara, reli, bandari na kadhalika. Naipongeza Serikali kwa mwendelezo mzuri wa utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa umeme Mto Rufiji, mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. Umeme, reli na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika uchumi wa Tanzania na nchi za maziwa makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki wakati dunia inaendelea kupambana na athari za vita vya Urusi na Ukraine na pia janga la *corona virus (covid-19),* tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kutokana na nchi nyingi tunazoshirikiana kibiashara na kiuchumi kukumbwa na mtikisiko wa kiuchumi. Katika kipindi cha hivi karibuni, tumeshuhudia wadau wakubwa wa maendelea wakibadili sera zao kiasi cha kuathiri mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyoguswa ni pamoja na afya na maeneo mengine ya kibajeti ya maendeleo. Serikali iendelee kujipanga kimkakati kuongeza uwekezaji katika kilimo, madini, uchumi wa bluu, maliasili na utalii ili kuongeza uzalishaji na tija. Serikali kupitia Msajili wa Hazina anapaswa kuendelea kuimarisha mitaji kwa mashirika ambayo yatachochea ukuaji wa uchumi ikiwemo benki za *TADB, TCB, TIB* na *ATCL* ili iweze kusimama kibiashara ikiwa ni nguzo muhimu hata kwa sekta zingine. Msajili wa Hazina anapaswa kupewa nguvu zaidi ili asimamie mashirika ya umma ili yaendeshwe kibiashara na kwa tija ya kiushindani kwa hapa nchini na hata nje ya nchi. Kuongezeka kwa tija kwenye mashirika ya kibiashara itapunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa mapato ya kikodi na hata mikopo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea hata kwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kugharamia ujenzi huo, kwa vile kutakuwa na fursa kubwa za usafirishaji. Pamoja na ujenzi wa *SGR,* napendekeza kuendelea na kuboresha reli ya *TAZARA* na uboreshaji wa bandari zetu ikiwemo ujenzi wa bandari kavu ikiwemo ya Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki ili kupunguza gharama za kusafirisha pembejeo na mazao. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru

reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija.

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu mkubwa kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu. Usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za usafirishaji mizigo kwa wateja wa bandari kutoka Zambia, DRC, Malawi na hata kwa kupunguza gharama za usafirishaji wa pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuna fursa nyingi za muda mfupi za kuongeza mapato kupitia hatua za kiutawala ikiwemo ya kuondokana na matumizi na malipo ambayo hayana tija kwa Serikali na hata walipa kodi. Kutokana na mahitaji makubwa ya uwekezaji kwenye miradi ya kimkakati, uchumi wetu utaendelea kuwa na mahitaji makubwa ya mikopo ya pesa za kigeni na wakati huo huo kulipa mikopo iliyoiva.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha mapato ya fedha za kigeni yanaongezeka kupitia mazao ya kilimo, madini na utalii. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatasaidia kuimarisha uhimilivu wa Deni la Taifa na pia kuendeleza utulivu wa shilingi yetu dhidi ya sarafu kuu za kigeni na hata kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei. Serikali ihakikishe kipaumbele cha kuwekeza kwenye kilimo ikiwemo pembejeo na umwagiliaji kwa lengo la kuongeza tija na pia kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kulinda mfumuko wa bei. Serikali inashauriwa kuchukua hatua zaidi za kuimarisha sekta za kilimo, utalii, na madini ili kukabiliana na athari za kiuchumi wa kidunia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na athari za kiuchumi uliokumba dunia nzima ikiwemo changamoto za upatikanaji wa fedha za kigeni, hatua za kuimarisha sekta hizo hapo juu, inaweza kuwa fursa kwa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi kwenye madini hasa dhahabu, viwanda vya mbolea kutokana uwepo wa mali ghafi za madini ya *calcium carbonate, lime* na *phosphate*. Dhahabu ina historia ya bei kutoyumba kwenye soko la dunia kwa

vile mabenki yanatumia dhahabu kwenye kuwekeza na kutokana pia na kuyumba kwa thamani ya shilingi na hata dola ya Marekani.

Pia Serikali inaweza kutumia dhahabu kama mbadala wa kuwekeza amana zake. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi kidunia, Benki Kuu nyingi duniani zimeanza kuwekeza zaidi kwenye dhahabu na hii ni ishara nzuri kwa bei ya dhahabu kuendelea kuimarika kwenye soko la dunia. Serikali ijielekeze kununua dhahabu kwa shilingi toka kwa wachimbaji wadogo na kisha kuzitafutia soko kigeni la moja kwa moja na hatua hii itapunguza na kuzuia uvujaji wa mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Benki Kuu kuendelea kununua na kuwekeza kwenye dhahabu, napendekeza hili zoezi lilenge pia kuuza dhahabu wakati bei zinapanda kwenye soko la Dunia. Pia Serikali iweke mkakati wa kusaidia wawekezaji Wazawa kwenye uchenjuaji wa madini ili waweze kukabiliana na ushindani kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mradi wa Liganga na Mchuchuma, napendekeza Serikali kuchukua hatua kuharakisha uwekezaji kwenye mradi wa madini ya Niobium ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanda cha Ferroniobium *(FeNb)* ambacho kitakuwa cha kwanza Afrika na cha nne duniani. Kutokana na mahitaji makubwa ya ujenzi wa reli, madaraja na reli ya *SGR,* kuna mahitaji makubwa ya vifaa vya chuma ambavyo ni imara, lakini vyepesi na vyenye ubora wa kimataifa. Kwa kutumia sheria zetu za uwekezaji, Serikali itumie fursa za kipindi hiki ili kuvutia wawekezaji kwenye madini ya viwandani ili yaongezwe thamani hapa kwetu na pia kuvutia malighafi ya madini toka nchi zingine ili yachakatwe hapa kwetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imebahatika kuwepo kwa madini ya Niobium ambayo yanapatikana milima ya Pandahill Wilaya ya Mbeya na mahitaji ya Ferroniobium *(FeNb end product)* yanaendelea kuwa makubwa duniani na hapa kwetu pia.

Mheshimiwa Spika, Serikali inahitaji kujiwekekea mikakati ya haraka *(quick wins)* ili kuhakikisha inaimarisha uchumi ikiwemo kuboresha urari wa biashara kukabiliana na athari za changamoto za mabadiliko ya sera za wadau wa maendeleo na hata vita vya Urusi na Ukraine. Kwa kutumia rasilimali zetu za madini, Serikali inaweza kutengeneza fursa nyingi ikiwemo kupitia Mradi wa Niobium na Kiwanda cha Ferroniobium, ajira 2,000 zitakazozalishwa wakati wa ujenzi na pia kutakuwepo ajira za kudumu zaidi ya 600 na *indirect jobs 7,000.*

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Ferroniobium utazalisha mapato kila mwaka shilingi bilioni 500 *(US$ 220 million)* ambapo mapato kwa Serikali kila mwaka shilingi bilioni 50 *(US$ 22 million)* na uhai wa mgodi ni zaidi ya miaka 30. Hiki kitakuwa kiwanda cha kisasa cha kwanza Afrika *(Modern Manufacturing Plant and Smelter)*. Pamoja na kuingiza teknolojia hii adimu na ujuzi *(skills transfer)* pia itakuwa itachangia huduma za kijamii *(Corporate Social Investment in Community)* na chanzo cha fedha ya kigeni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upotevu mkubwa wa fedha za Serikali ikiwemo miradi ya Serikali Kuu na Halmashauri, napendekeza Serikali kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ili kuongeza ufanisi na uhuru wa Wakaguzi wa Ndani. Serikali ihakikishe Mkaguzi wa Ndani wakati wote anakuwa huru kutoka kwa Afisa Masuuli. Wakaguzi wa ndani wa halmashauri wasimamiwe na Mkaguzi Mkuu wa Mkoa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Serikali iimarishe uhuru wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(Internal Auditor General)* na napongeza Serikali kupandisha hadhi ya Ofisi kuwa na Fungu la Bajeti linalojitegemea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mwigulu L. Nchemba (Mb.) na Naibu wake Mheshimiwa Hamad H. Chande (Mb.), Katibu Mkuu - Ndugu Natu El-maamry Mwamba, Naibu Makatibu Wakuu Ndugu Jenifer C. Omolo, Ndugu Amina K. Shaaban na Ndugu Elijah G. Mwandumbya,

wataalamu wa Wizara na taasizi zilizoko chini ya Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya kwenye kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Fedha kwa sababu kwa kipindi hiki cha miaka mitano, usimamizi wake wa kukusanya mapato na kutafuta fedha za kuendesha Serikali na kutekeleza miradi mbalimbali ndiyo unatufanya leo tutembee kifua mbele. Mimi kule Moshi Vijijini miradi iliyotekelezwa na Serikali imesharekodi zaidi ya shilingi bilioni 50.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia kuhusu changamoto mbalimbali zinazowakabili wajasiriamali wanaofanya biashara za aina mbalimbali na nitatoa mapendekezo ya jinsi ya kuzitatua ili kuboresha ufanisi wa biashara za wajasiriamali. Utatuzi wa changamoto hizi utasaidia sana Wizara kufanikiwa kwenye kutafuta na kukusanya mapato ya Serikali kupitia kwenye kundi la wajasiriamali.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuuliza, Je, Mungu aliruhusu biashara? Jibu ni ndio. Mwanzo 34:10. [10] Nanyi mtakaa nasi, na nchi hii itakuwa mbele yenu; kaeni, na kufanya biashara humo, mkapate mali humo. Na katika vitabu vitakatifu, inaonekana kwamba zilifanyika biashara za aina mbalimbali.

Nehemia 13:16,20 inasema [16] Tena wakakaa humo watu wa Tiro, walioleta samaki, na biashara za kila namna, wakawauzia wana wa Yuda siku ya Sabato, na mumo humo Yerusalemu. [20] Basi wenye biashara na wachuuzi wa bidhaa za kila namna wakalala nje ya Yerusalemu mara mbili tatu.

Mheshimiwa Spika, vitabu vitakatifu vinatambua kwamba biashara inasababisha utajiri. Wana wa Mungu tunaelekezwa kufanya biashara halali tutajirike na hivyo basi kufanya biashara kama zile wanazofanya wajasiriamali siyo dhambi. Ezekieli 28:5 [5] Kwa hekima yako nyingi, na kwa biashara yako, umeongeza utajiri wako, na moyo wako umeinuka kwa sababu ya utajiri wako.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoekezwa hapo juu, wajasiriamali wamekuwepo tokea zama za kale, na ni kundi muhimu katika jamii linalotoa mchango mkubwa hivyo basi Serikali inatakiwa iliangalie kundi hili kwa jicho la pekee kwa ajili ya ustawi wao na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali ni watu wanaoanzisha na kuendesha biashara zao wenyewe badala ya kutegemea ajira ya moja kwa moja kutoka kwa mwajiri. Watu hawa wako katika makundi mbalimbali. Kwa mfano, wale wanaofanya:-

Moja, biashara ndogo ndogo ambazo hazihitaji mtaji mkubwa kama uuzaji wa vyakula; kuuza chipsi, maandazi au kahawa, uuzaji wa bidhaa za kawaida kama chumvi, sabuni au bidhaa za matumizi ya kila siku, na biashara za soko kama kuuza mboga, matunda, au bidhaa za nyumbani sokoni.

Pili, biashara za huduma; huduma za urembo kama saluni za nywele, huduma za vipodozi, au masaji, huduma za usafirishaji kama kuendesha bodaboda, bajaji au magari ya uchukuzi, na huduma za elimu kama kufundisha masomo, kozi za mtandaoni, au kutoa ushauri wa kitaaluma.

Tatu, biashara za kilimo; kilimo cha mazao kama kuzalisha mazao kama mahindi, mpunga, mboga, na matunda kwa ajili ya kuuza, ufugaji kuku, ng'ombe, mbuzi, au samaki, na uzalishaji wa mbegu na miche: kuuza mbegu za mazao au miche ya miti.

Nne, biashara za sanaa na ubunifu; sanaa ya michoro, kuuza michoro au kazi za mikono, muziki na filamu kama kuimba, kucheza, au kutengeneza filamu, na ubunifu wa mitindo kama kutengeneza nguo au viatu vya kipekee.

Tano, biashara za fedha; udalali wa hisa kama kuuza na kununua hisa kwa wateja, wakala wa pesa kama kufungua wakala wa huduma za kifedha kama M-Pesa, Tigo Pesa, au *Airtel Money,* na kutoa mikopo midogo kama kuwakopesha watu fedha kwa riba.

Sita, biashara za kilimo-biashara; usindikaji wa unga kama kutengeneza unga wa mahindi, sembe, au unga wa lishe, uzalishaji wa bidhaa za chakula kama kutengeneza asali, siagi ya karanga, au juisi, na uzalishaji wa mbolea kama kutengeneza mbolea za asili kutoka kwa mabaki ya mimea au wanyama.

Saba, biashara za burudani na utalii kama usimamizi wa safari za watalii kutoa huduma za kutembelea vivutio vya utalii - *tour guide,* maonesho ya sanaa kama kuendesha maonesho ya utamaduni.

Mheshimiwa Spika, wajasiriamali waliotajwa hapo juu ni nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi, kwani wanachangia katika kuzalisha ajira, kuleta ubunifu, na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi. Hata hivyo, safari ya ujasiriamali imejaa changamoto nyingi zinazoweza kuathiri ukuaji wa biashara na kufikia malengo ya kifedha na kimaendeleo. Changamoto hizi zinatokana na sababu za kutokuwa na elimu ya biashara, kifedha, sera na sheria zisizo rafiki, kiteknolojia, masoko ya bidhaa, kiutawala, na kijamii ambazo mara nyingi huwa na athari kubwa kwa biashara mpya au ndogo.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zikipatiwa ufumbuzi, kundi hili la wajasiriamali litachangia kikamilifu kwenye kufanikisha vipaumbele vya bajeti ya Wizara ya mwaka 2025/2026 kwenye kutafuta na kukusanya mapato ya Serikali kufikia shilingi trilioni 50.17 kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto kubwa za wajasiriamali ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, changamoto ya elimu na mafunzo ya biashara kwa jamii; elimu ya biashara ni muhimu kwa wajasiriamali wa makundi yote kama yale yaliyoainishwa hapo juu ili kufanikiwa katika uendeshaji wa biashara zao. Hata hivyo, baadhi ya wajasiriamali hawana ujuzi wa masoko, usimamizi wa fedha, na mbinu za kujenga mikakati ya biashara. Kwa mfano, mjasiriamali anayejishughulisha na biashara ya kilimo anaweza kushindwa kujua jinsi ya kupanga bei, kutafuta masoko, au kudhibiti gharama

za uzalishaji. Kukosa ujuzi na elimu ya biashara huathiri ufanisi wa biashara na kuzorotesha maendeleo ya biashara ya mjasiriamali.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali ianzishe programu maalumu za kutoa mafunzo ya usimamizi wa biashara na ujuzi wa kibiashara kwa wajasiriamali. Katika hili, wajasiriamali wanapaswa kupewa mafunzo ya ujuzi wa kibiashara na usimamizi wa biashara ili kuwasaidia kuwa na mipango bora na kuongeza ufanisi wa biashara zao. Vilevile, jamii inapaswa kuelimishwa kuhusu umuhimu wa elimu ya biashara na ujuzi wa kibiashara ili kuwawezesha wajasiriamali kufanikiwa na kuongeza tija na kuchangia kwenye ulipaji wa kodi.

Pili ni changamoto ya upatikanaji wa mitaji na rasilimali za kifedha; wajasiriamali wengi hukabiliwa na changamoto ya kukosa mitaji ya kuanzisha na kukuza biashara zao. Upatikanaji wa mikopo ni mgumu kutokana na masharti magumu ya benki na taasisi za kifedha ambazo mara nyingi huhitaji dhamana kubwa kutoka kwa wajasiriamali. Kwa mfano, nchini Tanzania, wajasiriamali wadogo hukosa mitaji ya kutosha kwa ajili ya kununua vifaa vya kisasa hali inayowafanya washindwe kushindana katika soko. Ukosefu huu wa mitaji unazuia wajasiriamali wengi kufikia malengo yao ya kifedha na kuathiri ukuaji wa biashara zao.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuanzisha madirisha maalumu katika mabenki kwa ajili ya kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wajasiriamali. Mikopo nafuu itaongeza urari wa biashara kwa kundi hili na kuongeza makusanyo ya Serikali kupitia kodi na ushuru mbalimbali. Pia itamaliza changamoto ya wajasiriamali hawa kutumiwa na wafanyabiashara wakubwa kuwauzia bidhaa zao kwani watakuwa na mitaji yao. Kwenye kutoa mikopo ya riba nafuu na mafunzo ya kifedha kwa wajasiriamali, Serikali na mashirika ya kifedha yanapaswa kutoa mikopo ya riba nafuu kwa wajasiriamali na kutoa mafunzo ya kifedha kwa ajili ya kuwasaidia kuanzisha na kuendeleza biashara zao.

Tatu ni changamoto ya kukosa ulinzi wa kisheria na kutokuwepo kwa sera madhubuti za ujasiriamali; katika baadhi ya nchi, wajasiriamali hukosa ulinzi wa kisera na kisheria wa biashara zao kutokana na ukosefu wa sera na sheria rafiki za kusimamia biashara ndogo ndogo. Hii hufanya wajasiriamali kuathiriwa na changamoto kama ushindani usio wa haki au utapeli.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuweka sera na sheria zinazolinda wajasiriamali wadogo. Serikali inapaswa kuweka sera na sheria zinazolinda biashara ndogo ndogo na wajasiriamali dhidi ya ushindani usio wa haki na utapeli ili kuhakikisha usalama wa biashara zao. Wajasiriamali wanapaswa kupewa mafunzo ya jinsi ya kulinda biashara zao kisheria ili kuondoa changamoto za ushindani usio wa haki na utapeli.

Nne ni changamoto ya ukosefu wa masoko na ushindani wa kibiashara; masoko ni kipengele muhimu kwa biashara yoyote, lakini wajasiriamali wanakutana na changamoto ya kupata masoko ya bidhaa na huduma zao. Wajasiriamali wengi hawana uwezo wa kufikia wateja kwa urahisi au kukidhi mahitaji ya wateja kutokana na gharama za masoko au kutokuwa na mipango bora ya masoko. Kwa mfano, hapa nchini Tanzania, wajasiriamali wanaojihusisha na kuzalisha mazao ya kilimo hukutana na changamoto ya kukosa masoko ya uhakika kwa mazao yao. Hali hii husababisha bidhaa zao kuharibika au kuuzwa kwa bei duni, jambo linalowasababishia hasara.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kusaidia wajasiriamali kufikia masoko ya ndani na nje. Katika hili jambo, Serikali na taasisi zinazoshugulikia masoko wanapaswa kuweka mipango ya kusaidia wajasiriamali kupata masoko ya ndani na nje ili kupanua soko la bidhaa zao na kuongeza mapato yao.

Changamoto ya tano ni matumizi ya teknolojia ya kisasa; teknolojia ya kisasa ni nyenzo muhimu kwa wajasiriamali kuongeza ufanisi wa uzalishaji na kufikia masoko mapya. Hata hivyo, wajasiriamali wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za teknolojia ya kisasa au ujuzi wa kuitumia. Kwa mfano, mjasiriamali anayefanya biashara za kilimo hapa Tanzania anaweza kukosa

uwezo wa kununua *computer* ya kumsaidia kufuatilia mifumo ya masoko duniani jambo linalomfanya kushindwa kupata taarifa za masoko duniani. Kukosa teknolojia ya kisasa huathiri uwezo wa wajasiriamali kufanikisha shughuli zao na kupunguza ubora wa bidhaa na huduma.

Naishauri Serikali kuhamasisha wajasiriamali kujielekeza kwenye matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa gharama nafuu. Serikali na mashirika ya maendeleo zinapaswa kusaidia wajasiriamali kupata teknolojia ya kisasa kwa gharama nafuu na kutoa mafunzo ya matumizi yake kwa ufanisi.

Sita ni changamoto ya kudhibiti gharama za uendeshaji na bei za malighafi; wajasiriamali hukutana na changamoto ya kudhibiti gharama za uendeshaji wa biashara na bei za malighafi. Bei za malighafi kama vile pembejeo za kilimo zikiwemo mbegu, mbolea na dawa mara nyingi huwa juu, jambo linaloongeza gharama za uzalishaji. Hali hii inawaongezea gharama za uzalishaji na kuwafanya kushindwa kushindana kwenye bei katika soko huria la bidhaa zao ukilinganisha na wazalishaji wengine. Changamoto hii huathiri faida ya biashara na kuathiri uwezo wa wajasiriamali kutoa bidhaa bora kutokana na kushindwa kumudu gharama za pembejeo.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali kuhamasisha wajasiriamali kuweka malengo ya biashara na kudhibiti gharama za uendeshaji. Wajasiriamali wanapaswa kuhamasishwa kuwa na malengo ya biashara na kujifunza kudhibiti gharama ili kuhakikisha biashara zao zinakua na kuimarika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuishauri Serikali kuwa ni muhimu kuhakikisha kuwa changamoto hizi zinazowakabili wajasiriamali zinawekewa mikakati ya kuziondoa ili kundi hili likue na liweze kuchangia katika maendeleo ya jamii na Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii ya kutoa mchango wangu pamoja na tu kuweka nyalio kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuja kuhitimisha rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu Rahimu, Mungu ambaye kwa uwezo wake ametujaalia kukutana siku ya leo hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya na kujadili mambo muhimu na adhimu kwa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini. Miaka yote hii niko katika sekta hii ya Wizara ya Fedha mimi na Mheshimiwa Waziri wangu. Hii ni imani yake kubwa sana na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais pia kwa namna anavyokuwa na uwezo mkubwa sana wa kutafsiri sera kwa vitendo na kila mmoja wetu anajua kwamba Mheshimiwa Rais ni mahiri sana kwenye kutafsiri sera kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni sera nyingi zilikuwepo kwenye makabati, zilikuwemo kwenye vitabu, leo Mheshimiwa Rais anazitafsiri kwa vitendo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais na tunaomba tumpe maua yake Mheshimwia Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa yale mema na makubwa ambayo ameyafanya katika nchi yetu, kila mmoja mwenye macho na asiye macho haambiwi tazama, anayaona mwenyewe na hii tunasema kabisa kwamba Mheshimiwa Rais kwa makubwa yale aliyoyafanya, hata kijana yule basi anaelewa kwamba mama anafanya mambo mazuri na makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba nikushukuru sana wewe na nikupongeze kwa mambo kadhaa. Naomba uniruhusu

nitaje matatu; jambo la kwanza, kwa kutambua mchango mkubwa sana wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mkasema hatutotambua kwa kushukuru tu kila mmoja wetu wakati akichangia, aah aah, tunamwita tunampa tuzo yake. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili kwa kuwa Rais wa *IPU;* siyo jambo rahisi, ni jambo kubwa sana. Nafasi ile imepata mtu sahihi na kwa wakati sahihi. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu naomba uniruhusu nimshukuru sana Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Waziri Mkuu, kwa maelekezo yao kwetu. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu pia nimshukuru *mentor* wangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwa kweli nimejifunza mengi na namshukuru kwa malezi yake mazuri. Hapa nilipofika leo nimesimama kwa miguu miwili ni kwa sababu ya malezi yake. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Kamati ya Bajeti wakiongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Oran Njeza, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wenzangu. Kwa kweli wamefanya kazi nzuri na wanatupa ushirikiano makubwa kwa kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao makubwa sana. Lile ambalo lilitokea Jumatano kama ya leo wiki iliyopita ni kwa sababu ya dua zenu na sala zenu, nawashukuru sana. Nami niwaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana kwa pamoja. Halafu niwapeni siri; uko usemi usemao zimwi likujualo halikuli likakwisha. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu wote *In Shaa Allah* mrudi awamu hiyo ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuje tushirikiane katika ujenzi wa Taifa hili, kwa sababu kama ingekuwa inaruhusiwa, kama ipo kwenye utaratibu Waheshimiwa Wabunge hawa walioshuhudia mema na

makubwa yaliyofanywa na kwa namna walivyosimamia na wao katika majimbo yao na mikoa yao, basi wangewekwa katika wino maalum wa dhahabu. Majina yao yaandikwe kwa wino maalum wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo ni siku ya kuhitimisha na mhitimishaji ni Mheshimiwa Waziri. Nataka niongee tu mambo machache. Waheshimiwa Wabunge wengi wameshauri na wameelekea kwamba tuimarishe ulipaji wa kodi, yaani uimarishaji wa upatikanaji wa mapato. Serikali hili imelipokea na tunaenda kulifanyia kazi na kwa kweli tumeandaa mifumo mingi na tunajitahidi sasa iende kusomana ili kukuza mapato ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ni kweli walichosema Waheshimiwa Wabunge, kwamba wako baadhi ya watu ambao labda niseme hawaitakii mema nchi yetu au wamekosa uzalendo, ambao wanakwepa kodi kwa makusudi na bahati mbaya wale ambao wanakwepa kodi baadhi ya watu wanawafurahia, wanawaona wanalolifanya ni jambo jema.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo bahati mbaya na tumeelekezwa kabisa na vitabu vyetu vya dini kwamba ukiona uovu, yaani kama mtu anakwepa kodi huo ni uovu. Ukiona uovu, ukiona tendo baya basi liondoe kwa mkono wako, kama huwezi lisemee, angalau sema tu, toa taarifa, lakini ukishindwa basi chukia tu usifurahie, chukia ingawa huo ni udhaifu kidogo unapaswa uliondoe ama ulisemee.

Mheshimiwa Spika, hili Serikali inaahidi itaenda kulifanyia kazi na tutahakikisha kwamba mianya yote ya ukwepaji wa ulipaji kodi imezibwa kwa wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Balozi Subira amesema tuongeze mapato kupitia bandari zetu, Serikali imeimarisha mifumo na tutaendelea kuimarisha na kuifuatilia na kusimamia kabisa kuhakikisha kwamba mifumo inasomana na tumeongeza mapato yetu hasa katika sehemu zetu za bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimewasikia Waheshimiwa Wabunge, wenzangu wakisema kwamba tuendelee kuimarisha *cash economy*. Serikali imeshatoa miongozo, imeshatoa maelekezo jambo hili lipo, hatutakiwi tutembee kama alivyosema ndugu yangu, wakati mwingine ni ushamba kabisa kutembea na pochi zile na fedha amesema ndugu yangu. Sio nzuri, kwanza tunaambiwa *wallet* ukiweka mfukoni kama umeweka upande hivi unaweza ukaumiza mgongo wako, kwa hiyo hatutaki wananchi wetu waende kuumiza migongo kupitia hizo pochi kubwa ambazo wameweka kwenye mifuko yao.

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, niwaambie kwamba haya tunaenda kuyafanyia kazi na tutaimarisha kuhakikisha kwamba tunatumia *cashless* katika matumizi yetu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niseme kwamba tumepokea pongezi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, zile za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tumezipokea kwa mikono miwili na niwaambie tu yale mema na mazuri yote ambayo mmeona Wizara ya Fedha imefanya basi Mheshimiwa Rais apewe maua yake kwa sababu yale ni maelekezo yake na kama kuna mapungufu ndani ya Wizara ya Fedha, basi mapungufu hayo ni ya kwetu sisi, yeye hayamuhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana familia yangu, watoto wangu, wake zangu nawashukuru sana kwa namna walivyotoa ushirikiano mkubwa lakini nawashukuru sana Wana-Kojani, Wana-Kojani nawashukuru sana na nawaomba sana pamoja Spika hapo nawe piga sala zako nirudi tena katika mjengo huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe sana wananchi wa Iramba Magharibi, huyu Mheshimiwa Waziri ambaye wametuletea bado tunamuhitaji sana. Niwaombe sana, sana waturejeshee mtu huyu, chonde chonde wasije kufanya masihara na hili, lakini niwaombe na mimi wananchi wa Uyole watuletee Spika wetu. Wananchi wakati huo wa Mbeya Mjini walimchagua Mbunge tu, amekuja

amekuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ameenda kuwa Rais wa Mabunge Ulimwenguni, sio kazi rahisi sana, niwaombe sana waturejeshee Mheshimiwa Spika, tuendelee kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache mimi naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mtoa Hoja aje ahitimishe hoja yake.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja hii siku ya leo, nikianza na kukushukuru wewe mwenyewe pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia pamoja na maoni ya Kamati ambayo ni kwa niaba ya Bunge zima, ambayo imefanikisha hotuba ya leo pamoja na maoni haya ambayo tumeyapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee zaidi niwashukuru na ndugu zangu wananchi wa kutoka Iramba ambao wapo hapa na kama unavyoona tukitumia lugha ya mashujaa, leo kwako hapa ni kama kwetu tu maana yake tuko wengi kweli kweli, tunakushukuru sana kwa nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikijibu hoja kwa ufupi kwa maana ya baadhi ya hoja zingine tutazitolea tamko kwenye hotuba kuu ya Serikali, niseme tu machache; moja tumepokea hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezitoa zikiwemo za taarifa nzuri ya Kamati pamoja na michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na kama ulivyoona michango iliyotolewa na Wabunge ni ya kibunge kweli kweli, ya kizalendo kweli kweili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, una Wabunge makini sana na Watanzania waliyochagua Wabunge hawa ni Wabunge ambao wamefanya kazi nzuri sana, hoja za kizalendo, hoja za kibunge na kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyotangulia kusema pamoja na wachangiaji Watanzania wasisite tena kuwarudisha Wabunge hawa ambao wamefanya kazi nzuri ya kizalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na hoja moja ambayo amechangia Mheshimiwa Kandege, kwa ukubwa wake; moja tumeipokea Mheshimiwa Kandege, hoja ya utekelezaji wa sheria yetu mpya ya masuala ya matumizi ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni. Tumeipokea na tumeshapata maoni mengi na tumepata maoni mengi pia hata kutoka kwenye sekta na bahati nzuri sana Gavana wa Benki Kuu pamoja na timu yake ya wataalamu yupo hapa lakini si tu kwamba yupo pia ameendelea kufanya vikao na sekta kuweza kuangalia ni jambo gani, ni sehemu gani inahitaji maboresho zaidi kuweza kuona ni sehemu gani inahitaji ufafanuzi na yote hayo tumeyapokea na yale ambayo yanahitaji marekebisho tutafanya na yale ambayo yanahitaji mabadiliko tutafanya na yale ambayo yanahitaji ufafanuzi kupitia Bunge lako Tukufu tutaendelea kuyafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nikumbushe tu kwamba kwa nini tulichukua hatua hizo, nchi karibu zote za Afrika na duniani tulipita kati ka kipindi ambacho kilikuwa kigumu sana cha upatikanaji wa fedha za kigeni na Bunge lako Tukufu litakumbuka. Kuna wakati nchi zinazotumia bandari yetu zilikuwa na mizigo inakaa bandarini mpaka siku 30, siku 40 mpaka siku 60 kwa sababu hawana fedha ya kigeni ya kutoa mafuta yao, ilikuwepo inakuwa pale bandarini.

Mheshimiwa Spika, si hivyo tu hata sisi pia tulikuwa tunapata uhaba huo pamoja na kwamba tulikuwa vizuri kuliko nchi nyingi za Afrika, lakini hata sisi Waheshimiwa Wabunge watakumbuka tulikuwa tunapata shida hiyo. Shida ambayo ilikuwa inatishia upatikanaji wa bidhaa za muhimu ambazo hazipatikani ndani ya nchi, mfano uagizaji wa mafuta, mafuta ya kula, *pharmaceuticals* ambazo zinatoka nje pamoja na bidhaa zingine ambazo ni za sekta binafsi kabisa za masuala ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, hii ilikuwa inatokana na nini? *Pressure* ya uhitaji wa dola ulikuwa mkubwa sana, sasa hivi pameimarika imarika tunaweza tukapata uhuru huo wa kulegeza legeza lakini kwa wakati huo kwa sababu kulikuwepo na utofauti wa uhitaji wa bidhaa ilikuwa ni busara Serikali lazima ichukue hatua na katika kuchukua hatua iweze kupata shuruhisho la tatizo ambalo lilikuwa kubwa. Sisi tumetangulia, nchi nyingine bado hawajaimarika kama sisi ambavyo tumeimarika. Kuna nchi bado wanashida kubwa hiyo ya kuweza hata kupata bidhaa muhimu kama mafuta, zipo nchi ambazo bado wanapata shida na kinachosababisha hasa washindwe kupata mafuta si kwamba mafuta hayapatikani kule yanakotakiwa kutoka, wanakosa fedha ya kigeni ya kuweza kulipia mafuta hayo, wapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo nchi nyingine zinashindwa kuchangia michango yao ya kimataifa, wana-*default* kwa sababu wanakosa fedha ya kigeni. Sisi tumepiga hiyo hatua, lakini tulichukua hatua kuna sehemu tuliweza kubana zaidi, kuna sehemu tuliweza kutokuelewana vizuri tu katika namna tuna maanisha nini kisheria, lakini angalau hivi tunavyoongea lile lililokuwa tatizo kubwa la kiwango hicho la upatikanaji wa fedha za kigeni halipo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye maeneo yale yapo ambayo kiukweli yalikuwa yanatakiwa tuchukue hatua kama hizo, kwa mfano, natoa mfano, kwa mfano taasisi ya Serikali inayotoa leseni kwa mwananchi, kwa nini imtake mwananchi ambaye fedha yake ya nchi ni shilingi ya Kitanzania, kwa nini imtake mwananchi apeleke dola kupewa leseni ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani hili ni jambo ambalo Serikali na Idara zake za Serikali inapotoa huduma kwa Mtanzania kwa kweli inatakiwa isimsumbue Mtanzania kwenda kutafuta dola na wakati ule ilikuwa haipo, inamtaka akalete dola katika mazingira ambayo hata Serikali inatambua kuna uhaba wa dola.

Kwa hiyo, tulisema baadhi ya maeneo kama hayo ambayo Serikali ndio inatoa huduma na inatoa huduma kwa Mtanzania tuliona tuondoe hilo sharti la kutaka alete dola, kwa hiyo, hilo

tuliona tuliweke kwa namna hiyo na nadhani kwenye hilo hatujapata usumbufu na wala hatujapata malalamiko kutoka kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine ambalo lilikuwa linahusisha masuala ya ada za shule, masuala ya nyumba na kuna maeneo mengine hata mahitaji ya watu wanafanyiana biashara kiwanja wakawa wanaweka sharti hilo kwamba walipane kwa dola. Hiyo tuliona inakiuka sheria na inawafanya wananchi wetu wapate shida ya kutafuta dola wakati fedha yao halali ya kikatiba, ya kisheria ni shilingi ya Kitanzania. Kwa hiyo hilo tuliona likae kwa namna hiyo, lakini yapo maeneo ambayo tumeona, ambayo Gavana wa Benki Kuu anaendelea kushauriana na wataalam pamoja na sekta husika. Yapo maeneo ambayo yanahusisha biashara kubwa kubwa zile za kimataifa, tumesema hata hivyo katika baadhi ya maeneo ilikuwa ni tafsiri tu kwamba kwa biashara ile ya kimataifa inayovuka mipaka ambayo inahusisha masuala mengine ya kimataifa ilikuwa ni tafsiri tu ilikuwa haihusishi kwamba na wao wanatakiwa wapate sharti hilo la shilingi.

Mheshimiwa Spika, ile ilikuwa imetajwa, ilikuwa imejumuishwa kwa ukubwa wa sheria ambapo kusudi lake lilikuwa sio hilo na kama bado kuna tafsiri itakuwa bado inaleta ukakasi tumekubaliana na wataalam wa Wizara ya Fedha pamoja na taasisi zetu ikiwemo Benki Kuu kuweza kuona maeneo yale ambayo yalikuwa yanapotoka kwa utaratibu wa tafsiri yake tuweze kuyanyoosha ili kusudi lililokuwa limekusudiwa liweze kufikiwa, lakini tumekaa pia na taasisi zinazofanya shughuli kubwa hizo, Wizara ya Nishati, *The Light* ya *TANESCO*, *TPDC* na maeneo mengine ambayo wanafanya shughuli kubwa ikiwemo na miradi mikubwa kama bomba la mafuta pamoja na maeneo mengine, tuweze kuona matatizo yanayojitokeza ili tuweze kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ilikuwa njema ya kuondoa *pressure* ile ambayo na kwa kweli leo hii tumeona imejitokeza kwamba tatizo lile la ukosefu wa fedha za kigeni tumelivuka na tunaamini kwamba tutaweza kurekebisha. Kilichokuwa kinatokea na hata sasa tunaendelea kusisitiza katika baadhi ya maeneo,

kama taasisi ya nje inafanya shughuli zake mathalani inauza bidhaa zake nje na inapata dola, ikija kulipa dola kwenye taasisi zetu ama kwa wananchi wetu bado dola inakuja na inatusaidia kupata dola. Kwa ukubwa ule mathalani wameuza kama ni dhahabu, wameuza kama ni…, taja bidhaa yoyote wameuza nje wakapata dola kama wanakuja kuilipa taasisi kwa dola hizo haitengenezi *pressure* yoyote ndani ya uchumi wetu, lakini kama wanataka wakalipe dola kwa viwango vikubwa vikubwa, lakini na wao kumbe dola hizo wanatarajia wazipate ndani ya nchi pale ndio tatizo linapoanzia kwamba yule aliye mkubwa ataenda kukusanya dola kote na wale walio wadogo watakosa hata za kufanya hivi vishughuli vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, tulifika wakati wafanyabiashara wetu walikuwa wanapata shida sana kwamba mtu anazunguka kwenye benki anapewa dola 500 yaani hata anahitaji dola 6000, dola 7000 anaenda kwenye benki anakusanya anapewa dola mia tano, mia tano. Mzigo wake umeshafika bandarini au mzigo wake umeshakuwa tayari au ameshaishiwa mzigo mwingine anataka aagize mizigo mingine, ilikuwa ni shida na ilikuwa inashusha kasi ya kukua kwa uchumi.

Kwa hiyo, tumelipokea kwa sababu sheria ilikuwa mwaka jana na sasa hivi tuna fursa ya sheria pale ambapo panahitaji maboresho ili twende vizuri zaidi tumepokea na tutaboresha na pale ambapo hapana malalamiko na panaenda sambamba na sheria tutaendelea kutoa elimu kama jambo lilikuwa ni suala la uelewa.

Mheshimiwa Spika, amelisemea vizuri ndugu yangu Kasalali na Wabunge wengine waliyoongea kuhusu jambo la masuala haya ya kodi. Ni kweli bado pana shida ya uelewa na uunganishaji kwamba maendeleo yetu ni kodi zetu, kila jambo tunaloliona la maendeleo ni kodi zetu. Zamani ambazo zilishapita, kwenye bajeti zetu kulikuwa na fedha zinaitwa fedha za misaada za kibajeti.

Mheshimiwa Spika, wakati ule ulishapita haupo tena, kwa sasa hivi kila kitu tunachokiona cha maendeleo, kuanzia miradi

mikubwa hadi ile miradi ya huduma za jamii pamoja na maeneo mengine yote ni fedha za kodi zetu na kuna mwingine atasema sasa kama ni kodi zetu mbona bado huwa mnakopa? Hata ukikopa utalipa deni kwa kodi zetu, kukopa ni kuyaleta mapato yako yote karibu ili utekeleze mradi, halafu uanze kurejesha kwa kipato chako cha muda mdogo mdogo cha mwezi mmoja moja na hili jambo si jambo geni hata katika maisha yetu ya kawaida huwa yapo kwamba mtu yeyote ambaye analipwa mshahara yule anayepitisha mshahara wake kama ni benki anampitishia mapato yake kwa mara moja ili afanye jambo moja kubwa halafu mapato yake yale anayoyapata aanze kurejesha kidogo kidogo. Huu ni utaratibu ambao upo hata kwenye maisha ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Wabunge huwa wanatumia utaratibu huo, anapata mapato yake, halafu anafanyia jambo lake kubwa la maendeleo, anachangia vituo vya afya, anachangia ujenzi wa madarasa, anaunga mkono pale ambapo wananchi wamejitolea, halafu mapato yake yeye anaanza kuwa pakame, yale mapato yake anaanza kurejesha kidogo kidogo kila mapato. Huu ni utaratibu wa kawaida na wala si jambo la kutisha wala watu wasitishike, kubwa tu ni kwamba bajeti ya Serikali inazingatiwa, Serikali haikopi zaidi ya ilichopitishiwa na Bunge lake Tukufu na vilevile haikopi kwenda kupeleka kwenye matumizi yasiyo ya maendeleo, mnakusanya unapeleka kwenye miradi iliyo ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba mradi amabo unaweza kuujenga kwa miaka mitano kwa kuchukua fedha kubwa mathalani dola bilioni tatu kama wa reli ya kisa ungeamua kuujenga kwa *cash budget* kwa makusanyo ya kila mwezi ungejenga kwa miaka 40. Sasa kiuchumi unasema nenda kachukue mkopo ambao utaulipa kwa miaka 40 ujenge kwa miaka mitano wananchi waanze kupata huduma halafu hiyo miaka 40 ambayo ndio ulitakiwa ujenge mradi kwa miaka 40 utatumia tu kufanya marejesho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki tunachokisema ndicho ambacho Serikali ya Tanzania inafanya, kwenye Deni la Taifa la Tanzania

67% ni mikopo ya *multilaterals,* Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *IMF*, mikopo ambayo kipindi chake cha kurejesha ni miaka 30 mpaka 35 mpaka 40 ndio maana nikiwa Waziri hapa nimeshuhudia ulipwaji wa mikopo ya Serikali ya Awamu ya Kwanza, Serikali ya Awamu ya Pili, ni mikopo ya muda mrefu, kwamba mradi ambao ulianzishwa na Serikali ya awamu ya kwanza tungeamua kulipa kwa mapato ya mwezi ndio ingetakiwa sasa hivi mradi mmoja uwe unamalizika leo, kwa hiyo inamalizwa kwa mara moja, lakini inabaki deni inalipwa kidogo kidogo kwa sababu mapato tuliyakusanya hivi.

Mheshimiwa Spika, asilimia tano ni mikopo ya nchi kwa nchi ambayo na yenyewe ni kama ile ile ya *multilaterals* ambayo ni midogo. Kwa zaidi ya 72% ya deni la Taifa ni ile mikopo ya muda mrefu ambayo riba yake ni ya chini takribani 23% mpaka 24% ndio ile ambayo inaangukia kwenye mikopo ya kibiashara na yenyewe ni kwenye maeneo mahususi sana.

Kwa hiyo, niliona nilisemee na hili kwamba ni jambo ambalo ni la msingi sana la kusisitiza mapato na wakati Mheshimiwa Kasalali, anaongea nikasema kule jimboni kwako kama kura zinapungua pungua kwa sababu wapiga kura wangu wapo hapa na wamenihakikishia nikatamani kama inawezekana kugawia tukugawie kidogo ili urudi utoe hoja za msingi hizo za kibunge na za kizalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wameongea na Waheshimiwa Wabunge wengine kama nilivyosema pamoja na Mheshimiwa Kingu, ambaye kaongea vizuri sana tumepokea hoja hizo; Mheshimiwa Hasunga kaongea vizuri sana tumepokea hizo hoja; Mheshimiwa Balozi wetu Mheshimiwa Subira kaongea vizuri sana tumepokea hoja hizo; Mheshimiwa Kandege ndio nilikuwa nafafanua tumepokea hizo hoja tutazifanyia kazi; pamoja na Balozi wetu aliyechangia mwanzoni pale mama Mheshimiwa Riziki Lulida, *my best* umechangia vizuri hoja zako tumezipokea na hili ambalo alikuwa analimalizia Mheshimiwa Kingu, la ndugu yetu Mtanzania na shughuli anayofanya tumelipokea na tutateta vizuri tuone ni kitu gani ambacho kinaweza kikafanyika, tutashukiriana na sekta

pamoja na *Foreign Affairs* tuone ni kitu gani kinachotakiwa kufanyika ili tuweze kufanikisha jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona kengele ya kwanza imeshagongwa nitumie fursa hii tena kuwashukuru Wabunge wote tumepokea hoja zenu, nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad, *MCC* - Mjumbe wa Kamati Kuu nakupongeza sana. Mheshimiwa Naibu Waziri ni Naibu Waziri wa viwango vya Wizara ya Fedha, Naibu Waziri wa viwango vya Hazina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri huyu amejaliwa hekima sana, amejaliwa ushirikishaji mzuri sana na Mheshimiwa Naibu Waziri mara zote hata ninapokuwa kwenye vikao vile vya lazima ambavyo kuna wakati nalazimika kuwa kwenye vikao vile hata wakati Bunge linaendelea ama Kamati zinaendelea huwanakuta ameweza kushirikiana vizuri na Kamati na ndiyo maana kwa kweli hata mara zote hata nisipokuwepo ni kama nipo tu kwa sababu Naibu Waziri anafanya kazi nzuri na tuwaombe wapiga kura wa Kojani waturudishie Naibu Waziri wetu, kazi anaiweza na anaifanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na kama walivyosema wengine, ili nisimtaje Mbunge mmoja mmoja kuwaomba wananchi wake waturudishie, nitumie tu fursa hii kuwaomba wananchi wa Uyole wakurudishe na Wabunge wako wote ili kuweza kumalizia hii kazi ambayo iliyokuwa inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamefanyaka kazi nzuri Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, Wana-Uyole waturudishie Spika wetu, waturudishie dada yetu anafanya kazi nzuri na wawarudishe Wabunge wote ambao kwa kweli wameshiriki kwenye shughuli hizi zote ambazo rekodi za maendeleo ambazo zimekuwa *recorded* katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri. Sasa Waheshimiwa, muda wetu umekwenda, lakini tunakaribia kumalizia hoja hii. Kwa hiyo, tunaendelea kidogo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi. Katibu. *(Makofi)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 001 – Deni la Serikali**

Kifungu 1001 – *Administration*……....................……Sh. 14,219,350,702,000

**MWENYEKITI:** Hebu soma upya.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1001 – *Administration*……....................……Sh. 14,219,350,702,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

Kifungu 1002 – *Fiance anc Accounts Unit* shilingi....

**MWENYEKITI:** Ngoja Katibu. Waheshimiwa Wabunge, tutapitisha kwa mafungu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

Kifungu1002 - *Finance and Accounts Unit* …...........Sh. 5,330,642,560
Kifungu 2001 – *Quality Assurance*…..………….……Sh. 1,567,750,000
Kifungu 2002 – *Technical Audit*…………….............Sh. 2,188,530,000
Kifungu 2003 – *Local Government Authorities Audit*................................Sh. 1,627,140,000
Kifungu 2004 – *Ministries, Independent Departments and Audit*……....…………….....……Sh. 2,165,330,000
Kifungu 2005 – *Risk Management Systems and Controls*…….........….……………………Sh. 917,548,440

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Business Support Division*…...............Sh. 3,416,515,000
Kifungu 1002 – *Internal Audit Unit* ……….....………Sh. 188,309,000
Kifungu 1003 – *Finance and Account Unit*…..............Sh. 372,700,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit*……............................Sh. 60,849,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 206,541,000
Kifungu 2001 – *Technical Department*….....................Sh. 663,565,000
Kifungu 2002 – *Zanzibar Office*…………..…….....….Sh. 201,550,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 013 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Unit*............................Sh. 3,029,843,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 100,360,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*................................Sh. 107,600,000
Kifungu 1004 – *Monitoring and Analysis Unit*………… Sh. 344,180,000
Kifungu 1005 – *Compliance Unit*…..............................Sh. 304,660,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*..........Sh. 64,870,000
Kifungu 1007 – *Legal and International Coordination Unit*……….............................................……Sh. 792,150,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*....................................Sh. 209,740,000
Kifungu 1009 – *Planning Unit*……….…….................…Sh. 209,040,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 021 – Hazina**

Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*............Sh. 2,738,640,000
Kifungu1003 - *Finance and Accounts-Debts Services* ..............................................Sh.1,050,630,000
Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unity (PPU)*.........................................Sh. 3,611,532,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*.......Sh. 850,874,044,000
Kifungu 2002 – *Policy Analysis Division*...................Sh. 806,901,701,000
Kifungu 4001 – *External Finance Division*.................Sh. 74,028,467,500
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unity*......Sh. 11,924,621,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*..............................................Sh. 7,726,640,500
Kifungu 6001 – *Debt Management Division*.............Sh. 9,986,364,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001 – *Consolidated Fund Services*…………Sh. 892,502,874

Kifungu 3002 – *Expenditure Management*……......Sh. 38,629,297,000
Kifungu 3003 – *Financial Management*…………...Sh. 39,270,380,156
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*……..................................……Sh. 10,880,112,970
Kifungu 3005 – *Sub Treasury Arusha*……….................……Sh. 422,670,000
Kifungu 3006 – *Sub Treasury Coast*…........................……Sh. 244,100,000
Kifungu 3008 – *Sub Treasury Iringa*…….........................…Sh. 252,195,000
Kifungu 3009– *Sub Treasury Kagera*……….................……Sh. 270,115,000
Kifungu 3010 – *Sub Treasury Kigoma*………................……Sh. 292,930,000
Kifungu 3011 – *Sub Treasury Kilimanjaro*……………..…….Sh. 252,770,000
Kifungu 3012 – *Sub Treasury Lindi*…….........................……Sh. 283,440,000
Kifungu 3013 – *Sub Treasury Mara*…….........................……Sh. 253,280,000
Kifungu 3014 – *Sub Treasury Mbeya*……........................……Sh. 243,690,000
Kifungu 3015 – *Sub Treasury Morogoro*……………......……Sh. 305,630,000
Kifungu 3016 – *Sub Treasury Mtwara*……........................…Sh. 244,162,500
Kifungu 3017 – *Sub Treasury Mwanza*……....................……Sh. 243,520,000
Kifungu 3018 – *Sub Treasury Rukwa*……........................……Sh. 243,650,000
Kifungu 3019 – *Sub Treasury Ruvuma*……......................……Sh. 321,750,000
Kifungu 3020– *Sub Treasury Shinyanga*…………….........Sh. 242,820,000
Kifungu 3021 – *Sub Treasury Singida* ……......................Sh. 243,960,000
Kifungu 3022 – *Sub Treasury Tabora*……........…………….Sh. 239,320,000
Kifungu 3023 – *Sub Treasury Tanga*……..…....………..…Sh. 266,165,000
Kifungu 3024 – *Sub Treasury Manyara*…………….........Sh. 293,310,000
Kifungu 3025 – *Sub Treasury Njombe*……….....………….Sh. 296,980,000
Kifungu 3026 – *Sub Treasury Geita*………….........…..…Sh. 333,660,000
Kifungu 3027– *Sub Treasury Katavi*………..……………Sh. 243,800,000
Kifungu 3028 – *Sub Treasury Simiyu*………...................Sh. 271,260,000
Kifungu 3029 – *Sub Treasury Songwe*………………..…Sh. 241,270,000
Kifungu 3030 – *Sub Treasury Dar es Salaam*……......…Sh. 407,870,000
Kifungu 4001 – *Local Government Finances*…........Sh. 1,282,270,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*…...........………Sh. 1,125,433,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Haya Waheshimiwa Wabunge, tutarejea Fungu 22 kwa hiyo, tunapitisha kwanza 23. Haya, rejea Fungu Namba 22.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 022 – Huduma za Mfuko Mkuu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…………………..…Sh. 3,147,920,108,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Samahani haijaingia kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge, ahsante sana.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*……………..Sh. 16,968,058,390
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…..........Sh.1,771,752,000
Kifungu 1003 – *Internal Audit Unit*….............................Sh. 575,927,440
Kifungu 1004 – *Ministerial Audit Division*..................Sh.14,301,749,000
Kifungu 1005 – *Local Government Authorities Division*………………...………………Sh. 25,872,952,181
Kifungu 1006 – *Performance Audits Division*…..........Sh. 7,789,558,229
Kifungu 1007 – *National Account Division*................Sh. 8,485,285,000
Kifungu 1008 – *Technical Support Service Unit*…......Sh. 8,969,311,600
Kifungu 1009 – *Public Authorities Audit Division*……Sh. 7,859,862,000
Kifungu 1010 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*…………………...…………..Sh. 2,720,860,400
Kifungu 1011 – *Procurement Management Unit*……Sh. 880,273,400
Kifungu 1012 – *Information and Communication Technology Unit*...............................Sh. 4,374,400,610
Kifungu 1013 – *Forensic Audit Unit*……….....………Sh. 5,187,508,750
Kifungu 1014 – *Quality Assurance Unit*……..............Sh. 1,414,565,000
Kifungu 1015 – *Government Communication Unit*….Sh. 706,036,000
Kifungu 1016 – *Risk Management and Compliance Unit*……………………………………………Sh. 270,100,000
Kifungu 1017– *Legal Services Unit*….........................Sh. 1,028,743,000

Kifungu 1018 – *Parliamentary Coordination Unit*.....Sh. 1,238,180,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 050 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.................Sh. 14,901,683,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.............Sh. 2,428,537,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…........................Sh. 114,294,529,000
Kifungu 1004 – *Legal Services Unit* ……………..........Sh. 3,034,276,000
Kifungu 1005 – *Government Communication Unit*..Sh. 2,376,027,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*….........................Sh. 1,643,564,000
Kifungu 1007 – *MCC Tanzania*……..…………….......Sh. 2,076,065,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*…..Sh. 2,475,008,000
Kifungu 1011 - *Monitoring and Evaluation Unit*….....Sh. 2,823,088,000
Kifungu5001 – *Government Asset Management Division*…….……………………….…….Sh.12,580,245,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*………………………Sh.10,950,392,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR– KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 006 – Idara ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali**

Kifungu 2001 – *Quality Assurance*…………….….......Sh. 175,750,000
Kifungu 2002 – *Technical Audit*……………….............Sh. 473,587,000
Kifungu 2003 – *Local Government Authorities Audit*………………………………………Sh. 177,260,000
Kifungu 2004 – *Ministries, Independent Departments and Audit*…………………………………Sh. 185,100,000

Kifungu 2005 – *Risk Management Systems and Controls*……………………………Sh. 266,700,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 010 – Tume ya Pamoja ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Business Support Division*……………..Sh. 958,949,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 021 – Hazina**

Kifungu 1009 – *Public Procurement Policy Unit (PPU)*……………..........…………..Sh. 1,000,700,000
Kifungu 2001 – *Government Budget Division*.......Sh. 578,284,090,800
Kifungu 2002 - *Policy Analysis Division*.....................Sh. 85,703,712,600
Kifungu 4001 – *External Finance Division*..................Sh.10,807,420,000
Kifungu 4002 – *Public Private Partnership Unity*....... Sh. 5,853,453,000
Kifungu 5001 – *Financial Sector Development Division*.............................................Sh. 12,644,720,600
Kifungu 6001 – *Debt Management Division*............Sh. 1,137,940,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko ya Serikali)*

**Fungu 023 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali**

Kifungu 3001 – *Consolidated Fund Services*…………Sh. 215,880,000
Kifungu 3002 – *Expenditure Management*…..............Sh. 125,200,000
Kifungu 3003 - *Financial Management*…..................Sh. 2,968,631,500
Kifungu 3004 – *Financial Operations and Standards*……………………………..…Sh. 2,721,120,500
Kifungu 4001 – *Local Government Finances*…...........Sh. 527,340,000
Kifungu 7001 – *Pension and Gratuity*…………………..Sh. 273,290,000
*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 045 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management Division*…………….….Sh. 7,712,090,000
Kifungu 1010 – *Planning, Monitoring and Evaluation Division*……………………….……Sh. 4,391,906,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 050 – Wizara ya Fedha**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……………Sh. 2,800,000,000
Kifungu 1003 – *Planning Division*…..........................Sh. 41,581,220,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…...........................…Sh. 600,000,000
Kifungu 1011 – *Monitoring and Evaluation*…………..Sh.1,092,600,000
Kifungu 5001- *Government Asset Management Division*…………………………….……Sh. 2,065,988,000
Kifungu 6001 – *Financial Management Information Systems Division*………………………Sh. 5,147,752,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa Hoja, Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) cha Kanuni ya Kudumu ya Bunge Toleo la Februari mwaka 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge zima.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji Wabunge hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Wote mmeafiki, ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya nyinyi kuhojiwa na wote kukubali, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kuwa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yamepitisha Rasmi na Bunge na pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa wasilisho la hoja hii lakini pia kwa namna michango hii ambavyo imeenda siku ya leo siyo jambo la kawaida sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunakupongeza Mheshimiwa Waziri, naamini ni hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa ambazo zimewaridhisha Waheshimiwa Wabunge hawa kupelekea michango hii. *(Makofi)*

Pia nimpongeze msaidizi wako wa karibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kukusaidia na kama ulivyosema wewe na sisi Wabunge tunaungana na maneno uliyoyasema kuhusu yeye, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia watendaji, baadhi ya watendaji wametajwa hapa na Waheshimiwa Wabunge lakini tunawapongeza watendaji wote wa Wizara hii kwa sababu ndiyo wanawezesha mambo mengi kwenda vizuri. Sasa leo muda wetu umeenda kidogo siku ya kusema kuhusu bajeti ile ya Serikali basi tutapata nafasi ya kuwapongeza kila mmoja wao na kwa kweli kwa ujumla kwa siku ya leo wachukue maneno haya kwamba tunatambua kazi yao kubwa wanayoifanya, tunatambua kujitoa kwao, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana kwa ajili ya Taifa letu na yale ambayo Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imeyasema hapa tunaamini mtaendelea kuyafanyia kazi kwa sababu na wao wamekiri kwamba mnatoa ushirikiano mzuri sana, na katika kipindi hiki mtaendelea ushirikiano na Kamati hii. Kwa hiyo, tunawatakia kila la heri katika siku hizi za mashauriano lakini baadaye itakaposomwa Bajeti Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nadhani wote tunaungana pamoja kuipongeza na kuishukuru Kamati yetu ya Bajeti; Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, lakini na Kamati nzima kwa kuendelea kufanya kazi usiku na mchana hasa katika kipindi hiki na tunawatakia kila la heri na tunawategemea kwa zile hatua zinazofuata baada ya hapa. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, basi naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 8.14 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 5 Juni, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*